ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tatu – Tarehe 19 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 2

Ujenzi wa Kituo cha Askari barabara ya Regeza Mwendo - Bububu

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Ukiacha Kituo cha Polisi cha Bububu hakuna tena kituo cha polisi kuanzia Bububu/Dole hadi Regezamwendo. Hali hii sio tu kwamba inapelekea uhalifu katika maeneo hayo, lakini pia barabara hii hutumika sana kama njia ya panya kwa madereva wa gari za mchanga wanaokwepa majukumu yao ya kisheria.

(a) Kwa kuwa wizara inalifahamu hili, ni hatua zipi ilizozichukua ili kuweka Kituo cha Polisi maeneo hayo kwa lengo la kupunguza uhalifu?

(b) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba barabara hii hutumiwa sana na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ambae pia Naibu Waziri Kiongozi na hivyo kukosekana kwa askari wa usalama barabarani huenda ikapelekea uhalifu usiotarajiwa?

(c) Kwa kuzingatia ufahamu huo je, wizara imekusudia lini itaanzisha ujenzi wa Kituo cha Polisi katika barabara hii kwa lengo la kuepusha uhalifu na kuimarisha usalama wa raia wetu?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kweli ukiacha kituo cha Polisi cha Bububu, hakuna tena kituo cha Polisi kuanzia Bububu, Dole hadi Regezamwendo, lakini nia ipo ya kujenga kituo katika eneo hilo hasa kwenye makutano ya barabara. Lakini Jeshi la

Polisi kwa wakati huu linawajibika kuhakikisha usalama wa eneo husika unakuwepo, kwa kuweka askari kwa muda wote katika maeneo hayo.

(b) Najua Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ambaye pia ni Naibu Waziri Kiongozi huwa anaitumia barabara hii ndio maana kila wakati askari wa trafiki hawakosekani kulinda usalama katika eneo hilo.

(c) Katika mchakato wa kuboresha Jeshi la Polisi, tumekusudia kujenga kituo kwenye eneo husika mara tu hali ya fedha itakapokuwa nzuri.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. pamoja na majibu yake mazuri ni kwamba ukianzia njia ya Bumbwini mwisho wa njia kuna kituo cha polisi, lakini ukitoka hapo mpaka Bububu hakuna kituo cha polisi. Lakini watu wa shehia wamejenga kituo kidogo cha polisi sehemu ya Nyumba ya Ndege lakini muda mwingi hawajatulia. Je, hilo analijua. Kama hakijatumiwa kina tatizo gani kisitumiwe?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kituo hicho cha polisi kilichojengwa na wananchi ni kweli kipo na hakijatumika, lakini kupitia swali lake Mhe. Mwakilishi naahidi kuanzia sasa hivi kituo hicho tutakifanyia kazi ili kianze kazi mara moja. ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

(a) Mhe. Waziri, tunaamini wananchi hivi sasa wameimarika na wako tayari kujenga vituo vya polisi kwa ajili ya usalama wao. Kwa kuwa Jeshi la Polisi au wizara inayohusika haijawa tayari katika kuelekea huko, wizara ina mpango gani kwa makusudi kuwahamasisha wananchi kuanza ujenzi wa kituo hicho ili wawe tayari?

(b) Katika hiyo nyumba inayozungumzwa hapa kuwa ni nyumba ya ndege, inasemekana kwamba nyumba hiyo ukilala unapigwa bakora. Je, hili nalo Mhe. Waziri analijua?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunisaidia ufafanuzi kusema kwamba bakora ni fimbo. Mhe. Spika, nakubaliana na hoja ya Mhe. Ali Suleiman kwamba Jeshi la Polisi pale ambapo hatujakuwa tayari kujenga kituo na hatujakuwa na uwezo wa kujenga

kituo, kama wananchi wanahisi iko haja hasa katika kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo pia na wao kupitia kwa viongozi wao katika eneo hilo kama kwa sheha, wanaweza wakajenga kituo cha polisi. Wananchi wengi wameshafanya hivyo katika maeneo mbali mbali. Kwa mfano, Mkunazini kuna kituo cha polisi ambacho wananchi wema walijenga lakini hata hivyo, kuna maeneo mengine mbali mbali.

Kwa hivyo, bado tunakubali maombi ya wananchi kujenga vituo vya polisi, lakini kitu tunachokiomba kabla ya kujenga kituo hicho, kwanza waje kwetu washauriane na sisi ili kuangalia vile vigezo ambavyo vinasababisha kujengwa hivyo vituo vya polisi. Kwa sababu sio kila pahala panaweza kuhitaji kuwekwa kituo cha polisi, lakini vile vile na kuangalia usalama wa kile kituo. Kwa sababu vituo vidogo kama hivi vinatakiwa zaidi navyo viwe katika hali nzuri ya kiusalama. Sasa lazima washirikiane na sisi katika kuangalia yale maeneo ambayo wanakusudia kujenga vituo hivyo, lakini tuko tayari kushirikiana nao.

Swali lake la (b) ni suala la nyumba ya ndege. Nyumba ya ndege haipo lakini hicho kituo kimejengwa katika hilo eneo ambalo linaitwa Nyumba ya Ndege. Suala la kulala watu kuwa wanapigwa bakora hili tutalifanyia kazi na kama yupo huyo mtu anayepiga bakora basi serikali itaweza kumshughulikia mara moja.

Mhe. Spika: Katika mashirikiano ni pamoja na kuona maeneo ambayo yako salama kwa bakora. *(Kicheko)*

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza. napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba, kwa kuwa mara nyingi baadhi ya gari za mizigo kama vile michanga, mawe na hata matunda, huwa yanatumia njia hii kama *panya road***.** Wakati huo huo kuna wakati wakipita mle kwenye vituo vya kawaida huwa gari hizi zinalipa kodi mbali mbali. Haoni ukosefu wa kuweko na vituo katika barabara hii kunanyima kuipatia mapato serikali na Idara ya Mapato. Je, ana mpango gani wa kuhamasisha Bodi ya Mapato ili waweko kule njiani na kupata mapato ya zile gari zinazokwepa mapato?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kama nilivyojibu swali la msingi kwamba pamoja na eneo hilo alilolitaja kwamba hapana kituo cha polisi karibu, lakini ukiangalia Mhe. Spika, katika maeneo hayo muda mwingi tunawaweka askari wa trafiki katika kuhakikisha kwamba hayo anayoyazungumza Mhe. mjumbe wenye magari kukwepa kulipa kodi ili wapate kukimbia. Kwa hivyo, tunawaweka askari kwa muda mwingi katika maeneo hayo.

Vile vile ukitoka katika maeneo hayo kabla ya kufika mjini, kwa sababu kama ukitoka njia ya ndani ya Regeza Mwendo lazima utakutana na kituo kidogo cha polisi kilichokuweko Mtufaani pale. Kwa hivyo, bado dereva hana njia ya kukimbia asikutane na kituo cha polisi hivyo usalama upo wa kutosha.

Lakini vile vile suala la kusema kwamba serikali inakosa mapato na labda kuishauri *ZRB* wende wakakae kule. Mimi nadhani *ZRB* wao hawakusanyi mapato kama haya ya gari zinazopita na mizigo. Taasisi inayohusika na kukusanya kodi hizi ni Idara ya Misitu na Mazao ya Baharini. Wenzetu wa Idara ya Misitu wanawaweka wafanyakazi wao katika maeneo mbali mbali hata kama hapana kituo cha polisi lakini wao wakati mwengine wanaweka *road block* kwa ajili ya kuangalia ile mali asili yote inayovunwa ili ile kodi iweze kupatikana. Kwa hivyo, suala hili ni la Maliasili sio la *ZRB* na wanafanya kazi zao vizuri katika kukusanya hizi kodi kwa hao madereva wanaobeba maliasili.

Nam. 26

Mikopo ya Benki

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:

Naipongeza serikali kupitia tawi lake la Benki la Chake Chake Pemba tangu kuanzishwa fursa ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi mwaka 2002. Tawi la Chake Chake hadi kufikia Juni, 2009 tayari limeshatoa mikopo yenye thamani ya Tshs. 4.49 Billioni kwa wateja wapatao 6,067. Pia katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Machi, 2009 tawi limeweza pia kukopesha wafanyakazi 5,789 mikopo yenye thamani ya Tshs. 4.11 Bilioni.

(a) Je, Mhe. Waziri katika mikopo hiyo iliyotolewa benki inapata faida ya kiasi gani?

(b) Kwa kuwa Kisiwa cha Pemba kina miji mitatu (3) Mkoani, Chake Chake na Wete lakini tawi lipo Chake Chake tu. Je, kuna mpango wowote wa kuweka (*ATM*) kwa Mkoani na Wete ili kuwapunguzia usumbufu wateja?

(c) Katika kupunguza wizi wa mishahara wenzetu Tanzania Bara wanalipa mishahara kupitia benki. Je na sisi serikali yetu ina mpango kama huo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 26 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi naomba kufanya marekebisho madogo kwenye takwimu alizoulizia swali.

Mhe. Spika, tokea Benki ya Watu wa Zanzibar kutoa fursa ya mikopo kwa wafanyakazi wa serikali mwaka 2002 hadi kufikia mwezi June mwaka 2009, Tawi la Chake Chake limeshatoa mikopo yenye thamani ya Shs. 10.077 bilioni sio bilioni 4.49, tumekwenda zaidi ya hapo mara mbili ya hapo.

Pia idadi ya wateja nayo imeongezeka kutoka ile iliyosemwa pale 6,067 hadi kufikia wateja 10,109. nafikiri lazima tuwapongeze watu wa Chake Chake kwa hatua nzuri sana wanayoitumia au benki inayotoa na wao wanaitumia vizuri.

Aidha, katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia mwezi wa Machi, 2009 Tawi la Chake Chake limetoa mikopo yenye thamani ya Shs. 1.126 bilioni kwa wafanyakazi wapatao 603.

Baada ya marekebisho ya takwimu hizo Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika mikopo iliyotolewa na benki tokea kuanzia mwaka 2002 hadi kufikia mwezi wa Machi, 2009, benki imepata faida ya Shs. 2.131 bilioni.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyolieleza Baraza lako Tukufu hivi karibuni, kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar Limited ina mpango wa kufungua vituo vya huduma katika maeneo tofauti ikiwemo miji ya Wete na Mkoani kwa lengo la kusogeza huduma zake kuwa karibu zaidi na wananchi.

(c) Mhe. Spika, kwa kuanzia serikali tayari imeshaanzisha utaratibu wa kulipa mishahara ya wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Benki yake ya Watu wa Zanzibar kama nilivyosema kwa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ili kama *pilot project* kwa lengo la kuangalia ufanisi wake kabla ya kuanza kutumika kwa wafanyakazi wake wote wa serikali.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. kwanza na mimi niwapongeze watu wa Benki kutoa kiasi hicho cha mikopo ambacho kimeweza kuwanyanyua wananchi au wafanyakazi kimaisha. Lakini katika mikopo huwa kuna marejesho, katika tarehe ambayo imetajwa hadi sasa ni marejesho ya kiasi gani yamesharejeshwa na wakopaji hao?

Kwa kuwa utaratibu wa kutoa mikopo au utaratibu mzima wa mtaji wa benki huwa unasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Hivyo, Mhe. Waziri haoni kiwango kilichotajwa kwa kutoa mikopo kwa upande wa Pemba tu kwamba Benki Kuu inaweza ikawa na wasi wasi wa mtaji uliobakia katika benki hiyo ambayo imetajwa yaani PBZ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa kweli ametaka takwimu marejesho ni kiasi gani kinachorejeshwa, kwa kweli sikujitayarisha kwa hizo takwimu. Lakini ninachoweza kuthubutu kusema kwamba marejesho ni mazuri, kwa sababu wengi wa wafanyakazi wanaokopa tunawakata moja kwa moja kwenye mishahara yao kwa hivyo, kumefunguliwa utaratibu wa *account* kule, pesa za mishahara zinaingia kwenye *account* na wao wanakatwa kwenye *account*. Utaratibu huo unakwenda vizuri kabisa.

Wale wengine sote tunajua benki yetu ilivyokuwa kali siku hizi kwa wale ambao hawarejeshi mikopo. Nafikiri sote tunajua kazi aliyokuwa anaifanya Caravan ya kunadi mali zao. Kwa hivyo, nashukuru sasa hali imetulia na wengi wana-*comply* kwa masharti yale ya mikopo hatuna tatizo kubwa lililojitokeza. *Alhamdulillahi* kama nilivyosema basi akianza mtu tunamtanabahisha, bwana wee tunaomba mkopo wako urejeshe kama inavyopaswa kabla ya hatua kali hazijachukuliwa.

Kuhusu wasi wasi wa mtaji wa benki kama ilivyoshauriwa na Benki Kuu, naomba kumhakikishia Mhe. Ame Mati kwamba hakuna wasi wasi wowote. Kwa sababu kile kiwango cha *minimum* cha mtaji kuwepo cha bilioni tano sisi PBZ tumeshakivuka, tuko wazuri tu na tunaendelea vizuri.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. kwanza tunawapongeza wenzetu wa Benki ya Chake Chake kwa kutoa fedha nyingi kwa wateja wao. Swali, je, Mhe. Waziri katika mikopo hii ya bilioni 10.109 imo na mikopo ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Amani Abeid Karume?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, hapa itabidi tukatofautishe lakini ninachofahamu zile ni pesa mbali kabisa, nafikiri sio *inclusive* pesa zile, hizi ni nyengine kabisa utaratibu wake mwengine. Nathubutu kusema kwamba hazimo hizi.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Katika majibu ya msingi alieleza kuwa katika Miji ya Chake Chake na Wete wataanzisha utaratibu wa kutoa njia maalum ili kuwarahisishia wananchi wa huko juu ya upatikanaji wao wa fedha. Katika suala huku kuna Kisiwa cha Pemba kina miji mitatu Mkoani, Chake Chake na Wete na kuna huduma ya *ITM*. Lakini hivi karibuni Tanzania Bara tulisikia katika vyombo vya habari kumezuka wimbi la baadhi ya watu kuiba fedha kupitia mitandao hii ya *ITM*.

Je, hapa Zanzibar kuna usalama wowote wa fedha uliowekwa za wananchi ili wizi huu usije ukafanyika na wananchi wakapata hasara pamoja na benki?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni majambazi wamekuwa wanavihujumu vituo hivi vya utoaji pesa vya *ITM* hata kufika kuvivunja kwa minajili ya kupata pesa. Mtizamo wetu sisi kwamba vituo vile tuviweke mahala penye ulinzi *maximum security.* Utakuta kwa mfano *PBZ* penyewe kule Forodhani tumeviweka nje kidogo tu lakini kwenye ulinzi wa askari pale. Hata *NBC* nao wameweka mahala penye ulinzi.

Hivi sasa tunafungua jengo la Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira *Sonara Building* pale napo wapo na wenzetu. Kwa hivyo, tunahakikisha angalau kwa kuanzia tunaweka mahala penye *maximum security* tena huyo atakaekuja akivunja pale tena huyo…, lakini ndio mwizi. Kwa hivyo, ushauri wake Mheshimiwa tumeupokea kwamba tujitahidi kuchukua indhari ili majanga haya na sisi yasitutokezee.

Nam. 11

Taa za Trafic lights katika Barabara ya Kariakoo

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Mhe. Waziri Mji wa Zanzibar ni mji pekee ulimwenguni kuwa na *Trafic Lights* mbili (ya Malindi na Mkunazini Unguja).

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuzingatia umuhimu wa taa hizi, unafikiri kitu gani kinakwamisha kuwekwa taa hizi katika makutano ya barabara eneo la Barabara ya Kariakoo Unguja?

(b) Hivi hizi taa mbili zilizopo katika eneo la Mkunazini na Malindi zimepatikana vipi?

(c) Mhe. Waziri huoni kuwa ipo haja ya kuwekwa taa hizi maeneo yote ya makutano ya barabara hususan sehemu za *"keep left"*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya S.M.Z – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ni muhimu kuwekwa taa za kuongoza magari (*Traffic lights*) katika makutano ya barabara eneo la Kariakoo Unguja. Lakini kilichokwamisha kuwekwa kwa taa hizo ni kutokuwa na uwezo wa kifedha kwa sasa wa kununulia taa hizo.

(b) Taa mbili zilizopatikana katika eneo la Mkunazini na Malindi zimepatikana kwa msaada wa Jumuiya ya Alyouseif kutoka Saudi Arabia (*Al-youseif Charitable Society*).

(c) Nakubaliana na wazo la Mhe. Mwakilishi kuweka taa hizo katika maeneo yote ya makutano ya barabara hali ya fedha itaporuhusu.

Mhe. Ame Ussi Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. kama hizi taa ziliopo zimepatikana kwa misaada kutoka huko alikokutaja. Je, kwa sehemu hizi nilizozitaja hawezi akaomba tena misaada hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya S.M.Z: Mhe. Spika, ushauri wake ni mzuri, lakini hata hivyo ni vizuri uweze kujitegemea mwenyewe badala ya kupita ukawa unaomba omba.

Mhe. Said Khelef Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Hivi sasa tunazo taa mbili za

Mkunazini na Malindi. Je, kuna sababu zipi kuwa taa zile zinakaa muda mrefu hazijatengenezwa?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya S.M.Z: Mhe. Spika, kwa kweli tunahitaji mafundi wa kutengeneza maeneo hayo. Sehemu ya Malindi na Mkunazini tatizo ni kwamba fedha na fedha hizo zinatokana na upatikanaji wa kompyuta ambayo ndio inayoweza kuongoza magari katika maeneo hayo. Kwa hivyo, ule uwezo wa kupatikana kompyuta utapokuwa mzuri ndio tatizo hili tunaweza kuliondoa.

Mhe. Fatma Abdulla Tamim: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri naomba kumuuliza kwani hizi taa zina gharama za kiasi gani zisizoweza kununuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hata ikawa wanatafutwa wafadhili wa kuombaomba?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya S.M.Z: Mhe. Spika, bei hasa kwa kipindi hiki siwezi nikakupa hasa, lakini naweza nikafanya utafiti wa kutosha ili kukupatia hesabu ambayo ni ya uhakika na iliyo sawa.

Nam. 67

Matumizi ya Eka Tatu

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:

Baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 Rais wa Kwanza Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aligawa eka tatu kwa wananchi wake ili walime na ziwasaidie kimaisha lakini hivi sasa kumezuka wimbi kubwa la kutolewa maeneo makubwa kuanzia Eka kumi, sita hadi nne katika maeneo mbali mbali hasa Kijichi, Selem, Kama na kadhalika. Isitoshe Eka hizo nyingine hutolewa katika maeneo wanayoishi watu kwa muda mrefu na huleta usumbufu mkubwa na kukosa raha ya kuishi kwa wasiwasi.

(a) Je, Mhe. Waziri kadhia hii unaifahamu?

(b) Hawa wananchi wa kawaida wanaopewa eka zaidi ya tatu huomba kwa matumizi gani?

(c) Je, Mhe. Waziri unajua kuwa baadhi ya waliopewa eka hizo wanavuruga mazao ya watu bila ya kulipa fidia. Je, hiyo ndio haki?

Nam. 67
Matumizi ya Eka Tatu

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 Rais wa Kwanza Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aligawa eka tatu kwa wananchi wake ili walime na ziwasaidie kimaisha. Lakini hivi sasa kumezuka wimbi kubwa la kutolewa maeneo makubwa kuanzia eka nne, sita hadi kumi katika maeneo mbali mbali hasa Kijichi, Selem, Kama na kadhalika. Isitoshe eka hizo nyengine hutolewa katika maeneo wanayoishi watu kwa muda mrefu na huleta usumbufu mkubwa na kukosa raha ya kuishi kwa wasi wasi.

(a) Je, Mhe. Waziri kadhia hii unaifahamu ?

(b) Hawa wananchi wa kawaida wanaopewa eka zaidi ya tatu huomba kwa matumizi gani ?

(c) Je, Mhe. Waziri unajua kuwa baadhi ya waliopewa eka hizo wanavuruga mazao ya watu bila ya kulipa fidia. Je, hiyo ndio haki ?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye vifungu a, b na c kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iligawa ardhi eka tatu kwa wananchi wake ili zitumike kwa kilimo na hatimaye ziweze kuwasaidia kimaisha. Kwa kawaida madhumuni ya ugawaji wa ardhi hizi kwa wananchi zitumike kwa kilimo tu na sio vyenginevyo na bado msimamo wa Serikali haujabadilika.

Mhe. Spika, napenda ifahamike wazi kwamba eka tatu ni jina ambalo limekuwa likitambulisha ardhi hizi za kilimo lakini ukubwa wa ardhi hizi zinatofautiana kwa mujibu wa Sheria Nam. 12 ya 1992 ya Matumizi ya Ardhi inaruhusu mtu kumiliki Ardhi hadi kufikia eka 20 na zaidi katika ugawaji wa ardhi za kilimo kumekuwa na wananchi waliopata zaidi ya eka tatu bila ya kukiuka sheria.

Mhe. Spika, ardhi hizi huwa hazitolewi kwenye makaazi ya watu na pale uharibifu unapofanyika mpewa anastahiki kwenda kwenye vyombo vya sheria au kufika katika Taasisi inayosimamia ardhi za eka tatu.

(a) Mhe. Spika, kadhia hii ninaifahamu na utaratibu wake ni kama nilivyoeleza kwenye utangulizi wangu.

(b) Mhe. Spika, kwa kawaida ugawaji wa ardhi hizi kwa wananchi zitumike kwa kilimo tu na si vyenginevyo. Kwa hivyo ardhi ikizidi ukubwa wa eka tatu bado matumizi ya ardhi hiyo huwa ni yale yale ya kuendeleza kilimo.

(c) Mhe. Spika, Sheria ya Matumizi ya Ardhi *(Land Tenure Act 1992)* inatoa mwongozo ambapo endapo utamkuta mtu akiwa anaitumia ardhi husika unapaswa kumlipa fidia au kukubaliana na miongoni mwa watumiaji wa ardhi hiyo na endapo ikiwa hilo halitafanyika na uharibifu kutokea ni vyema suala hilo likawasilishwa katika vyombo vya Sheria ili ichukue mkondo wake. Mwongozo wa Sheria pia uko wazi juu ya umiliki wa ardhi, uvamizi wa ardhi kwa upande wa mwananchi wa kupanda vipando na baadae kudai ni eneo lake nao haukubaliki.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Nia ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ni kugawa ardhi kwa eka tatu tatu ili kila mtu apate ardhi hizo.

Lakini Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba kwa ardhi ya wakulima mtu anayo haki ya kupata hata eka 20. Je, hii ni sheria gani yenye usawa kwamba wengine wapate eka 20 lakini wengine nikiwemo mimi hawapati hata eka tatu. Ni utaratibu gani unaotumika wengine wapate wengine wasipate ?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kama nilivyosema, mara baada ya Mapinduzi serikali ilitaifisha mashamba yale tunayoyaelewa na kuyagawa kwa wananchi kwa eka tatu tatu. Wapo wengine hata wakati huo walipata chini ya hapo na wapo waliokuwa wamepata zaidi ya hapo. Kama nilivyosema sheria ile ilikuwa haizuii.

Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba sio sote ambao tutaweza kupata ardhi hiyo. Kwa mfano, kabla ya Mapinduzi idadi yetu ilikuwa ni watu laki tatu, hivi sasa idadi yetu imeongezeka na kufikia watu milioni moja na kidogo, lakini ukubwa wa ardhi yetu uko pale pale haujaongezeka. Kwa hiyo, ni wazi kwamba bado tatizo la ardhi litaendelea kuwepo kwamba wengine wataweza kupata ardhi hiyo, wengine hawatopata, wengine watapata kidogo, wengine watapata kubwa. Lakini ni vizuri wale ambao wamepata kidogo watumie vizuri na wale waliopata kubwa kama mtu ana eneo lake la eka 20 basi anaweza akamuazima mwenziwe kwa kilimo chetu cha kawaida. Kwa sababu wakati mwengine mtu

anaweza kuwa na eka 20 lakini asizitumie zote. Kwa hiyo, anaweza kumuazima mtu mwengine na tunafanya utaratibu huo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nia njema ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume wananchi wake wote waishi kwa uwezo wa kilimo na kila panapostahiki kutolewa eneo litolewe ili wananchi wafaidike.

Kwa mwelekeo huo Mhe. Spika, kuna wananchi wengi katika mashamba mbali mbali walifanya mpango wakakata msitu wakapata maeneo ya ukulima ambao wanaendesha maisha yao zaidi ya miaka 40 hivi sasa kama maeneo ya Nguruweni na kwengineko.

Mhe. Spika, kwa kuwa wananchi hawa walifyeka msitu ule muda mrefu na hivi sasa unawaendeshea maisha yao wao na watoto wao, lakini kuna wajanja fulani wamejitokeza kutaka kupimiwa maeneo yale kwa nguvu ili wananchi wale wahamishwe. Je, Mhe. Waziri analifahamu suala hilo. Kama analifahamu hatua gani za msingi zimechukuliwa ili wananchi wale wasinyang'anywe ardhi yao ?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, hilo silifahamu lakini nashukuru kwamba Mhe. Mwakilishi amenijulisha na ningemuomba basi tushirikiane ili kuona vipi wananchi hao tunawasaidia.

Lakini napenda niseme kwamba fursa ya mwanzo ya mtu anayepewa ardhi ni mfano wa hawa wananchi aliowataja Mhe. Mwakilishi. Kama wamefyeka msitu huo na wakauimarisha basi fursa ya mwanzo ya kupewa ardhi ile ni yule aliyepata kazi ya kuufyeka na kuuimarisha, sio wale kina Mhe. Ali Suleiman Ali na kina Tafana tunaokuja kudandia tu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu lake ameeleza kwamba eka hazitolewi katika maeneo wanayoishi watu.

(a) Je, Mhe. Waziri anafahamu kwamba Meli 10 njia ya Kama kapewa mtu mmoja eka anayejulikana kwa jina la Mzee Khamis katika maeneo wanayoishi watu, akazozana na mtu mmoja akampandisha Mahakamani yule mtu nyumba amevunjiwa na hivi sasa anaishi nyumbani kwangu ?

(b) Mhe. Spika, nguruweni hivi sasa kumeingia tatizo kama hilo wananchi wanalima mazao yao lakini zinapimwa eka halafu wanang'olewa mazao. Je, Mhe. Waziri analifahamu tatizo hilo ?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nataka nikiri hayo siyafahamu. Lakini bado nataka nimshauri Mhe. Mwakilishi kama hilo lipo basi yeye mwenyewe na hao wananchi tukae pamoja tuone vipi tunaweza kusaidiana na wananchi wetu hawa ili wasiadhibiwe bure.

Nam. 13

***Parking* ya Vyombo vya Moto, Hospitali ya Mnazi Mmoja**

Mhe. Ame Ussi Juma - Aliuliza**:-**

Hivi karibuni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeanzisha utaratibu wa kutoza Tsh. 500 kwa magari na Tsh. 200 kwa vyombo vya moto vinavyotumia maringi mawili kwa ajili ya *parking* katika eneo la Hospitali ya Mnazi Mmoja.

(a) Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba *parking* hiyo haijaandaliwa kutoa huduma hiyo kwa kuzingatia ukweli kwamba haijatengwa na kutengenezwa ipasavyo.?

(b) Kwa kuzingatia msongamano wa magari na vyombo vyengine unaopatikana hospitalini hapo na zaidi baada ya kuweka utaratibu huu wa *parking*. Je, haoni kwamba unasababishwa zaidi na kutojiandaa ama kuandaa *parking* ya kisasa ?

(c) Mhe. Waziri, kwa kuwa mapato yanayopatikana kutokana na *parking* hiyo hayakuorodheshwa katika Mswada wa Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa 2009/2010. Je, fedha hizi zinazotozwa kwa ajili ya *parking* hiyo zinakwenda wapi na zinatumikaje ?

(d) Je, kuna mwongozo wowote wa kimaandishi unaoelezea namna ya upatikanaji na utumikaji wa fedha hizi zinazokusanywa kwa huduma hii ya *parking ?*.

(e) Kama upo, Je, kwa kiasi gani haupingani na sheria na kanuni za fedha za mwaka 2005 ?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye vifungu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa hivi karibuni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeanzisha utaratibu wa kutoa Tsh. 500 kwa magari na Tsh. 200 kwa vyombo vya moto vya maringi mawili kwa ajili ya kuegesha *(parking)* katika eneo la hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, sio sahihi kwamba msongamano wa magari na vyombo vyengine unaopatikana hospitalini hapo unatokana na utaratibu wa kuanzisha *parking* hiyo. Itakumbukwa kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja imejengwa wakati ambapo idadi hiyo kwa Wazanzibari ilikuwa chini ya laki tatu wakati sasa idadi hiyo imeongezeka hadi kufikia zaidi ya milioni moja. Aidha, kutokana na kukua hali ya uchumi idadi ya wamiliki wa vyombo vya moto pia imeongezeka lakini eneo la hospitali limebakia vile vile na hata kupungua kutokana na kuongezeka kwa majengo.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa mapato yanayopatikana katika *parking* hiyo hayakuorodheshwa katika mswada wa mapato na matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka huu kwa vile fedha hizo zinaingizwa katika mfuko wa hospitali ambapo mwongozo wa upatikanaji na utumiaji wa fedha hizo ni sawa na ule unaotumiwa katika michango mingine ya Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja (kuweka usafi wa mazingira ya hospitali zetu za Mnazi Mmoja, Mwembeladu na Kidongochekundu).

Mhe. Spika, mpango wa ukusanyaji wa mapato kwa huduma hii unasaidia hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kwa vile unaimarisha mazingira yaliyopo kama bustani na usafi kwa jumla jambo ambalo linaleta haiba kwa wananchi na wagonjwa wanaofika katika hospitali hiyo.

Nam. 23

Ajira ya Walimu

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Kutokana na upungufu mkubwa wa walimu uliojitokeza kwa Wilaya zote nne (4) za Kisiwani Pemba, Wizara ya Elimu imeanza utaratibu wa ajira kwa Wilaya ya Micheweni na Mkoani. Tayari mchakato wa ajira hiyo umeshafanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa Makao Mkuu ya Wizara kwa utekelezaji wake.

(a) Kwa kuwa Wilaya zote za Pemba zina tatizo linalolingana kwa nini Serikali imeamua kutoa ajira kwa Wilaya ya Mkoani na Micheweni pekee ?

(b) Kwa kuwa tatizo kama hilo la upungufu wa walimu pia linaukabili Mkoa wa Kaskazini Unguja. Je, ni lini ajira zitatolewa kwa upande wa Mkoa huu hasa ukizingatia kuwa vijana waliosomea ualimu wapo wengi . ?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa tatizo la uhaba wa walimu linazikumba Skuli za Wilaya zote za Pemba na baadhi ya Wilaya za Unguja. Ni kweli pia hivi sasa mchakato wa kupata Walimu wa kuajiri umeshakamilika.

Mhe. Spika,

(a) Serikali imeamua kutoa ajira za walimu kwa awamu na katika awamu ya kwanza, kwa wilaya za Pemba, ajira zitatolewa kwa skuli za Wilaya ya Micheweni na Mkoani tu. Hatua hiyo imechukuliwa kutokana na wilaya hizo mbili kuwa na upungufu mkubwa wa walimu ukilinganisha na Wilaya za Chake Chake na Wete.

(b) Zoezi kama hilo pia limefanyika kwa skuli za Mkoa wa Kaskazini Unguja na mchakato wa kutambua mahitaji ya walimu katika Skuli za Mkoa huo sasa umekamilika. Maombi ya kuajiri walimu waliopendekezwa yatapelekwa Idara ya Utumishi Serikalini hivi karibuni kwa kupatiwa kibali. Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi na wananchi kwa jumla kuwa Serikali pia inakusudia kuajiri walimu kwa skuli za wilaya zilizobakia kabla ya kumaliza kwa mwaka huu wa fedha.

Nam. 29

Vyuo vya Amali

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza**:-**

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kujenga Vyuo vya AMALI Mkokotoni, Unguja na Vitongoji, Pemba kwa lengo la kuwapa mafunzo vijana wetu katika fani mbali mbali, ili wamalizapo

mafunzo hayo waweze kujiajiri wenyewe na kuipunguzia Serikali tatizo kubwa la ajira katika nchi yetu kwa jumla.

(a) Je, katika mafunzo hayo patakuwepo kwa wanafunzi wa kutwa na dakhalia ?

(b) Kwa kuwa lengo la vyuo hivi kutoa ajira kwa vijana. Je, wamalizapo mafunzo/masomo yao watapata fedha na vifaa vya kuanzia miradi yao?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Vyuo vya Mafunzo ya Amali vilivyoko Mkokotoni, Unguja na Vitongoji, Pemba vimeanzishwa kwa lengo la kuwapatia mafunzo vijana wetu katika fani mbali mbali ili watakapomaliza mafunzo yao waweze kujiariji wenyewe au kuajiriwa na kuchangia katika kupunguza tatizo la vijana wasio na ajira nchini mwetu.

Mhe. Spika,

a) Vituo hivyo vimepokea wanafunzi wa kutwa na wale watakaoishi dakhalia. Vituo vimeshapokea wanafunzi wapatao 350. Baadhi ya wanafunzi wataishi katika dakhalia za vituo mara taratibu zitakapokamilika.

b) Wahitimu wa vituo hivyo ambao watapenda kujiajiri wenyewe watapatiwa mkopo wa fedha wa kununulia zana za kufanyia kazi na mali ghafi baada ya kukamilisha mafunzo ya ujasiri amali.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza naipongeza serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuanzisha vyuo hivi ambavyo vitawapa fursa vijana kupata taaluma na kujiajiri.

Kwa kuwa vyuo ni vingi, vijana kuna ada wanalipa. Je, hawa wanaosoma kutwa watalipa ada kiasi gani na hao wanaokaa dakhalia watalipa kiasi gani kwa mwaka ?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa sababu sikujitayarisha na swali hili nitamletea kwa maandishi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vyuo hivi vinaitwa vyuo vya amali na tayari sasa hivi vimeshafunguliwa.

(a) Je, chuo hiki cha Mkokotoni kina *field* ngapi za kusomesha na kile cha Pemba Vitongoji kina *field* ngapi za kusomesha ?

(b) Kwa kuwa wanachukua mafunzo ya amali. Je, anatuhakikishia kwamba kila ile *field* iliyofunguliwa ina *machinery* na *tools* zake ?

(c) Je, kuna walimu wa kutosheleza kwa hizo *field* zilizofunguliwa katika sehemu hizo za Mkokotoni na Vitongoji.?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika,

(a) Sina uhakika ni *field* ngapi lakini ninavyoelewa ni kwamba kuna *field* mbali mbali zikiwemo za *mechanic*, ufundi friji, ufundi umeme, mambo ya ufugaji na kadhalika. Kwa hivi sasa siwezi kusema ni *field* ngapi lakini namhakikishia kwamba nitampatia hilo jibu.

(b) Mhe. Spika, jengine vifaa vya kutosha hivi sasa vipo na vimeshafika.

(c) Mhe. Spika, kuhusu walimu nalo pia tumejitayarisha vya kutosha katika *field* zote hizo.

Nam. 4

Ununuzi wa Meli ya Serikali

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Bila ya shaka inafahamika kwamba kukosekana kwa meli ya Serikali inayotoa huduma ya bei nafuu kwa wananchi wetu wanaosafiri kwenda Pemba na Tanzania Bara kunapelekea kuwepo kwa usumbufu mkubwa. Wananchi wetu wanalazimika kutumia nauli kubwa kwa kutegemea usafiri wa meli za watu binafsi.

(a) Je, Mhe. Waziri unategemea kipindi gani utanunua meli ya Serikali ili itoe huduma nafuu kwa wananchi wetu ?

(b) Hivi Serikali inafuatilia vipi utendaji wa meli za watu binafsi wanaozitumia vibaya meli zao kujinufaisha binafsi na kuwakandamiza wananchi wetu wanyonge ?

(c) Je, Wizara haioni kwamba ipo haja ya kurejesha tena utaratibu wa kutafuta vivuko vya uhakika na vya kisasa ili kuwasaidia wananchi wetu wanaokaa visiwa vya Tumbatu, Charawe na venginevyo ?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba nia na lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwapatia usafiri bora na wa uhakika wananchi wake bado ipo kama dhamira hiyo ya Serikali ilivyowekwa. Wizara yangu imekuwa katika mchakato wa kulifanyia mabadiliko ya kimiundombinu ya uendeshaji Shirika la Meli ili liweze kutoa huduma bora kwa wananchi wake. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia wizara yangu imejiwekea malengo kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ni kuziuza meli zake chakavu kwa kuanza na MV Mapinduzi na baadaye kununua meli mpya ambazo zitakuwa na uwezo wa kutoa huduma nzuri na za usalama kwa abiria.

(b) Wizara yangu kupitia Afisi ya Mrajis wa meli inazifuatilia meli zote za watu binafsi ambapo imekuwa ikishirikiana kwa karibu na wenye meli ili kupanga kwa pamoja viwango vya nauli, usalama wa abiria na mizigo yao, haki za mabaharia na udhibiti wa nidhamu za wafanyakazi wa vyombo pamoja na matajiri wao. Aidha, ili kuona kwamba mambo hayo yanatekelezwa Wizara yangu kupitia Afisi ya Mrajis wa meli ina utaratibu wa kufanya kikao na wenye meli kila baada ya kipindi cha miezi 3 ili kujadili masuala mbali mbali yanayohusu usafiri wa baharini.

(c) Kwa vile Serikali imeruhusu biashara huria, Wizara yangu haina mpango wa kupeleka vivuko katika visiwa vidogo vidogo isipokuwa inatoa wito kwa wafanyabiashara wa meli kuangalia uwezekano wa kufanya biashara hizo katika visiwa hivi.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameeleza kwamba yupo tayari kujitayarisha kutafuta meli nyengine ili kupunguza haya makero.

Je, anafikiria nini kilichokuwa kinasababisha kuwa meli zikiwa katika Taasisi ya Serikali haziendeshwi kwa mapato na faida. Lakini zikipelekwa katika taasisi binafsi zinafanya kazi kwa faida na hapo hapo taasisi hizo binafsi zinajitangaza redio kifua kuwa baada ya miaka miwili wanafanikiwa kupata meli nyengine.

Je, katika wizara yake anahisi kuna tatizo gani linalosababisha meli hizi za serikali zisifanye kazi kwa faida ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, Shirika letu la Meli limekuwa halipati faida kubwa kwa sababu katika utafiti wetu tumeona kwamba miongoni mwa sababu ni kuwa lina wafanyakazi wengi kuliko mahitaji, pia hivi sasa lina meli chakavu. Ndio maana katika jibu la msingi Naibu Waziri alisema kwamba tunatarajia kuanzisha utaratibu mpya wa ajira katika Shirika la Meli na tayari tumeshaomba Idara ya Utumishi ili kuwe kuna *sign in* na *sign off* kwa ajili ya mabaharia na kuwapunguza wafanyakazi wa ofisini pengine kwa asilimia karibu 40 ili tuendane na wakati.

Sasa hili halitokani na redio kifua isipokuwa utaratibu wa ajira zamani kidogo ulikuwa hauwendi vizuri kutokana na muundo wa shirika. Tunatarajia baada ya muundo huu na kupata meli mpya shirika letu tutafanya kazi kwa faida na kwa misingi ya kibiashara.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri alikiri kwamba Afisi ya Mrajis ndio inayoshughulikia usalama wa meli na abiria.

(a) Ni kwa nini hivi sasa bei ya meli kutoka Pemba kuja Unguja kupitia boti inafikia shilingi 35,000 kwa tiketi moja ?
(b) Naomba nifahamu meli ya MV Serengeti *life time* yake ni miaka mingapi na hivi sasa inaruhusika kuchukua abiria Zanzibar ?
(c) Kwa kuwa tumepata taarifa kwamba meli ya MV Mapinduzi imeuzwa na tayari mnunuzi amejitokeza. Naomba nijue ni nani na ni kiasi gani serikali imepokea ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kuhusu bei za nauli kufikia shilingi 35,000 kwa Pemba hili sina taarifa nalo lakini kama yeye ana uhakika hivyo naomba tuwasiliane ili tujue tunachukua hatua gani.

La pili MV Serengeti *life time* yake mimi siielewi lakini wiki iliyopita niliwaagiza Mrajis wa Meli aende akaifanyie ukaguzi kuiangalia ubora wake na kuangalia kama bado ina haki ya kuchukua abiria ambao wameruhusiwa sasa

hivi. Tukiona kwamba inazidi kuchakaa basi tutawapunguzia idadi ya abiria wa kuchukua katika meli hiyo. Sasa hivi wanachukua kama abiria 900 nafikiri, lakini tunatarajia baada ya ukaguzi ama tuendelee na hawa au kuwapunguza kutokana na hali tutakayoikuta kwenye meli.

Mhe. Spika, MV Mapinduzi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeruhusu kuuzwa kwa dola laki nne na nusu, kampuni moja tu ndio ilikuja kutoka Dar es Salaam. Sina uhakika kama tayari wameshalipa kwa sababu malipo ya meli hii yatafanyika Wizara ya Fedha, isipokuwa fedha hizi zitawekwa katika akaunti maalum kwa ajili ya kurejeshwa Shirika la Meli kwa mchakato wa kutafuta meli mpya.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kusema kwamba meli ya MV Serengeti hivi sasa imo katika kuangaliwa juu ya uzima wake. Lakini Mhe. Waziri alikubali kwamba kama meli hiyo itakuwa haina mwelekeo mzuri itapunguziwa idadi ya abiria ili iende kutokana na uwezo wake.

Je, Mhe. Waziri haoni kama meli hiyo haistahiki kuchukua watu kabisa kwa kuwa mbovu, si bora ikakaa ikatengenezwa kuliko kuhatarisha usalama wa hawa watu kidogo ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tusitumie mambo ya kuangalia kwa macho, hata sisi binadamu tunatakiwa tupime afya tusiangalie mtu kwa macho tu. Sasa wacha meli ikakaguliwe baada ya matokeo yale *surveyor* wetu atakuja kutuambia. Kama mbovu haifai kuchukua abiria tutaizuia kabisa kuchukua abiria, kama inaweza kuchukua abiria tutairuhusu kwa kiwango ambacho kitaruhusika. Lakini ni lazima tuikague kwa sababu naye mwenye meli asije akalalamika upande wa pili kwamba kafanyiwa hujuma. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi watuvumilie tuifanyie ukaguzi na baadaye tutatoa jibu kwamba inafaa kuchukua abiria au haifai.

Nam. 40

Kukauka kwa Miti ya Karafuu

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza**:-**

Hivi sasa miti mingi ya mikarafuu Unguja na Pemba inakauka kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo za kukatwa kuni za kupikia, kukatwa majengo ya kujengea nyumba, kupandwa kwa vipando mfano migomba pembezoni mwa

mikarafuu kwa kuchimbiwa mashimo na kuikata mizizi ya miti hiyo pamoja na kuwepo kwa uchafuzi wa mazingira.

(a) Je, Wizara ina mkakati gani wa kuliimarisha zao la karafuu ambalo bado ni uti wa mgongo wa uchumi wetu ?

(b) Wizara inachukua hatua gani ya kupunguza matatizo mbali mbali yanayoikuta miti ya karafuu ?

(c) Kwa kuwa kila msimu mikarafuu hupandwa kwa miche kutolewa bure. Je, baada ya hatua hiyo Wizara huchukua jitihada ya kufuatilia maendeleo ya upandaji na ukuaji wa mikarafuu hiyo ?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, ina mikakati ya kuliendeleza zao la mikarafuu na kutoa miche bila ya malipo. Vile vile kutoa elimu kwa wakulima. Hivi sasa Wizara yangu ina mpango wa kutoa zawadi kwa wakulima bora wa zao hilo.

(b) Wizara yangu kwa kutumia wataalamu wake imekuwa ikijitahidi kutoa elimu ya uzalishaji bora na utunzaji wa mikarafuu kwa wakulima katika kila shehia yenye mikarafuu za Wilaya zote za Unguja na Pemba ili kupunguza matatizo mbali mbali yanayolikabili zao hilo.

(c) Mhe. Spika, ni kweli kuwa kila msimu mikarafuu hupandwa kwa miche kutolewa bila ya malipo. Kwa hivyo, baada ya hatua hiyo Wizara ya Kilimo huchukua jitihada ya kufuatilia maendeleo ya upandaji na ukuaji wa mikarafuu hiyo kupitia wataalamu wake waliopangiwa kazi Wilayani.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Kwa kuwa miti hivi sasa inakatwa ovyo. Je, Mhe. Waziri huoni kuwepo kwa misumeno ya moto kunaongeza kasi ya ukataji wa miti ikiwemo mikarafuu ?

(b) Je, ni kauli ipi ya serikali ambayo imechukua kuhusu uingizwaji na utumiaji wa mashine hizi ?

(c) Je, Mhe. Waziri huoni ukataji wa miti ovyo ni uharibifu wa mazingira na uchumi wa nchi yetu ?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba kuwepo kwa misumeno hii kwanza inahatarisha mazingira na pia inaendeleza wizi mkubwa unaojitokeza wa miti. Kwa sababu sio wale ambao wanaruhusiwa wakati ile mti kisheria, ni watu ambao wanaiba.

Wito tunaoutoa kwa Wizara yetu kupitia kwa Serikali tunataka tuhakikishe kwamba misumeno hii tunaitafuta na pia kuipiga marufuku ili isiendelee na uharibifu huu wa mazingira. Tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi, masheha, madiwani pamoja na watu wengine wote wenye nia nzuri na Serikali yetu, basi watusaidie kuwatambua wale watu ambao wana misumeno hiyo na wanaitumia kinyume cha utaratibu, ahsante.

Mhe. Said Khelef Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuulia swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi ni mkulima wa mihogo, mikarafuu na minazi. Sasa ninataka Mhe. Waziri anifahamishe hao wataalamu wanaopita kuiangalia hii mikarafuu tunayoipanda wako wapi mbona mimi siwaoni?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, labda inawezekana ikatokezea bahati mbaya ikawa anapishana na wataalamu wetu, kwa sababu na sisi muda mwingi tunakuwa katika harakati za kikazi. Wakati mwengine yeye siku za Jumamosi na Jumapili ndio huzitumika kwa kilimo kwa mujibu wa maelezo yake na wataalamu wetu siku hizo wanakuwa wamepumzika.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba kama huko kwake hawajafika, basi tutajitahidi ili wataalamu wetu waweze kufika hata katika shamba lake yeye na mashamba ya watu wengine.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ajira ya Zanzibar ni tatizo kuipata na kwa kuwa tayari watu wengi wameshaimiliki misumeno hiyo na kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema tayari anaifanyia mbinu ya kuipiga marufuku. Kwanza nimuulize,

(a) Je, wale watu ambao wanayo na wanaimiliki atakapopiga marufuku atawalipa fidia au vipi?

(b) Dai lake ni kwamba wasimamizi wakubwa na watoaji wa vyeti vya ukataji wa miti ni Wizara yao. Je, amejipanga vipi kuhusu wafanyakazi wake wa maliasili kwa wale ambao hawafuati utaratibu, atawazuia kazi au atawafumbia macho?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kuhusu watu wenye misumeno na anasema kwamba ndio ajira yao. Kwa kweli kwa sababu wao wameingiza misumeno hii kinyume cha utaratibu na hatukuwataka kwamba waagize misumeno labda tuna miti mingi sasa hivi imetuzidi inataka ikatwe.

Kwa hivyo, sisi Kama serikali kwa kupitia wizara ya kilimo hatutowalipa fidia na wale ile misumeno hatutowanyang'anya. Tutakachokifanya sisi ni kuwapiga marufuku kwamba misumeno hiyo isifanye kazi ya uharibifu wa mazingira.

Mhe. Spika, nafikiria labda kwa Zanzibar kuna jambo moja ambalo linatukwaza wengi. Watu wengi wanachukulia kwamba miti kama ni adui zetu. Leo ukiwa na mibuyu, kwa mfano ikiwa chini ya nyumba yako basi unataka kuhakikisha kwamba mibuyu ile imeondoka na kwa imani ile ile kwamba kwenye mbuyu anakaa jini. Lakini hata ndani ya chumba chako jina anaweza kukaa.

La msingi ni kuelewa kwamba sisi tunaitegemea miti na miti inatutegemea sisi. Kwa hivyo, moja katika hali ya kiserikali ni kuhakikisha kwamba miti haikatwi na tunapanda miti zaidi.

Mhe. Spika, suala la wafanyakazi wangu kuwa tutawafumbia macho. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba hatutowafumbia macho. Jambo moja liliopo katika suala la ukataji miti ni kama vile inavyokwenda mahakama. Kwa sababu huwezi tu ukaamua kama wewe ni hakimu ukasema kwamba leo labda mtu fulani atiwe hatiani, ni nguvu zile za ushahidi.

Kwa hivyo, katika kukata hii miti moja linalofanyiwa kazi ni kwamba unaomba karatasi na inarudi katika shehia yako. Sheha kwanza anakua mtu wa mwanzo halafu inakwenda kwa Afisa wa Wilaya, baada ya kutolewa kile kibali kwa miti ambayo inahatarisha maisha, tuna ujenzi wa maskuli yetu, utengenezaji wa barabara basi humo ndio tunatoa ruhusa. Lakini mwahala mwengine mote huwa wanakata miti kinyume cha utaratibu na kama atatokezea afisa anatoa kibali cha miti ambayo haihatarishi mambo hayo ambayo nimeyataja, basi huyo

tutamchukulia hatua na tuko tayari kushirikiana na Mhe. Mwakilishi yeyote na mwananchi mwengine yeyote.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na Mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Majadiliano yanaendelea)

Taarifa

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea na majadiliano, nimepewa taarifa kwamba wale wasajili wa simu kutoka Zantel leo wako ukumbi wa juu hapo na kwa ratiba walioweka leo ni siku yao ya mwisho.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wale wanaohitaji kusajili simu, wajumbe pamoja na wafanyakazi wetu, basi wasajili hao wapo katika ukumbi wetu wa juu.

Mhe. Naibu Waziri Habari, Utamaduni na Michezo: Taarifa kidogo Mhe. Spika, huu usajili unaofanyika wa Zantel kama mtu hakuwahi kujisajili watachukua hatua gani, watamfungia *line* yake au vipi. Kwa sababu wana wateja zaidi ya milioni moja, sasa kama wateja laki tano hawajawahi vipi watawafungia?

Mhe. Spika: Wapo juu hapo, nadhani utakapokwenda utaweza kuuliza swali hilo na watakujibu. Kwa hivyo, tuendelee na majadiliano.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunirejeshea nafasi yangu ya kuchangia mswada huu unaohusiana na mambo ya kodi. Mhe. Spika, katika mswada huu nitakwenda kwenye ukurasa wa 22 kifungu cha 8(1) na (2). Kifungu hiki kinahusiana na usajili wa muda na usajili wa mpito.

Kwa kweli Mhe. Spika, kadiri nilivyosoma kifungu hiki sijakifahamu. Kwa hivyo, la mwanzo nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleweshe amekusudia nini juu ya usajili wa muda na usajili wa mpito

Mhe. Spika, katika suala zima la usajili huu wa muda na wa mpito mimi nimepitikiwa na jambo ambalo nataka niitahadharishe Serikali au hii idara inayohusiana na mambo ya kodi.

Mhe. Spika, wafanyabiashara siku zote ni wajanja, la mwanzo wanalofukuzia wao ni kupata faida na kutafuta maslahi kwa njia yoyote. Sasa Mhe. Spika, katika sekta ya biashara sasa hivi kuna maslahi mengi sana ambayo jumuiya za kimataifa na Serikali yetu imeweka mazingira hayo ili watu waingie kwa kuipatia serikali mapato pia kuongeza uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, miongoni mwa maslahi hayo ni mambo ya ruzuku. Hivi karibuni nimemsikia Mhe. Rais katika redio kuwa alihudhuria shughuli moja ambayo wafanyabiashara wetu wanapokea ruzuku ya asilimia 50 ya mitaji yao ili kuendeleza. Sasa kwa sababu wameshasikia kuna fedha hizo au kuna fursa hizo, nachelea watu waliokuwa wadanganyifu wakaja kuitumia fursa hii kwa kujipatia pesa hizo. Anaweza kuazima pesa popote akasema mimi sasa nina milioni 200 ili apate na yeye milioni 200 akaongeza kipato chake.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naitahadharisha serikali kwa nafasi hii ya usajili wa muda na usajili wa mpito isijekutumika hivyo. Au nafasi za maonesho ya kibiashara. Maana yake unaweza kusikia leo kuna maonesho ya biashara Beijing au Ufaransa akaona ngoja nikate leseni ya mpito mimi na akenda akatumia fursa hiyo. Pengine akawa mjanja zaidi akawakosesha nafasi kwa wale ambao wanaofanya biashara kikweli kweli.

Vile vile nafasi nyengine ni kuilaghai Serikali kwa kujipatia *passport* tu, akiambiwa kwenda huko huwezi kupata lakini mpaka kwa wafanyabiashara, basi akaitumia nafasi hiyo.

Kwa hivyo, nimeitoa mifano hii Mhe. Spika, yote ni kwa ajili ya kuitahadharisha Serikali katika kuwasajili hawa watu wa mpito na watu wa muda. Kwa hivyo, katika usajili huu ingawa mimi sikufahamu, lakini kwa vile inavyonipitikia nimeona Serikali ichukuwe hadhari kabisa juu ya suala hilo la kutumika usajili huo katika njia zilizokuwa si sahihi.

Mhe. Spika, kwenye sehemu ya 4 na 5 ya mswada kwa pamoja, hii inahimiza namna gani Serikali au idara ya mapato inawahitaji wafanyabiashara kuwafanyia makisio na marejesho ya mikopo au ya kodi.

Mhe. Spika, na hapa vile vile ni lazima na hao wanaofanyiwa makisio hayo au wanaotarajiwa. Jambo muhimu kwanza ni kuhakikisha wafanyabiashara hao wawe ni endelevu, sio zile biashara za mkono tu. Ikiwa tutawaingiza wafanyabiashara wa mkononi. Mfano amechukua vitenge vyake 6 na mivao ya kanga 6 tukawataka walipe kodi, basi tutakuwa tunawaonea baadhi ya wafanyabiashara hao.

Mhe. Spika, ni lazima Mhe. Waziri angetupa kiwango cha watu hawa ambao kwa mtaji gani watakuwa wanatakiwa kufanyiwa makisio biashara yao ili waweze kurejesha na kufanya marejesho ya shughuli nzima ya biashara yao ili wakusanyaji wa kodi waweze kujua kima ambacho anastahiki kukilipa.

Mhe. Spika, kwa hapa nakusudia lazima kuwe na msamaha kwa wafanyabiashara hawa wadogo wadogo na wasiingizwe katika eneo hili. Hata kwa wale ambao watakuwa wamefanya biashara basi izingatiwe kiwango, kwa sababu kuna baadhi ya nchi hufanya makisio kwa biashara yako kwa mwezi mzima utaweza kufanya hiki, akapangiwa makisio ya kodi.

Pia Mhe. Spika, ningependa ikazingatiwa je, kile kiwango cha biashara kimefikiwa na kama hakikufikiwa anataka kuja kulipa je atakuja kupunguziwa mwisho. Biashara yako itakuwa ni tani 10,000 za kuingiza mchele, lakini hakuingiza huko zimeingizwa tani 5 tu, na huku imeshafanywa makisio kwa mwezi unaweza kulipa kodi hii, kwa sababu meli haikufika au bidhaa imeharibika au mali imeibiwa. Je, kwa watu kama hawa, hawa wataalamu wetu wa kufanya makisio watachukua hatua gani juu ya mfanyabiashara au mlipa kodi wa aina hiyo. Lengo langu ni mtazamo wa Serikali juu ya kadhia ya aina hiyo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 22 kinahimiza sana wafanyabiashara walipa kodi kuwa na kumbukumbu. Kwa hivyo, hapa nataka kuzungumza mambo mawili tu ili niweze kumaliza huu mchango wangu.

Mhe. Spika, kumbuka tunakwenda katika karne hii tuliyonayo ya 22. Mambo ya makaratasi sasa yamepitwa na wakati, maandiko, kumbukumbu na mawasiliano yote sasa yanakwenda kwa compyuta.

Sasa Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri katika hali hii kwa upande wetu sisi tumejidhatiti au tumejitayarisha vipi katika mawasiliano haya ya compyuta, kwa sababu kuna wafanyabiashara wengine wamekwenda juu kabisa, isiwe kumbukumbu zao wameweka kwenye kompyuta, sisi tunalazimisha tena aje kwenye karatasi.

Kwa hivyo, ningemuomba anihakikishie Mhe. Waziri je, idara yetu imejidhatiti vipi katika mtandao wa sasa wa kuweka kumbukumbu zake. Pia kwa wafanyabiashara kuwe na vitengo maalum za kuwapa taaluma ya uwekaji kumbukumbu zao hasa hizi za kulipia kodi. Tuwafundishe namna ya kuendesha shughuli, lakini huu uwekaji wa kumbukumbu unataka taaluma maalum. Anaweza mtu akawa ni mfanyabiashara mzuri lakini taaluma ya uwekaji wa kumbukumbu hajui. Unaweza ukaja mzigo leo basi mkamuuliza *bill of land* iko

wapi hanayo, sijui *invoice* umeweka wapi haijui, moja iko kwenye *briefcase,* moja kaweka kwenye sanduku na nyengine kaweka kwenye mchago.

Kwa hivyo, uwekaji wa kumbukumbu Mhe. Spika, ni fani. Je, vyuo vyetu hivi vinasisitiza hivyo, wafanyabiashara wetu wanajua. Huu ni mtazamo wangu Mhe. Spika, katika kifungu hiki cha 22.

Mwisho Mhe. Spika, kodi ni moja katika njia za kuipatia Serikali mapato. Sasa Wizara ya Fedha yenyewe inavyo vitengo vya kukusanya kodi na taasisi nyengine zina kodi zake. Sasa narejea suala langu, kwa vile vitengo vyote vinavyokusanya kodi je, sheria hii ndio itai-*accommodate* na mambo yote hayo. Hizo taasisi zote zitaitumia sheria hii katika mambo ya ukusanyaji wa kodi watafuata humu au kila mmoja na yeye itabidi mwenye kukusanya afanye utaratibu wake atunge sheria yake ya ukusanyaji wa kodi.

Jengine Mhe. Spika, kodi kama za Baraza la Mji utaratibu wake umekuwa na kero, sijui kwa watu wa mjini, lakini kwa sisi tunaotoka shamba, kodi zinazokusanywa na Baraza la Manispaa linaudhi. Mkulima, maana ndio kazi yetu hatuna mambo ya afisini kule wala viwanda. Kazi yetu kubwa kuvua, kufuga, kulima, kukata kuni na makaa.

Mhe. Spika, hivi sasa ukiingia sokoni, hasa soko letu la Mwanakwerekwe, kwanza gari unaambiwa lazima iingie ndani na nafasi yenyewe haipo ya kutosha ya kuteremsha mizigo. Sio hivyo tu, lengo linalotakiwa pale ukalipe pesa. Pakacha moja shilingi 500, mkungu wa ndizi uulipie. Mhe. Spika, kodi kama hii inatuudhi, ingawa anasema anasafishia.

Kwa hivyo, itafutwe namna ya kuweza kupatikana kodi hii. Dereva anatoleshwa kodi kwa kuingiza gari pale, ndio sababu pengine hata nauli ya abiria kupanda. Kwa sababu kama unapakia mzigo anakuambia hapana, au inazidishwa kodi ya kupakia mzigo juu ya bodi anaongezewa mkulima na hali bei ya ule mzigo anaokuja kuuza sokoni hajui anaanza kulipishwa kodi kwanza. Kwa sababu dereva akishaambiwa pale akija na gari lazima aitie ndani, maana yake kimewekwa kibao pale sokoni Mhe. Spika, kama utaona. Gari haina ruhusa ya kuteremsha mzigo nje iingie ndani, makusudio ni ikalipe kodi kule. Kwa hivyo, ni lazima dereva atamlipisha aliyekuwa na mzigo.

Kwa hivyo, gharama ya mzigo inaanza pale. Akipata dalali basi baadae mzigo wote anakuja kupata mlaji, dalali apate zake, mchuuzi apate zake na halafu tunasema maisha magumu muhogo hauliki na ndizi hainunuliki. Hizi kodi za udoho udoho Mhe. Waziri azitizame, japo sio afisi yake inayokusanya lakini yeye ndio dhamana wa mapato ya Serikali. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, kodi hata kwenye barabara zetu zinazojengwa na wananchi. Mhe. Spika, mimi bado ninasikitika, barabara hizi za Kilimatinde, Darajani, Mchangani hapo zilikuwa nyembamba, Serikali tukasema tuzipanuwe, basi zimepanuliwa ili wateja wanaokwenda mule madukani wapate nafasi ya kujimwaga. Sasa hivi serikail imepiga michoro mule, badala ya watu kupita basi imekuwa kwenye barabara zetu ndio mwa kuegeshea magari, halafu kumewekwa watu wa kukusanya kodi. Utaratibu huu unakwenda nje kabisa ya malengo yetu, magari yana udhi, mbanano unazidi, vibaka wanapata nafasi ya kusuguana na wateja na kuwachania mifuko yao kinamama na kinababa kupokonywa simu za mkononi na fedha zao kwenye mifuko.

Mhe. Spika, barabara imetengenezwa kwa mfuko mkuu wa Serikali, sio manispaa. Sasa inakuaje sasa barabara zilizotengenezwa ili ziweke haiba katika mji halafu tunahalalisha kuwekwe mistari ya kuegeshea magari. Mhe. Spika, kodi za aina hii, nafikiri itakuja katika huo mswada unaokuja, nadhani katika hizo pesa chafu. Pesa zile ndio pesa chafu, kwa sababu kusudio la barabara ile ni tupite, sasa wewe unakwenda kuruhusu pawekwe magari na kupokea pesa hizo, hizo ndio katika pesa chafu Mhe.Waziri ajuwe, mswada wake unakuja. Lakini kwa mujibu wa maneno ya semina yale tuliyozungumza kwamba pesa hizi ni chafu. Kwa hivyo, Serikali isikusanye pesa hizo za kuegeshea magari katika barabara zetu kuu ambazo tunatakiwa wenyewe tupite kwa kujimwaga.

Halafu jengine ni hali ya ukusanyaji wa kodi. Mhe. Spika, tumezungumza wakusanyaji wa kodi kwenye mahoteli na kwengineko, nashukuru sasa hivi wamejitahidi. Lakini kama wakusanyaji wa kodi wetu wa Baraza la Mji hali yao sio nzuri hasa kwenye kivazi. Mhe. Spika, mkusanyaji wa kodi utamuona kavalishwa kiroba cha plastiki kama mbwa wa *race* wa Ulaya wale. Kule Ulaya mbwa hufanyishwa *race*, lakini kila mmoja huvalishwa nambari yake kwa kizibao cha juu. Sasa hapa kwetu wanavaa vile wanakusanya kodi, hii ni aibu Mhe. Spika, watumishi wa serikali kuvishwa kiroba kile.

Mhe. Spika, ninaiomba serikali utaratibu huu iwache mara moja. Mhe. Mkuu wa Mkoa wewe ndio dhamana wa Baraza la Mji, wewe ni mkuu wa utawala wa Serikali unajua, wale tunawavalisha viroba vya manjano ambavyo ni sare za mbwa wa *race* katika sehemu za Ulaya, sisi tunawavisha ndio za kukusanyia kodi, zinatutia aibu Mhe. Spika. Nani yule unaambiwa yule ndio mkusanya kodi, aah! Aibu. Naiomba serikali iwahurumie watu wale, wavalishwe nguo zinazoelekea kuwa huyu ni mkusanya kodi. Wale kwa hali ile hata hiyo kodi yenyewe nafikiri haipo, yeye mwenyewe hali yake mbaya. Kodi hiyo nafikiri yote itaingia kwenye mifuko yake kutokana na hali yake.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hapa nimetoa mifano, lakini mazingira ya wakusanya kodi lazima nayo yazingatiwe, kwa sababu unakwenda kukusanya kodi, huyo

mtoa kodi ajuwe hasa huyu mtu anakuja kukusanya kodi. Lakini mtu anakwenda kukusanya kodi mtu mwenyewe anamdharau, aah! mimi sina bwana wewe chukua kanywe kahawa. Hata kile kiwango chenyewe kutokana na hadhi ya yule mkusanyaji hatutokipata.

Sasa hii sio kwa wale wa Baraza la Mji tu na wengine wote wakusanyaji wa kodi kama hawakuwekewa mazingira yaliyokuwa mazuri, basi fedha zinazokisiwa basi hazitopatikana.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mwisho wa wiki na mwanzo wa wiki kwa kunipa mchangiaji wa mwanzo, nakushukuru sana. Baada ya mchango huu Mhe. Waziri kasikia na naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kuchangia mswada huu wa usimamizi wa kodi.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea mswada huu muhimu juu ya kuhakikisha kwamba kodi inasimamiwa vyema na fedha zifike Serikalini kwa kulenga maendeleo ya nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Spika, katika ulimwengu wetu huu, nchi nyingi duniani zinategemea kuendeshwa na kodi mbali mbali, ili zipate mahitaji yake ya kujikimu katika uendeshaji wa nchi, na huduma mbali mbali ambazo zinategemewa juu ya upatikanaji wa kodi hizi.

Pia Mhe. Spika, nikiri kwamba usimamizi ukiwa mzuri, basi mafanikio yatapatikana na usimamizi ukenda sahihi zaidi, basi yule mlipa kodi huwa ana hamasa za kulipa kodi kwa wakati ili Serikali iweze kupata kodi yake bila usumbufu .
Mhe. Spika, tukiangalia kwenye mswada huu kuna maelezo mengi pamoja na vifungu tofauti vikiwemo vile vya adhabu kwa kucheleweshe kulipa kodi na mambo mengine.

Kwa hivyo, niseme kwa kuwa mswada huu malengo yake ni kuhakikisha usimamizi mzuri wa walipakodi, basi ningeomba Mhe. Spika kupitia kwako, kama jina la mswada huu linavyojieleza ni Usimamizi wa Kodi, basi uwe hivyo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Zanzibar ni sehemu ambayo imezungukwa na bahari, tokea wakati wa wazee wetu mpaka na sisi leo tupo hapa, yaani historia

hiyo. Kwa kweli asilimia kubwa ya nchi yetu inategemea biashara mbali mbali, kwa ajili ya kuweza kujiendesha na kuhakikisha kile kinachopatikana kinawafikia wananchi juu ya huduma za jamii mbali mbali katika nchi yetu.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana mwaka 1964 mara baada ya Mapinduzi Matukufu Mhe. Rais wa kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alizuia biashara zote ziwe mikononi mwa serikali. Suala hili alilifanya kwa makusudi kwamba unapoidhibiti biashara, basi pato la nchi litakua na ukiachia pato la nchi litakosekana na itakwenda kwenye njia ambazo si nzuri za utekelezaji wa maendeleo ya wananchi wake.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha miaka ya 1964 mpaka 1972 Marehemu Mzee Karume alipofariki, hali ya uchumi wa nchi yetu ulikuwa ni mzuri tena harakati zake zilikuwa zinakwenda vizuri. Mhe. Spika, nakumbuka katika suala la kudhibiti uchumi pamoja na mapato ya serikali. Kwa kweli serikali ilifanya mengi zipo kumbukumbu nyingi na sisi wakati huo tulikuwa wadogo tulishuhudia.

Kwa mfano, Nyumba za Maendeleo za Michenzani, Kilimani, Kikwajuni, Chakechake, Wete, Mkoani pamoja na sehemu mbali mbali za nchi yetu mpaka vijijini, kama vile Makunduchi, Gamba na kwa upande wa Pemba Micheweni na Kengeja nyumba hizo zipo Mhe. Spika. Kwa hivyo, hali ile ilikuwa ni kudhibiti mapato ya serikali pamoja na nchi kwa jumla ndipo mafanikio yale yalipopatikana.

Mhe. Spika, vile vile tunaweza kusema kwamba mara baada ya kifo cha Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Mwenyezi Mungu amrehemu na amlaze mahala pema peponi, zikaja awamu nyengine na serikali ikaona hakuna haja ya kuelekea kwenye biashara isipokuwa wapewe wananchi, ili wapate fursa ya kusaidia nchi yao, lengo si baya tena ni zuri.

Lakini kwa bahati mbaya haikuwepo taaluma ya kutosha kwa wakati huo, wafanyabiashara wengi walijilimbikizia mali kutokana na kutokuwepo kitu cha kuwasimamia au kuhakikisha kwamba ile biashara anayoifanya yeye, basi apate faida pamoja na serikali pia juu ya kupelekea majitahiji mbali mbali katika pato la nchi katika kuwasaidia wananchi wake.

Mhe. Spika, mfanyabiashara yeyote tunategemea apate faida, wakati anapopata faida ile basi ajue inazo sehemu mbili kwamba pato lake yeye binafsi pamoja na lile la serikali. Kwa hivyo, napenda kuchukua fursa hii kwa kuipongeza serikali kwa kuangalia usimamizi wa kodi za shughuli mbali mbali katika nchi yetu zinasimamiwa ipasavyo, kwa ajili ya kuhakikisha kuwa pato linapatikana na maslahi ya nchi yetu yanaendelezwa.

Kwa kweli hali ya biashara hapa kwetu ni ngumu. Nadhani hali hii inatokana labda na usimamizi ambao kidogo siufahamu unavyokwenda. Mhe. Spika, kwa mfano kipindi kifupi kilichopita nyuma miaka ya 1990 mpaka 2000, basi wafanyabiashara wengi wa Tanzania Bara, Rwanda, Burundi, Zaire hivi sasa Congo, Zambia walikuwa wanakuja kuchukua bidhaa tofauti hapa kwetu.

Lakini baada ya kwenda kwenye mifumo mbali mbali ya usimamizi wa kodi hizi, basi tulifikia pahala Mhe. Spika sisi tuliokuwa tunatoa mali hapa na kupeleka kwa wenzetu imegeuka hivi sasa, yaani badala ya sisi kupeleka kule imekuwa sisi ndio tunaochukua kule na kuleta kwetu. Kwa hivyo, biashara inaonesha dhahiri kwamba imedidimia.

Mhe. Spika, hali hii inatokana na matatizo ya ushuru wa kodi zetu. Kwa sababu kodi ni sehemu moja ya serikali kupata maslahi yake na wala haikataliki. Lakini suala la kuwa na kodi mbili kwa baadhi ya bidhaa huwa linanitatanisha akili yangu na wala silifahamu *(Makofi)*.

Kwa maana hiyo, Tanzania Bara biashara zimekuwa rahisi kuliko Zanzibar kwa nini. Kwa sababu kwanza wenzetu wanatumia chombo kimoja tu *TRA* peke yake. *TRA* inakusanya mapato yake kutokana na kinachokusanywa, lakini baadaye hakuna mtu mwengine wa pembeni anayekusanya tena kwa maslahi ya sehemu nyengine.

Mhe. Spika, hili ndilo lililodidizima nchi yetu kuwa isiende mbele baada ya *TRA* kukusanya kodi hapa Zanzibar na *ZRB* pia kuwa ni mkusanya kwa baadhi ya bidhaa nyengine.

Kwa mfano, hivi sasa ukiichukua gari kutoka Dubai, Ufaransa au hata Japan na kuileta hapa basi *TRA* ya Tanzania inakwambia gari yako imeileta katika nchi yetu na imepitia katika njia ya kisheria, yaani haina matatizo utalipia dola. Mhe. Spika, haya ni makubaliano ya bidhaa iliyotoka nje ya Tanzania, kwa sababu Tanzania ni nchi moja na tunaamini kwamba *TRA* ni moja.

Isipokuwa jambo la kushangaza hii gari unapoichukua hapa Zanzibar na kuipeleka Tanzania Bara unailipia tena, je kuna nini hapa na huku ndiko kukuza au kudidimiza uchumi wetu. Kwa hivyo, kodi hii iangaliwe kuna kitu gani ambacho kinachosababisha adha hii *(Makofi)*.

Vile vile gari ile umeinunua na kuja kwenye Bandari ya Tanzania Bara, ikiwa Dar-es-Salaam, Tanga, Mtwara au sehemu nyengine, basi unapoitoa kule kwa ajili ya kuileta hapa Zanzibar huna malipo tena, yaani malipo yanakubalika kule moja kwa moja.

Mhe. Spika, nadhani hapa kuna mchezo ambao umepangwa kwamba kinachotoka huko kikiingia kwetu basi kifanyiwe malipo mara mbili, yaani kodi kama vile hali ya kukomoana kwa upande mwengine. Kwa kweli nayasema hapa kwa ushahidi Mhe. Spika, tena na muomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika ayasikilize sana haya tunayomwambia, kwa sababu yana maana na tunahitaji ufafanuzi mzuri kuhusiana na suala hili *(Makofi)*.

Kwa kweli tatizo la *TRA* si kubwa, lakini ni kubwa. Kwa sababu wao kama wanaaminiana na ndivyo ilivyo, hii *ZRB* ingeachiwe ikawa inakusanya kama ni wakala kwa sehemu ya *TRA*. Kwa mfano, ndani ya mswada huu umeeleza kwamba mfanyabiashara yeyote atakayemfanyia Kampuni ya Shihada *Enterprises*, sasa mimi ninayewakala wangu na anapoleta ule mzigo basi itahisabika ameuingiza wakala. Kwa hiyo, wakala yule atatakiwa alipe kwa mujibu wataratibu zilizowekwa.

Mhe. Spika, kwa upande wangu *ZRB* ni wakala mzuri sana wa *TRA* na ninaamini kama itasimamia vyema, basi Wallahi hatutopata matatizo katika nchi yetu na linalopelekwa Bara litakwenda sahihi bila ya kuingiliwa na utata ambao hatuufahamu unatokea wapi *(Makofi)*.

Kwa sababu nchi zote duniani zinategemeana na kwa bahati nzuri sisi Tanzania ni nchi moja. Sasa kama ingekuwa bidhaa naitoa hapa na kuipeleka Kenya au Uganda ama Rwanda au Burundi ingekuwa suala jengine. Lakini nikiitoa hapa Zanzibar naipeleka Tanzania Bara, yaani tofauti yake ni Zanzibar na Bara tu. Kwa hivyo, sioni sababu kwa nini bidhaa zinazotoka hapa Zanzibar zinapofika Bara hawa *TRA* sisi tuhaifahamu kule kwa hiyo ilipiwe tena na hili ni kero *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwenye mswada huu ningeomba sana Kamishna wa *TRA* Tanzania Zanzibar akaekewa lengo na wala asiwe anamua yeye anavyopenda na hivyo si sahihi. Kwa maana hiyo, lazima kuwe na kitu cha kum-*control* yeye na wala sio aseme kwamba hiki mimi nimependa hivi basi kiwe hivyo haiwezekani, kwa sababu hii ni nchi tena yenye serikali kamili ambayo yenye kutegemea biashara tokea historia ya nchi hii.

Vyenginevyo hatwendi na kila siku tutazidi kuwa masikini na matokeo yake tutawalaumu wafanyabiashara wetu kumbe wao wanalanguliwa kutokana na mambo ambayo hatuyajui. Mhe. Spika, naomba sana ili twende vizuri tena kwa usahihi katika masuala yetu mbali mbali, vyema *TRA* wakakaa na *ZRB* kwa ajili ya kufanya tafiti zao. Tunajaribu kukupeni kazi hii hebu ifanyeni na ikiwa na maslahi basi wawapongeze na ikiwa haina maslahi ni wajibu wetu kuwaambia hapa kuna makosa na ongezeni nguvu katika hili.

Mhe. Spika, bidhaa utakayoinunua Tanzania Bara leo kama vile shati, shuruali hata viatu ni rahisi mara tatu kuliko hapa Zanzibar. Kwa mfano, zamani kulikuwa na viatu vinavyoitwa bata mdogo au mkubwa, raizoni, yaani leo ukinunua kutoka Tanzania Bara basi unakipata rahisi kuliko kukinunua hapa na kitu ambacho kinashangaza sana.

Kwa kweli huko tunakotoka Mhe. Spika, watu wote wanaotoka Mbeya, Iringa, Shinyanga, Morogoro, wanaotoka kwetu Tanga na kwengineko wote walikuwa hapa Zanzibar. Vile vile wakati boti inapofika hapa basi hoteli ya kukaa haipatikani, yaani zile hoteli zetu ndogo ndogo na watu hawafika mpaka mitaani kwetu Ng'ambo kwa ajili ya kutafuta nyumba za kukaa *(Makofi)*.

Mhe. Spika, naomba pawe na mazungumzo mazuri nakubali kwamba kodi zikusanywe. Lakini kodi ziwe na manufaa kwa nchi yetu pamoja na wananchi wetu kwa jumla. Kwa sababu hivi sasa Mzanzibari anaishi katika maisha magumu sana na hata wale wenzetu wanaotoka Tanzania Bara, basi wanasema Zanzibar chakula ghali, maana tunazungumzia masuala ya biashara, yaani Zanzibar vitu ghali sana *(Makofi)*.

Kwa mfano, zamani watu walikuwa wakipiga simu Zanzibar kutoka Bara na kusema Mheshimiwa tafadhali utakapokuja nichukulie zawadi kama vile vitambaa pamoja na vitu vyengine mbali mbali. Lakini leo inasikitisha kwamba mtu anapotoka hapa kwa ajili ya kwenda Bara, basi ataagizwa kuchukua zawadi kama vile viatu au nguo, kwa sababu wenzetu vitu vyao ni rahisi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, hali hii yote naweza kusema ni usimamizi au huu mpango uliopo si mbaya nadhani unahitaji kuangaliwa upya, ili uhakikishe kwamba hii kodi hasa inamfika mlengwa na kufaidika kulingana na hali ya maisha.

Vile vile kubwa ninalolikumbuka huko nyuma kwa kuwa Zanzibar ilikuwa ni Kitovu cha Biashara, pale Msikiti Mablue ule uliokuwepo zamani palikuwa na majahazi mengi ambayo yalikuwa yakitoka Somalia. Kwa kweli Wasomali wengi walikuwa wanakuja hapa Zanzibar na bidhaa tofauti kama vile miswala, mikeka, samaki aina ya papa, nguru pamoja na vitu vyengine mbali mbali tele mitaani na leo hatuwaoni.

Mhe. Spika, Wasomani kwa shida iliyowapa kwenye nchi yao nadhani kwanza walisema wanakuja kufanya biashara Zanzibar na walikuwepo wawili watatu na wameshindwa, ambao walikuwa kwenye mipira na bidhaa nyengine. Lakini nafikiri hawakuacha kwa kuwa walishindwa hivyo, labda hapa walishindwa kutokana na kodi zinavyokwenda zimewasumbua kidogo.

Kwa hivyo, napenda kusema kwamba kodi ni suala zuri, lakini kodi hii inalengwa iwanufaishe wananchi wake. Kwa mfano, wenzetu katika nchi za nje hawa wafadhili mbali mbali duniani wanakusanya makodi tofauti kwa wananchi wao, lakini kodi ile inayo manufaa mpaka sisi inatufikia huku.

Mhe. Spika, maana yake kodi ile inaendesha nchi yao kama vile barabara, maji pamoja na kila kitu kizuri, kwa hiyo fungu lililobakia tuwapelekee masikini, kwa sababu sisi ni masikini tu tukitaka tusitake tena ni masikini sana. Kwa hivyo, hakuna hata mmoja hapa ambaye atakayesema tunao uwezo wa asilimia mia moja tuweze kujiendesha wenyewe hatuwezi. Mimi nipo hapa ambaye ni Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kwahani, asilimia kubwa ya wananchi wangu najua ni masikini sana na inabidi niwaonee huruma kwa mambo mbali mbali.

Hali kadhalika na wale wenzetu walioko nje kila wanachokipata kikipindukia kiwango basi wawapelekee ndugu zetu kwa ajili ya kutumia. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili la mashirikiano baina ya *TRA* na *ZRB*, nadhani watakapokaa pamoja na kuafikiana kwamba wakala awe mmoja wa mwenziwe basi malalamiko pamoja na manung'uniko yataondoka.

Kutokana na hali hii, ndio maana mfanyabiashara yeyote anakwambia kule Zanzibar biashara ni ngumu wala hatuzifahamu. Kwa sababu leo wafanyabiashara wengi wa Zanzibar wako Bara tukitaka tusitake, yaani hivi sasa kila mtu anakwambia natafuta sehemu Bara na hapa kwetu wanakimbia, hivyo mapato tunayakosa kutokana na usimamizi ambao naona kidogo ni mgumu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema *TRA* na *ZRB* mimi ninazungumzia sana kwa sababu wao ndio wakusanyaji wa mapato na suala la usimamizi unakuja kwao wao. Kwa hivyo, nadhani ni vyema Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze huu kuhusu mizigo au bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara, mwananchi ametoka na hapa na kufika kule Dar-es-Salaam anambiwa wamekuachia hapa lazima ulipe tena, wakati malipo yale madogo madogo wanasimamia wenyewe.

Vile vile nakumbuka kwamba viongozi wetu wa juu walisema kuwa biashara ya mifukoni masikini basi waachiwe watu wajihangaishe. Lakini leo mizigo au bidhaa zinazotoka Tanzania Bara kwa jumla unatozwa kodi tena, hali hiyo ndio inayomuongezea ukali wa maisha. Sasa mzigo au bidhaa zile uzichukue na kuzipeleka Tanzania Bara basi huulizwi chochote unakwenda bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, naiomba serikali kwa hili ikae japo kuwa ipo sheria, lakini sheria sio Msahafu, kwa sababu hapa tunafanya marekebisho ya mambo mbali mbali na wala sheria hii sio mpya, isipokuwa inafanyiwa marekebisho ya kuweka mkakati juu ya kukusanya mapato.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala hili liangaliwe kwa faida ya wananchi wetu juu ya kuhakikisha kuwa kila linalowezekana kufanywa, basi lifanywe kwa ajili ya kuleta manufaa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kuna matatizo mengine ambayo yamejitokeza, mswada huu ni mzuri kama nilivyosema, kwa sababu mswada huu ndio ule isipokuwa umeongezwa mambo mengine tu. Lakini tatizo lililojitokeza kama nilivyozungumza kwamba wapo wafanyabiashara wadogo ambao ni wengi tukilinganisha na wafanyabiashara wakubwa.

Kwa mfano, leo nchi hii ya Zanzibar wafanyabiashara wengi ni wadogo ambao wenye biashara za mikononi na wala sio kama wale Wamachinga. Isipokuwa nakusudia kwamba mtu anatoka hapa na mfuko wake masikini na kwenda kule kuhangaika na kuleta hapa. Sasa kodi zinavyotoleshwa mimi nimeona tu kwamba watalipa kodi.

Lakini namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kuwa kodi hizi ziwe na maslahi kwa mfanyabiashara, ikiwa maslahi mazuri kwa mfanyabiashara basi ndipo bei za vitu au bidhaa zitakaposhuka. Mhe. Spika, kodi hizi zikiwa mkakati mkali kwa wanyabiashara wetu wadogo basi nikuongezeka kwa bidhaa zetu kupanda bei na kuwazuia wananchi wetu wasipate fursa ya kuishi vizuri.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hili aliangalie la wafanyabiashara wadogo wadogo, kwa ajili ya kuweza kujisaidia wao wenyewe, lakini na wananchi wetu wapate faida ya kuhakikisha kwamba wanapata nafuu nna kuendesha maisha yao ya kila siku *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika maeneo ya biashara kwa mfano mtu amefungua duka lake moja kubwa ameweka milango kiasi ya milango minne, lakini leseni yake ni mlango au mtu mmoja. Kwa sababu kwenye mswada huu unaeleza kwamba mtu anayo maduka mengi, basi atalipa kodi kutokana na maduka yake.

Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa ajili ya kupata kufahamu vizuri zaidi. Kwa mfano, mimi nimefungua maduka katika eneo langu moja na kutoa milango kiasi minne kwa jina la leseni yangu

moja na kuweka bidhaa tofauti kama vile mchele, nguo, vifaa vya magari pamoja na vinywaji mbali mbali.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hapa atupe ufafanuzi mzuri kwa ajili ya kuelewa, kwa sababu bado hatujafahamu na wengine tulioupitia sana huo mswada tumeuona na tunajua maelekezo yake. Lakini ninamuomba kwa faida ya wananchi wetu kwa kuepusha usumbufu, kwa sababu wengine wataogopa, kwa mfano kumbe vile mimi nimekata leseni hii kwa mwaka analipa shilingi 200,000/- au 300,000/- na duka au leseni ni moja kumbe sivyo, kwa kweli yamo manufaa ambayo niyaona ndani yake.

Isipokuwa namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, basi akitizame sana kifungu hiki kwa ajili ya kutoa ufafanuzi mzuri, ili wananchi wafahamu nini azma ya leseni pamoja na biashara mbali mbali walizowekwa.

Mhe. Spika, wananchi wetu hawana mashaka makubwa sana, lakini wanatupa maelezo ambayo tunaamini ya msingi. Kwa sababu mimi siwezi kuzungumza mswada huu wa masuala ya usimamizi wa kodi bila ya kuwapitia wafanyabishara mbali mbali kwa ajili ya kupata maoni yao. Kwa kweli bado maoni ya wafanyabiashara wanakiri kwamba hali ya biashara kwetu Zanzibar ni nzito kulinganisha na wenzetu wa Tanzania Bara.

Hali hii nadhani inasababishwa na mambo mawili kwa wakati mmoja, kwa sababu tunajua *ZRB* shughuli zake ziko huku Zanzibar na *TRA* ziko kwa upande wa mwengine, yaani Tanzania. Lakini wakati mwengine wakiyajumuisha pamoja basi huwa matatizo makubwa kwa wafanyabiashara pamoja na wananchi wetu kwa jumla.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala hili aliangalie na alifanyie kazi kwa ajili ya kupata faida wananchi wetu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nimeliona katika shughuli za biashara mbali mbali tulizonazo, kuna wananchi wetu ambao wanachukua biashara Bara au sehemu nyengine tofauti kwa madhumuni kwamba biashara inapofika hapa aipeleke sehemu mbali mbali. Kwa mfano, mimi ninalo ghala sehemu fulani na wala sio duka, yaani ghala la kuhifadhia bidhaa kwa muda na wala dukani haipo maana unapokwenda pale unaandikiwa risiti na uende pahala fulani kwa ajili ya kuchukua bidhaa.

Kwa hiyo, hapa pia namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kwa kuwa bidhaa ile haipo dukani na unapokwenda unaandikiwa risiti na kwenda ghala fulani. Je, hali hii inakuwa vipi, yaani bidhaa ile itahisabika

imetoka dukani au kwenye ghala, sijui vipi na risiti nimepewa dukani. Sasa kule ghalani ambako mali yote ndio iko inajulikana vipi pamoja na usimamizi wake unakuwa vipi. Kwa sababu tunazungumza suala la kukusanya mapato pamoja na usimamizi mzuri.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie na atakapokuwa kufanya majumuisho, basi alitolee ufafanuzi ili wananchi wetu wapate kufahamu jinsi gani ya kuendesha shughuli zetu pamoja na usimamizi mzuri kwa walipa kodi.

Mhe. Spika, suala la mwisho kabisa naishukuru serikali kwa muda huu wote. Kwa kweli naishukuru kwa kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wetu mbali mbali katika nchi yetu wanajitahidi kuleta bidhaa tofauti kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu. Kwa hivyo, bila ya wao kuwa na mahusiano mazuri na serikali basi haya yote yasingekuwepo.

Kutokana na hali hiyo, niwashukuru sana wafanyabiashara wetu wa Zanzibar kwa kuhakikisha kwamba kila kinachohitajika, kwa mfano kwenye mchele, nguo pamoja na mambo mengine tunapata hata kama hali inakuwa ngumu, lakini si kukosa kabisa kama vile nchi nyengine za jirani.

Mhe. Spika, niseme kwamba pamoja na juhudi hii nzuri ya serikali, bado taaluma na maelewano mazuri yanahitajika baina ya serikali na wanafanyabiashara na wala si vibaya mara kwa mara Wizara husika ya Utalii, Biashara na Uwekezaji pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi kuwa na vikao vya pamoja na hawa walipakodi wetu. Kwa sababu hawa ndio walipakodi wetu wakubwa, kwa ajili ya kuelezwa pamoja na kufahamishwa na wafahamu nini wanachoelezwa, ili serikali ipate faida.

Suala la mwisho kabisa ambalo lipo hapa. Mhe. Spika, hakuna jambo ambalo serikali inakosa mapato kuliko risiti. Kwa sababu risiti ni chanzo cha kukusanya mapato na bila ya risiti mapato yanakosekana, kwa maana hiyo mfanyabiashara huona ni jambo dogo tu, kwa mfano mtu ananunua kitu cha fedha nyingi kama vile shilingi 500,000/- au 600,000/- anaondoka bila ya kupewa risiti. Kwa hivyo, pale pato la serikali linakosekana kutokana na udhaifu uliopo.

Mhe. Spika, naiomba serikali kwamba bado msisitizo, mkakati pamoja na elimu kwa wananchi vinahitajika kwa mtu yeyote anayeuziwa kitu ni lazima awe na risiti, kwa sababu risiti ile ndio faida ya serikali inamopatikana na kodi ile bila ya kupotea.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, niseme kwamba nawapongeza kwa

dhati tena naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu. Pamoja na hayo, Mhe. Spika naongeza kitu kidogo na wala usikasirike naipongeza *Simba Sport Club* kwa kuifunga JKT Ruvu bao 4 – 1 na kuwasha *indicators* kuwa itachukuwa ubingwa kabla ligi kumalizika *(Kicheko/Makofi)*.

Baada ya hayo, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Assaa Othman Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zilizotuleta ndani ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa heshima yako naomba na mimi nitumie muda wako mfupi kiasi kwa kusema machache.

Mhe. Spika, jina la mswada huu ni Mswada wa Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi. Kwa hivyo, tunapaswa kujenga utaratibu mzuri na kuwa na usimamizi maridhawa kusudi lengo lililokusudiwa la kukusanya kodi liweze kufikiwa.

Mhe. Spika, kodi ni tegemeo kuu la nchi na makusanyo mazuri ya kodi kunakuwa na ufanisi mzuri wa uendeshaji wa shughuli za serikali. Kwa sababu hiyo basi, wachangiaji wengi wamezungumzia ni vipi wafanyabiashara wetu wanapata tabu ya kuendesha shughuli zao za biashara kutokana na utaratibu mbovu. Sasa tunaleta sheria itakayojenga utaratibu na usimamizi mzuri kupatikana kwa kodi hizo.

Mhe. Spika, mimi nadhani hebu kwanza tuweke utaratibu wa hawa wafanyabiashara wetu ambao wamekubali pamoja na mazingira ambayo sio mazuri kubaki hapa nchini katika hali hiyo hiyo, lakini wanawasaidia wananchi wenzao wa Zanzibar. Tokea juzi mifano imetolewa hapa kwamba wako Wazanzibari wana biashara kubwa wako huko Tanzania Bara wanalipa kodi kubwa ya mabilioni. Kodi hiyo kama tungeipata hapa kwetu basi ingetusaidia sana.

Mhe. Spika, serikali ingechukua nafasi maalum kutaka kujua hivi ni kwa nini hawa Wazanzibari wanaondoka Zanzibari wakati hapa ni kwao na ni kisiwa cha amani na utulivu. Je, hawa uzalendo umewapungua au kuna kasoro zipi? Katika hili Mheshimiwa nitamuomba ndugu yangu Mhe. Waziri Kiongozi ni mara nyingi tokea tuanze Baraza hili tunapiga kelele kuhusu biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara juu ya usumbufu wanaoupata wafanyabiashara wetu bandarini Dar es Salaam hili suala sasa hivi limeshakuwa gumu mno.

Mhe. Spika, hivi sasa tunamaliza mwaka wa nne na huko nyuma tumelikuta bado halijapata ufumbuzi. Mhe. Spika, nadhani mwenzetu ndani ya vikao vyake vinavyoshughulikia kero na hili nalo ni kero gumu na zito. Kero ambalo linadhoofisha uchumi wa nchi hilo ni kero, kero ambalo linatoa matumaini ya maisha ya watu ni kero na lisibaki kero kwa namna iliyozoeleka. Maana ukisema hilo liwekwe kama ni kero la Muungano basi ni kama kulitupa kwenye dampo la taka. Sasa hivi Mheshimiwa tunataka kero lipatikane ufumbuzi wake.

Mhe. Spika, kero hii inadhoofisha maendeleo ya nchi. Matokeo yake tunawarudia wafanyabiashara wetu ambao uwezo wao ni mdogo wa kufanya hizo biashara. Tunakubaliana kwamba wafanyabiashara wetu wengi ni wale wadogo wadogo bado uwezo wao ni mdogo. Mhe. Spika, hawa badala yakuwapa vivutio vya kuwafanya kwa hiari zao bila ya mbinu wala ujanja wazilipe hizi kodi zinavyostahiki. Lakini tunawarundukia kodi nzito kufidia kodi kubwa ambazo tunazikosa basi na wao tutawafanya watukimbie katika hali hiyo.

Mhe. Spika, suala la *TRA* limetajwa na tutaendelea kulitaja kwa sababu inaonekana ni kikwazo kikubwa mno. Mimi hukaa nikajiuliza hivi ni kwa nini wenzetu wasituamini. Wakati mmoja tumekwenda kuonana kule Dar es Salaam Kamati ya Fedha na Uchumi walituambia kwamba suala la malipo kwa *TRA* walidhani kwamba suluhisho ni ku-*harmonize* kwa namna walivyoitaka wao mimi nilikataa kama mjumbe. Wao walisema kiwango kitakachowekwa pale Mtwara, Tanga na Dar es Salaam ni hicho hicho kiweko Tibirinzi, Wesha na Malindi Unguja. Mimi nikasema kwa sauti pana kwamba hili sio sahihi na kama Mzanzibari naikataa.

Mwenyekiti wangu Mhe. Salmini Awadh Salmini alikuwepo walipotaka nitoe wazo, mimi nilisema ku-*harmonize* haina maana tu yakuweka *flat rate*, lakini tunaweza ku-*harmonize in agreement* Bara kiwango kiwe hiki na Zanzibar kiwango kiwe kile kufuatana na hali ya wafanyabiashara wetu na biashara tuliyonayo sasa hivi. Mhe. Spika, Zanzibar sasa hivi tumebaki na jina kwamba ni Kituo cha Biashara Afrika Mashariki na Kati hili jina tumelirithi, lakini tumeshindwa kulienzi na kuliendeleza.

Mhe. Spika, mimi nitasikitika sana tukipoteza kila kitu kwani muda wako huu ni waziri mwenye dhamana mambo haya yakienda hivi tutakujapaswa kujibu kwa vizazi vinavyokuja, hii hali haipendezi hata kidogo. Baadaye watu wa *TRA* walikubali kwamba tunaweza Zanzibar tukawa na namna yetu ya ushuru. Lakini inanishangaza kwamba mnapokaa mkazungumza mambo kama haya ukiondoka tu basi yanabadilika. Mhe. Spika, mimi namwambia Mhe. Waziri kwamba haya ni malalamiko ya wafanyabiashara wetu, na sisi ni wajibu wetu kuyasemea na pahala pakusema ni hapa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi ndiye tuliyemtwisha dhima nzito. Basi nafasi hii akiitumia vizuri kwa umri wake alionao bado ana nafasi nzuri ya Wazanzibari na kupata imani za Wazanzibari. Ataweza kuandika *record* yake vizuri ili katika hizo kero na yeye ahesabiwe amekwamua wapi na wapi kwa faida ya nchi hii.

Mhe. Spika, jengine Kamishna humu amepewa nafasi kubwa. Mimi naona ingelipendeza zaidi tukasema kama sheria itakavyoona inafaa kulioko kumtaja mtu na nafasi yake. Kuna mapungufu mengi kwani sisi ni binadamu hili Mhe. Waziri ningeliomba litizamwe tena ili iweze kuletwa faida nzuri.

Mhe. Spika, kuna kodi ambayo kwa Zanzibar tungeipata kwani wafanyabiashara wetu wangelipata nafuu kubwa ya kuwabandikizia mzigo mzito wa kodi. Hizi ni kodi zinazokusanywa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitaitaja moja tu ya Mamlaka ya Mawasiliano kuhusu Kampuni ya Simu ya *ZANTEL*.

Mhe. Spika, ni pesa nyingi sana na kwa masikitiko Zanzibar haiambulii na hata senti tano. Mhe. Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano hivi inakuwaje kinachovunwa ndani ya jamhurii hii, hili suala la *ZANTEL* kinachopatikana chote kinakwenda Tanzania Bara, Wazanzibari hatupati kitu.

Mhe. Spika, waziri mwenye dhamana pamoja na Waziri Kiongozi ningekuomba sana utusikilize kilio hiki kwani hizi ni haki za Wazanzibari zinapotea kila siku wala hatusikii kutajwa ndani ya kero. Je, hii haionekani kwamba ni kero au mmeshahalisha vyetu vihalalishwe kwa Bara ni haki yao na sisi tunavyochuma pamoja sisi hatumo.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu misamaha ya kodi ni kwamba hatukatai wanaokuja kutusaidia kwenye maendeleo. Lakini utaratibu na usimamizi uwe mzuri kuhakikisha ni vile ambavyo kweli tumevisamehe visilipiwe kodi kwa faida yetu. Lakini kuna vyengine kwa sababu serikali inafaidika basi ilipe mambo yote hayo.

Mhe. Spika, jengine ni vivutio kwa wale walipa kodi wazuri basi tuwape moyo ili wasije wakatukimbia tena kama wengine. Kuwapa moyo sio lazima kumkamua ng'ombe mpaka atoe maji hana tena hata damu. Nadhani viwango vikubwa sio suluhisho, tuwawekee viwango vitakavyokidhi haja kwa sababu kwa kadri ninavyofahamu mlipa kodi ni mwananchi. Mwananchi huyu anayepata shilingi 150 kwa siku anashindwa na hata kula yake ya siku na kodi juu alipe.

Mhe. Spika, kipindi cha sikukuu nguo hazinunuliki. Hapa kwetu wenye mbavu kidogo wanakwenda Dar es Salaam, wengine wanaagiza kwengine. Lakini kusema kweli mambo ni mazito na tuna dhima kubwa ya kuhakikisha wananchi wetu wanapata afueni ya maisha yao. Ni vipi angalau vile vinavyopaswa awe navyo na vile vinavyostahiki kuvipata ni haki zao basi wazipate na sisi tusimamie huo ndio wajibu wetu. Mhe. Spika, narudia tena kumwambia Mhe. Waziri Kiongozi ili mambo yake yanyooke basi haya ya wananchi nayo yanyooshe ili upate wepesi.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwamba yote haya tunayoyazungumza na mengine mengi humu ndani ni kwamba utawala bora ni kiungo. Utawala bora ndio mashine kuu ya kuyasimamia haya. Tukikosa utawala bora basi tusijidanganye ni vurugu tena ambalo mapato yake ni hasara zaidi kuliko faida. Kwa hivyo, naiomba serikali iyasimamie kwa kufuata katiba ya nchi hii, sheria tunazozitunga, kanuni zetu na taratibu zetu za kuendesha mambo na zile lugha za kukatisha tamaa za baadhi ya viongozi. Mhe. Spika, ni kwamba sheria tunazitunga wenyewe hapa na sisi ndio wa kuzisimamia na tunaapa kwamba tutazilinda halafu alisimama mmoja wetu akasema sisi tukitaka letu tunaamua hiyo sheria na katiba tia mfukoni. Kwa kweli lugha hii ni nyepesi kuisema lakini ngumu na ni kubwa zaidi.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na mimi kutoa machache, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza. Namuomba Mhe. Waziri mwenye dhamana hii atufafanulie mle tulimotaka ufafanuzi, atupe maelezo mule tulimohitaji maelezo kwa faida ya wananchi wa nchi hii. Nakushukuru sana.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, na nichukue fursa hii ya kutoa mawazo yangu kidogo kwani mawazo yangu mengi yameshachukuliwa na wachangiaji waliotangulia. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nakushukuru wewe Mhe. Spika, pia namshukuru Mhe. Waziri ambaye anawasilisha Mswada huu wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Usimamizi wa Sheria ya Kodi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, katika mswada huu nitamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha nisiunge mkono kwanza mpaka nipate maelezo mazuri ambayo yanaweza yakanitoa wasi wasi. Kwa sababu sheria hii inasema ni kuweka masharti ya usimamizi wa sheria ya kodi na mambo yanayohusiana na haya.

Mhe. Spika, ukiangalia katika ukurasa wa 34 inaonekana kwamba sio kuweka masharti mazuri, lakini ni kufanya marekebisho ya sheria zile ambazo zimetajwa. Sheria zile ambazo zimetajwa bahati nzuri vile vifungu ambavyo

vinaonekana vitaondoshwa lazima nikiri kwamba kuanzia mwaka ule uliotajwa mpaka leo zile sheria zake nilimozihifadhi sijazipitia na sijaziona.

Kwa mfano, sheria ya marekebisho ya sheria ya ongezeko la thamani namba ya 1998 hiyo ni sheria ya zamani sana. Mimi nakiri kwamba sheria hiyo nilipoiweka sipajui. Lakini sio mimi peke yangu niliyekosea hata huyu aliyeleta mswada huu amekosea sana kwa sababu utaratibu wa miswada kuja Barazani unatakiwa ufike kabla ya siku 21 ili wale watu ambao wanashughulikia kufanya marekebisho au kutunga sheria nyengine wapate muda wa kutafakari. Kwa hivyo, kwa muda walioleta Mhe. Waziri wa Fedha mimi kama mjumbe sikupata muda wa kuutafakari pamoja na wataalamu. Kwanza nikiri mimi sio mtaalamu lakini wapo wataalamu.

Mhe. Spika, katika ile sheria ya *VAT* ilikuwa inahusisha kwamba mtumiaji wa bidhaa analipia asilimia 20 kwa hivyo kama amenunua kwa kilo moja, amenunua gunia, aliyenunua kwa jumla sheria hiyo ilikuwa iko hivyo. Hivi sasa Mheshimiwa katika marekebisho yaliokuja sijui kwamba hapa mtumiaji au mfanyabiashara ambaye tunamfanyia marekebisho na kama tunamfanyia marekebisho mtumiaji na hofu yakuwa marekebisho haya yatamuongezea mzigo mtumiaji.

Kwa wakati huu kumuongezea mzigo mtumiaji ni hatari kubwa zaidi na hata kama unamuongezea mzigo mfanyabiashara hatari zaidi, kwa sababu mfanyabiashara anakwenda na mahesabu. Mhe. Spika, lazima tuone kwamba tunapoirekebisha hii sheria tulikuwa tujue kwamba mazingira yepi tunayotaka kurekebisha kwa kuwabana wafanyabiashara au tulikuwa tunarekebisha jambo gani. Ndio pale niliposema kwamba sitaunga mkono mpaka nipate maelezo mazuri hasa sehemu hii ya 10 kifungu cha 71,71,73,74 na 75 hapa tunaleta unafuu gani kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, katika sheria yoyote inayofanyiwa marekebisho wajumbe wanatakiwa wawe makini sana kwa sababu wanarekebisha kwa maeneo yote mawili, mfanyabiashara au mtumiaji wote hawa wanataka maslahi. Kwa muda mrefu sisi tunachokisisitiza ni kwamba serikali iongeze vianzio vya mapato. Sio siku zote kazi yetu sisi kuwabana wafanyabiashara na watumiaji tukasema tunaweka mazingira mazuri ni lazima kwamba maeneo mengine turidhie. Mhe. Spika, haiwi samaki unapomvua kwa mshipi basi akivuta sana samaki wewe kidogo uachie ili yule samaki usije ukampapua lile shavu.

Kwa hivyo, lazima tuone ni kitu gani ambacho tunakiangalia katika ukusanyaji maana tusisubiri sifa kubwa serikalini huku upande wa urai kukawa kugumu. Mhe. Spika, sio samaki tu hata *pump* kubwa ya maji kama bomba litakuwa halina pakutolea pumzi basi kuna eneo huwekwa *valve* kwamba ule upepo uwe

unapita ili maji yende kwa urahisi. Kwa hivyo, tukisema tunabana au tunachuja bila ya kuwa na maelekezo mazuri, basi tunaweza tukakosana na wafanyabiashara na pia tutawaumiza watumiaji.

Mhe. Spika, kwa kipindi kirefu sasa hivi watumiaji walikuwa na matumaini kwamba wanapata unafuu katika vyakula na vifaa vya ujenzi. Lakini madhali inakuja sheria hii ya marekebisho mimi imenitia hofu sana kwamba inaweza ikapandisha bei kidogo bidhaa zetu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha mimi sitaunga mkono ghafla mpaka nipate maelezo mazuri kuhusu huu utaratibu tutakaosimamia wakumsaidia mtumiaji au wa kumsaidia mfanyabiashara. Mhe. Spika, nikishakupata maelezo hayo sina tatizo lakini kama itaongeza chochote katika mtumiaji mimi sheria hiyo sitokubaliana nayo. Mhe. Spika, kinachotakiwa ni kwamba tuisitize serikali itafute vianzio vyengine vya mapato ili kuwapa nafuu jamii.

Mhe. Spika, jambo jengine nililokuwa nataka kulichangia ni kwenye kifungu cha 16. Mhe. Spika, katika sehemu hii masharti ya ridhaa inanitia wasi wasi kimaelezo, sielewi hasa imekusudia nini masharti ya ridhaa kwa mlipa kodi. Mhe. Spika, siku zote mlipa kodi hatakiwi awe na ridhaa anatakiwa afuate utaratibu. Kwa hivyo, tukisema kwamba mlipa kodi afuate masharti ya ridhaa tunaweza tukaja kukosa walipa kodi ambao wanalipa kodi kwa utaratibu na tukawapata wale wakarofi ambao wanapitia kwa Kamishna wakatumia kifungu hiki ikiwa tuna tatizo.

Mhe. Spika, sehemu hii naomba ifanyiwe marekebisho au tupate maelezo mazuri. Mfanyabiashara siku zote ni mjanja, na mfanyabiashara ni mtu ambaye anaweza akakwepa kodi kwa ufundi ambao anautumia. Mimi nashangaa sana kwa mfano mfanyabiashara anafanya biashara zake Dubai na soko lake liko Zanzibar, lakini ana ujanja wa kuifanya risiti au waraka wa malipo kule alikonunua ukawa mdogo kuliko bei ya bidhaa ambayo anaisafirisha na anaileta. Sasa hii nayo ni moja ya njia ambazo zinaweza zikatoa mwanya kwa sababu huko atakuwa kapata, hapa kapata, na nimepeleleza sana wako wakala ambao si rasmi hapa Zanzibar. Wanapotoa bidhaa anamshauri mtu kwamba bei halisi hii hapa kwa mfano shilingi milioni tano, lakini wewe fanyafanya toa shilingi milioni tatu ,katika hizo moja yangu na mbili zitafanya kazi.

Sasa bado ziko njia nyingi sana ambazo zinaumiza au zinaharibu sana kodi. Masharti kama haya yaliyowekwa hapa yanaweza yakatoa mwanya mkubwa zaidi baada ya ule uliyopo. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akawa makini sana katika uteuzi wa mawakala.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie hicho kifungu hasa cha Uteuzi wa Mawakala. Mawakala katika kifungu hiki ukurasa wa 30 kifungu cha 50,

tungepata sifa zao kuliko kuokota mawakala ambao wanaweza wakatia hasara sana katika utaratibu mzuri wa kukusanya kodi.

Tuna uzoefu kama kamati tunapokutana na mawakala tutachukulia mfano mawakala wa Shirika la Bima. Shirika la Bima ni zuri na ni shirika ambalo linakwenda vizuri kwa mashirika ya serikali. Lakini pale lilipoweka mawakala wa ukusanyaji au wauza bidhaa zile za bima basi yalitokea matatizo mengi. Kwa mfano, mawakala wengine wanaweza kumpa maelezo mwenye gari aitie kwenye jiti ife baadae atakuwa ndiye mshughulikiaji mzuri wa kupata yale malipo. Kwa hivyo, Shirika la Bima likawa linapata tabu sana.

Sasa, lazima tuone kwamba mawakala ambao wanateuliwa wasiwe mawakala wale ambao kaka yake ndiye Kamishna, mjomba wake awe wakala japo hana uzoefu wa biashara au usimamizi wa makusanyo. Tungependa sana tutumie yale maneno ambayo rafiki yangu Mhe. Rashid Seif hupenda kuyatumia kwamba tusiwe na ujomba katika hili, tukiwa na ujomba au huyu katoka wapi, najua haipo, lakini hii itatuharibia sana. Ningeomba sana kwamba tunapochagua mawakala wawe na sifa ambazo zinastahiki. Sifa zao pia sio wakati ule Mhe. Waziri anataka kutengeneza kanuni tungezijua mapema hawa wana sifa gani kibiashara au ki usimamizi wa kodi? Kwa sababu humu haikuainishwa kwa hivyo, tunaweza kuletewa tu mawakala ambao wao wenyewe watawataka.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atapokuja kufanya majumuisho basi atwambie sifa za mawakala wanatakiwa wawe vipi kwa sababu mambo ya fedha haya, uhasibu wake kiasi gani, mtaalamu kiasi gani, amefanya kazi ana uzoefu wa miaka mingapi. Tusiletewe wakala tu wakatangazwa lakini kumbe sifa zake sizo.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa mujibu wa kuogopa kurudia yale ambayo wameyasema wenzangu, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe baada ya kupata maelezo yale ambayo nimeyaomba, nitakuwa tayari kuunga mkono kwa kiasi ambacho nitahisi panaungika mkono. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kuweza kupata nafasi ya kuchangia mswada huu. Mimi nadhani sitokuwa na mengi sana na makubwa kwa sababu inaonekana mambo mengi tayari yamezungumzwa.
Mhe. Spika, ukienda kwenye madhumuni ya mswada huu unaona kwamba umeletwa kwa lengo la kuweka taratibu za aina moja za usimamizi wa sheria zote za kodi zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar.

Tunajua kwamba tuna sheria nyingi ambazo zinasimamiwa na Bodi ya mapato Zanzibar karibu sheria saba au zaidi. Lakini hapa zimeletwa sheria hizi tano zenye mfumo ambao unakwenda kwenye biashara.

Mhe. Spika, hili si jambo baya, lakini kama ambavyo walitangulia kusema wenzangu pamoja na yote mapato ambayo tunalenga kukusanya nimuombe Mhe. Waziri tuweke viwango ambavyo vitakidhi haja, viwango vyenye kushawishi mtu au mfanyabiashara kulipa kwa hiari, lakini pia viwango ambavyo vitawapa unafuu wananchi wetu.

Mhe. Spika, sote tunajua hali ya maisha ya Wazanzibari tulivyo, tunajua pato la Mzanzibari kwa mwaka na kwa siku, Mheshimiwa halizidi dola moja, tuseme ni kama shilingi 1,200 au 1,300 haizidi hapo. Sasa kadri ambavyo tunatengeneza hivi viwango vyetu vya mapato, lakini pia ni lazima tutizame upande mwengine wa shilingi yule ambaye tunamuwekea.

Mimi nataka nianze kwenye ukurasa wa kwanza kwenye tafsiri. Kuna neno ‘biashara’ limewekwa maana yake hapa, naomba kunukuu Mhe. Spika. Biashara maana yake ni aina yoyote ya biashara au shughuli ya biashara. Sasa mimi kidogo nina wasi wasi na hii tafsiri, kuwa biashara maana yake ni biashara. Hapa Mhe. Spika, tuna biashara nyingi mimi nadhani tafsiri ya biashara hii ingekuwa biashara maana yake ni biashara yoyote inayoruhusiwa kwa mujibu wa sheria za nchi, kwa sababu biashara tunazo nyingi na wafanyabiashara pia ni wajanja, lakini kuna zile biashara ambazo zinakubalika kwa mujibu wa sheria zetu za nchi. Unaposema biashara ni biashara tu Mhe. Spika, kwa kuwa inatia kipato mimi nadhani hatujafika huko.

Mhe. Spika, kwa sababu kwa wenzetu hata madanguro ni biashara, hata wale ambao wanajiuza basi ni biashara ambayo inatambulika na inakatiwa leseni. Sasa mimi nadhani hatujafikia huko kuwa biashara ni biashara ili mradi inatia tija. Inawezekana wafanyabiashara wetu wakaweka kama ni mfano wa *guest* likasajiliwa na kupewa leseni, lakini ikawa ndani kuna mambo ya madanguro na mambo mengine ambayo si ruhusa kufanya katika nchi yetu. Kwa hivyo, ili hili lisijelikatuletea utata mimi nadhani tungeweka kitu kilicho wazi katika hili. Kwa sababu hivi ilivyo naona kama sijui kama ni utaalamu wa uandikaji wa kisheria ambako mimi siko huko lakini naona kama haijakaa sawa.

Sehemu ya pili kuna usajili. Hii inalenga kumjua mlipa kodi, kumhakiki, kumfuatilia. Mhe. Spika, ili serikali iweze kutekeleza mipango yake usajili ni kitu cha muhimu, kwa sababu kodi kwa sehemu kubwa ndio ambayo inaendesha nchi, hata zile nchi za wenzetu ambazo zimefanikiwa na zina maendeleo makubwa ya kiuchumi basi utaona kama kodi ndio ambayo

inawasaidia sana kwa kiasi kikubwa kuweza kufanikisha ile mipango wanayojipangia.

Mhe. Spika, inaonekana kodi ambazo tunazitarajia sana kwa asilimia kubwa ndani ya nchi yetu ni zile za uingizaji wa bidhaa. Ni zile wafanyabiashara wetu ambao wanachukua bidhaa kutoka nchi za nje na kuleta kwetu kuja kuuza. Lakini ili serikali ikusanye kodi zaidi kuna haja ya uendelezaji wa uchumi wake hasa viwandani.

Jana nilishuhudia utiwaji wa saidi wa soko la pamoja, na Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Katiba na Utawala Bora alikuwepo katika hafla ile ya utiaji wa saini. Sasa Mhe. Spika, wakati saini imetiwa ya soko la pamoja sisi bado tunatarajia biashara ambazo zinaletwa na wafanyabiashara wetu kutoka nje, tunaweza tukajikuta tuko katika hali mbaya sana zaidi ya hii tuliyonayo. Kwa hivyo, serikali ione na itilie maanani juu ya umuhimu wa kurejesha vile viwanda, japo imeonekana kama viwanda vikubwa sana haiwezekani, lakini hata vile viwanda vidogo vidogo ambapo tunaweza tukatengeneza bidhaa zetu angalau zikenda katika hili soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, ni lazima tukubali viwanda kuwa vinainua uchumi wan nchi. Kwa bahati nzuri mimi nimesoma kidogo katika mambo ya biashara, siku moja nilikwenda darasani nikamkuta mwalimu wetu tayari keshachora kitu ukikiona kimekaa kama yule mungu wa Kibaniani kwenye ubao, kachora duara halafu lina mikono. Mimi nikaona haya leo makubwa, lakini kumbe alikusudia kutoa mfano wa kiwanda ambacho kinaweza kikaleta tija ndani ya nchi.

Mhe. Spika, mkono mmoja wa kiwanda kile alionesha ni namna gani ambavyo unachukua *raw material* kutoka nje yanakuja kwenye nchi. Yakija kwenye nchi yale yanalipiwa kodi, mkomo mmoja ni kuajiri wafanyakazi wa kile kiwanda, mkono mmoja kuna ulipiaji wa umeme na maji, mkono mmoja kuna wataalamu ambao tutawaagiza labda kutoka nje waje wasaidie kile kiwanda kutupa utaalamu ambao hatuna. Lakini Mhe. Spika, mkono mmoja ulio mkubwa ni kuweza kutoa ile bidhaa na kuipeleka nje ambapo napo pia tunapata kodi.

Kwa hivyo, kitu kimoja, kiwanda kimoja unaona tunapata kodi kutoka mikono saba au nane na ndio maana mimi nilipoona lile *diagram* nikaona kama ni Mungu wa Kibaniani vile alivyochawanya miguu na mikono Mhe. Spika.

Sasa kama kweli tuna nia ya kuongeza pato Mhe. Waziri anasinzia sijui kama ananisikia, kuna haja ya kuhakikisha kama tunarudisha viwanda ndani ya nchi, hususan katika changamoto hizo zinazotukabili za soko la pamoja.

Mhe. Spika, kwenye usajili nambari 2, inaeleza mtu kuweza kusajili biashara yake zaidi ya mara moja. Hapa nilikuwa nataka maelezo ya ziada, sijui Mhe. Waziri alikusudia kitu gani na hapa ndipo ninapoiona ile haja ya mambo kama haya muhimu yanapoletwa barazani tukawa tunapata mafunzo au semina ambazo zinatuwezesha kuweza kuchangia wajumbe wako wa baraza.

Mhe. Spika, kuna biashara ya ujenzi, nguo na vipodozi. Lakini kwenye biashara ya nguo unaweza ukakuta kuna mambo mengi ambayo yanaendana na nguo, sasa hapa kwenye mswada huu sijui wamekusudia kua mimi nauza hijabu ,niorodheshe, banio la nywele niorodheshe, wengine wamesema mabegi kwa sababu utakuta maduka ya nguo kuna na mabegi yananing'inia uorodheshe au vipi. Au kwa wale wanaouza biashara za ujenzi wana bati waorodheshe, saruji au nondo waorodheshe, kama mimi duka langu ni la ujenzi lakini ninauza bati, saruji na nondo. Mimi duka langu ni la vipodozi nauza nywele za kubandika, poda na perfume.

Mhe. Spika, hapa bado mimi sijapafahamu na ikiwa wananchi hawatajua hasa unakusudia nini inaweza ikawaletea matatizo baadae kutokana na biashara zetu zilivyo, hatuna biashara za nchi ambazo zimeendelea kama unakwenda kununua kitu basi soko zima kuanzia Darajani mpaka Amani huko ni mikanda tu ya suruali na viatu, soko zima huko ni nguo tu za watoto hatujafikia huko. Wafanyabiashara wetu wengi biashara zao ni za mchanganyiko. Sasa sijui hapa Mhe. Waziri alilenga nini hasa?

Lakini pia kwenye huo huo usajili nambari 3, tunaelezwa kuwa pia mfanyabiashara anayefanya biashara zaidi ya eneo moja pia itabidi ajisajili hivyo. Sasa inawezekana Mhe. Spika, najitolea mfano mimi mwenyewe ni muuzaji mkubwa wa *pampers* za watoto tuseme, lakini nina duka langu kubwa yaani makao makuu na ninazo branji zangu ndogo ndogo ambazo nachukua bidhaa zile na kupeleka. Sasa kwenye huu usajili duka moja liko Kwahani na jengine liko Majestiki, makao makuu yangu yako Majestiki, lakini branji yangu iko Kwahani na nyengine Amani, jengine liko Makunduchi, sasa sijui utatakiwa usajili kwa kila duka wamekusudia au duka moja kama ni makao makuu na hizi nyengine zitakuwa ni *branch* tu, na viwango vyake vya usajili pia nadhani havitakuwa sawa kati ya makao makuu na zile *branch.*

Mhe. Spika, naomba ufafanuzi wa hilo.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 7(2) kuna kufuta usajili. Kamishna kapewa uwezo wa kusajili au kuzuia usajili. Sasa kama ambavyo wamesema wenzangu ambao wametangulia. Kwanza huyu Kamishna ni mtu, tusitizame tukaweka kigezo kwa yule aliyepo, inawezekana aliyepo ni mtu mzuri tu lakini ni binadamu anaweza akamaliza muda wake akastaafu na mambo mengine kama

hayo. Ijapokuwa hapa nimeona mwisho huku kuna kukata rufaa, lakini inaonekana kama kamishna huyu kapewa madaraka makubwa mno na mengi ambayo hata bodi sijui kama itakuwa na kazi ya kufanya, kazi zote kapangiwa Kamishna kuzifanya.

Lakini zaidi ya hayo, mimi nikipima haya madaraka ambayo kapewa kamishna wingi wake na adhabu zilizomo humu kila kifungu kuna kifungo, Mhe. Spika, ni mtihani wakati yule ni binadamu. Zaidi ya hayo, madaraka hayo makubwa sijaona kifungu hata kimoja iwapo yeye atafanya makosa, atafanywa nini, au atachukuliwa hatua gani, naona ya mfanyabiashara tu, faini, kifungo kuna vifungo mpaka vya miaka 10.

Mhe. Spika, kweli tuna nia ya kuimarisha kodi au tuna nia ya kuwafunga pingu hawa wafanyabiashara wetu wawili watatu ambao tumebakia nao na tukawafurusha kabisa wakaondoka machoni. Wafanyabiashara wengi wemetukimbia ukweli ni huo, mwaka 1995 na 2000 ni tofauti na leo na mambo kama haya ya kero ndogo ndogo ambazo tunazidharau ndizo zinazotuumiza, ni lazima turudi tukae tusimpe mtu madaraka kama aliyekuwa ni malaika. Kuna bodi lakini haionekana kama itakuwa ina-*function* kwa sababu yote yaliyomo humu kaelekezwa Kamishna.

Mhe. Spika, mfano kama huu hiki kifungu cha 11(1) kinampa uwezo Kamishna akipata tetezi tu kama kua mtu anafanya biashara bila ya kusajiliwa basi aweze kumsajili yule mtu. Utamsajili vipi mtu bila ya kumwita, kumhoji, Mhe. Spika, tujijue kama sisi ni binadamu na tusijipe madaraka ambayo yanatoa ile sifa ya kibinadamu kama ni malaika huna kosa ni lazima madaraka mengine tutizame kama huyu kamishna wetu tumempa madaraka ambayo ni makubwa sana.

Kifungu cha 9(1) kuna cheti cha usajili na kimeonesha cheti hiki kuwa ili usajiliwe, basi jina la mfanyabiashara ambalo sina tatizo nalo, jina la biashara yenyewe, sehemu ya biashara na *tin number*. Sasa mimi nasema wafanyabiashara wetu wako kimakundi na sioni kama hii sheria imefafanua.

Mhe. Spika, tuna wafanyabiashara watatu, tuna wafanyabiashara, tuna watafuta chejio, kuna hawa *frame* bega leseni mbio, wote hawa naona tumewaweka kwenye wafanyabiashara. Mimi nakwenda kwenye biashara Mhe. Spika, unajua hilo, ninaona wale watafutaji chejio sio wafanyabiashara ni watafutaji chejio, kwa sababu siku zote pesa inachuma pesa nguvu inachuma chejio, sasa wale watafutaji chejio dola 2000 au 3000, tiketi ya kukopa, wanaweza wakakusanya mizigo yao yote, kama wafanyabiashara tisa. Kuna mfanyabiashara huyo keshachukua makontena yake wakenda abaa na mie niakilia, ikapimwa pale kwa kilo uzito ukajulikana, haya basi wewe utalipa kiasi fulani. Sasa huyu nae pia tunamuweka kuwa lazima awe na tin number,

huyu mtafuta kijio, fremu bega leseni mbio. Mhe. Spika, nao pia tunawahitaji hawa kwa sababu nao wanafanya kazi zao za halali wanajipatia rizki na watoto. Namuomba Mhe. Waziri hili nalo alitazame.

Mhe. Spika, kifungu cha 14 (1) kuna "Usajili wa vifaa vya kuhifadhia bidhaa". Hapa mimi sijafahamu naomba Mhe. Waziri pia atakapokuja anifahamishe. Ni bidhaa za mfano upi ambazo zimekusudiwa vifaa vyake ni lazima uvisajili. Kwa sababu hizi biashara zipo nyingi inawezekana mimi nauza malai au koni, kwa hivyo hapa ninavyohisi kwa sheria hii itabidi nisajili nina freezer ambalo nagandishia hizo koni, lakini nina vibakuli vile vya koni. Mhe. Spika, hapa nataka maelezo ya ziada ni biashara zipi na za aina gani ambazo zinahitaji huo usajili.

Mhe. Spika, kifungu cha 15 "Taarifa ya mabadiliko" inayoeleza kwamba unapofanya mabadiliko ya biashara yako utoe taarifa kwa Kamishna kwa mwezi mmoja. Sasa biashara zetu kama nilivyosema, wengi wa wafanyabiashara wetu tukiondoa lile kundi kubwa ni wa kubahatisha, unakwenda kwa namna ya upepo unavyokwenda. Unaweza ukatoka hapa na kwenda kuchukua nguo, lakini ukifika ule ukaona kuna *sale* ya *handbag*, viatu na mikanda ya suruali.

Mhe. Spika, kuna biashara ambazo mimi nakubaliana unaweza ukatoa taarifa, lakini zile biashara ambazo za viwanda, leo hutaki tena kutengeneza maji unataka kutengeneza juice ya embe hapo unatoa taarifa kwa Kamishna. Lakini hizi biashara zinazokwenda kwa upepo unavyokwenda, utoe taarifa kwa Kamishna kwa mwezi mmoja na ikiwa hukufanya hivyo kuna kifungo na faini, sidhani kama kweli tuna nia ya kuwasaidia wafanyabiashara wetu.

Mhe. Spika, kifungu cha 31 kuna "Tarehe ya malipo ya kodi". Hapa tunaelezwa na kumewekwa tarehe ya malipo ya kodi. Iwapo mfanyabiashara wetu atashindwa kulipa kwa tarehe ile ambayo kawekewa basi napo ndio nikasema hii imejaa kifungo na faini. Lakini haikuelezwa hapa kama tutamjuaje yule mfanyabiashara kuwa ile tarehe 25 ambayo kawekewa alipe hakuweza kulipa. Kuna sababu gani za msingi ambazo zimemsababisha asiweze kulipa. Ni binadamu ingetazamwa, lakini Kamishna kukaa tu ikaonekana kama hakulipa na adhabu hizi zikaweza kufanya kazi sidhani kama tunamfanyia haki mfanyabiashara wetu.

Inaonekana hapa itabidi tujenge jela kubwa kwa ajili ya wafanyabiashara wetu. Kwa sababu kashindwa kuna faini, kuna riba, lakini bila ya kutazama ni kitu gani ambacho kimesababisha ashindwe. Tumeonekana kama ni waunda ngoma tunajivutia sisi. Kwa sababu hapa imeelezwa kwamba iwapo siku ya mbele

yake ya ile siku yako ya kulipa kuna sikukuu au tuseme si siku ya kazi basi ulipe siku moja kabla ya ile tarehe yako ambayo umewekewa.

Lakini hapa haikuwekwa kama labda kuna siku ambayo itakuwa sio ya kazi tuseme leo ni tarehe 25 unatakiwa ulipe tarehe 24, ikiwa tarehe 25 ile itakuwa sio siku ya kazi. Haikuelezwa kama unaweza kulipa tarehe 26 baada ya siku ile ya kazi. Mhe. Spika, kweli biashara hiyo ya upande mmoja itakwenda. Sisi tunahitaji kodi lakini tunawahitaji wafanyabiashara, sasa yale maneno ya wenzangu waliosema hawa tutawafanya tuwakamue mpaka baada ya damu watoke maji, mimi naona mwisho itakuwa ni donda utoke usaha tuwakose kabisa.

Lakini Mhe. Spika, kifungu cha 33 (2) naomba kunukuu. "Kiwango cha riba kitatozwa chini ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki kitakuwa kiwango cha biashara cha mikopo ya benki pamoja na asilimia tano ya ziada kwa mwaka".

Mhe. Spika, Benki ya Biashara tunajua ni namna gani ya riba zake ambazo zinatoa na siku zote hapa tunakuwa tunapigia kelele suala hili, lakini inaonekana bado serikali inaling'ang'ania na haijataka kutufahamu. Kwa nini iwe ni kwa Benki ya Biashara na isiwe ile riba ambayo itatolewa iwe ni kwa sawa sawa na Benki Kuu. Ni lazima tuwafikirie na hawa watu tusijivutie sisi tu.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman juzi alisema ile ya bata kutaga yai la dhahabu ukamchinja ukaona ni bora upate kwa pamoja yote ambayo yatakuwa tumboni, ndio mfano wa haya.

Mhe. Spika, hapa pana kifungu cha 40 (1) "Malipo kwa awamu". Mhe. Spika, katika kipengele kimoja hapa ambacho nimeona kimewasaidia wafanyabiashara wetu ni hiki. Kwa kweli hiki kidogo kitaweza kuwapa pumzi wafanyabiashara wetu kwa wale ambao wanaonekana si wakorofi na wanajitahidi kulipa, basi haya malipo ya awamu ni vizuri kama yalivyowekwa wafanyiwe. Mhe. Spika, kile kivutio nilichosema ni mfano wa hiki, kuwafanya wavutike, kuwafanya walipe kwa hiari, kuwafanya walipe bila ya hiyo kwenda na polisi mkafanya mambo ambayo hayaleti maslahi ndani ya nchi.

Mhe. Spika, kifungu cha 44 Kamishna kapewa uwezo wa kujilipa. Iwapo mlipa kodi atashindwa kulipia kodi ile ambayo anadaiwa atapeleka kesi ile Mahakamani na Kamishna ana uwezo wa kujilipa.

Mhe. Spika, mimi kinachonishtusha ni hizo njia za kujilipia. Hili nitarudia kusema ule uwezo mkubwa ambao kapewa Kamishna. Kesi imekwenda Mahakamani na imeonekana kama Kamishna ni lazima alipwe. Ni kwa nini basi dhamana hii iwe ni ya Kamishna. Hatuna dalali ambaye anauza mali ya

serikali, kesi ikitoka Mahakamani akakabidhiwa dalali na yeye ndio ikawa muuzaji wa ile mali na Kamishna akasubiri kupewa chake mkononi. Kwa nini yeye Kamishna awe ndio mkamataji.

Lakini kwenye kifungu hiki Kamishna anaweza kuvamia nyumba yoyote au jengo lolote na kukamata bidhaa yoyote akishirikiana na polisi tu. Kwa hivyo, hii bado iko upande mmoja. Kama kuna matatizo ambayo yatamfika Kamishna wetu ni hapa kwa sababu na wafanyabiashara kama tulivyozungumza nao ni wajanja. Hii kesi haitakuwa moja ya kupeleka mtu Mahakamani. Hapa haikueleza upande wa pili wangechukua nafasi gani katika hili. Hii kweli Kamishna na polisi tu awe ndio kielelezo tosha cha kuweza kwenda kuingia katika jengo la mtu au duka akaweza kuchukua bidhaa yoyote na kwenda kuiuza. Kweli ni haki Mhe. Spika. Kwa nini usipewe nafasi upande wa pili kuwa yeye mwenyewe au wakala wake ikawa nay eye ni shahidi katika lile zoezi ambalo linafanyika pale.

Lakini mbali ya hayo, pia haikuelezwa kama ile bidhaa ambayo anaichukua Kamishna basi ilingane na soko na kile ambacho kitachukuliwa pale. Kama nilivyosema Kamishna ni binadamu anaweza akawa kishaona kesi hii kwenye duka hili kuna kitu fulani, kwa hivyo akaweza kuwapanga watu wake ambao anaweza kuwauzia ile kwa bei ya chee. Sasa badala ya kuwa tunamsaidia yule mfanyabiashara wetu ikawa tunamkomoa. Kwa hivyo, nadhani hili Mhe. Waziri alione, kwanza ile bidhaa ilingane na soko ambayo itauzwa, isiwe kama kitu kina thamani ya milioni kikenda kikauzwa laki moja itakuwa hatumsaidii mfanyabiashara.

Lakini pia wakati anapokwenda Kamishna na polisi basi na upande wa pili uwepo. Lakini pia la tatu kwa nini tumbebeshe huu mzigo Kamishna, tutakuja kumpigisha rungu la kichogo huyu kama kafumaniwa au atakuja kwenda jela huyu. Kwa sababu tunaye dalali wa mali za serikali kwa nini awe Kamishna ndio muuzaji.

Mhe. Spika, mimi naomba nimalize kwa haya madogo ambayo nimezungumza lakini kuleta ombi kwako. Mhe. Spika, sisi ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao tumeletwa hapa na wananchi kuja kuwasemea matatizo yao, kuja kuwapitishia kitu ambacho kitaleta maslahi ndani ya nchi. Lakini kwa nini mawaziri wako wanatugeuza sisi kuwa ni *rubber stamp.* Mhe. Spika, dubwasha kama hili kanuni inaeleza ni namna gani ya mjumbe anavyotakiwa kupata mswada unampa leo, kesho aje achangie, unatarajia nini Mhe. Spika, kama si kudhalilisha Baraza lako.

Mhe. Spika, toka juzi nimeingia nilikuwa nina malaria yale ambayo hayaonekani kwa vipimo lakini unaona dalili. Kwa hivyo, hapa nilikuwa nipo

nipo tu. Nimejaribu kuupitia jana usiku lakini nilipokuletea ile karatasi ya kuwa nitachangia kutokana na kuona hali ilivyokuwa ndani ya Baraza, ilikuwa Mhe. Spika, karibu unakamatia. Maana yake unasema majadiliano yanaendelea tunatazamana, mimi namtazama Mhe. Ame Mati Wadi tunahimizana, sasa inakuwa kama tunaburuza hatufanyi kitu ambacho kitaleta maslahi. Mswada kama huu ambao umejaa vifungo, rufaa, faini si chini ya zaidi ya miaka kumi leo tunakuja kukaa hapa mia kwa mia.

Mhe. Spika, mimi nawashangaa wale ambao wanasema ninaukubali mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wangu. Unawasemea wananchi wako ambao hawajui kitu kilichomo humu, hujenda kuwauliza, hujenda kutafuta mawazo yao watakwambia nini kuhusu hilo. Mhe. Spika, wasitufanyie hivi litaonekana Baraza lako halina uwezo wakati mimi naamini hakuna mwanagenzi humu ndani. Hata Mhe. Asha Moh'd Hilal ambaye kaingia juzi na uzuri wake ana sifa ya ualimu tayari si mwanagenzi tena. Leo tunakamatiana hapa nenda wewe tunaliburuza tumeshaambiwa kuanzia tarehe 15 mpaka 31 tunataka liende tu siku zetu zisikatwe. Hatufiki Mhe. Spika, inawezekana tutimize wajibu wetu.

Mhe. Spika: Suala hili alilolitaja Mhe. Zahra Ali Hamad ni la kweli liko ndani ya kanuni kwamba miswada ipatikane mapema. Tumelizungumza kwa mapana sana ndani ya vikao vyetu vya kamati ya uongozi, kwenye *briefing* zetu na mjumbe amelizungumza hapa ndani ya Baraza.

Niiombe serikali basi ione ukweli huo na tufuate taratibu za kanuni kwamba miswada ipatikane mapema siku 21 kabla ya kuwasilishwa kusomwa kwa mara ya kwanza. Tujitahidi iwe hivyo.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala kwa kutuwezesha kuifikia siku hii na muda huu tukiwa bado tupo hai.

Mhe. Spika, mimi nataka nipate fursa fupi sana ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi. Mhe. Spika, mimi mswada huu ningependa sana niuchangie kiujumla jumla kwa sababu wajumbe wengi wameshaupitia kifungu kwa kifungu hadi mjumbe ambaye sasa hivi amekaa kitako amejaribu kupitia kifungu kwa kifungu kwa kadri alivyoweza.

Mhe. Spika, mimi nataka nioneshe wasi wasi wangu juu ya masuala mazima ya haya mambo ya kodi. Mhe. Spika, watu wengi humu katika Baraza lako wameshatembea nchi mbali mbali hasa hawa Mawaziri. Miongoni mwa Wajumbe wa Baraza hili wengine huwa wanafanya biashara kama ambavyo Mjumbe amesema. Lakini nasikia sina hakika maana mimi ukitoa Tumbe na bandarini kule sina ninapokwenda pengine labda Afrika ya Kusini.

Sasa basi, katika hali hiyo Mhe. Spika, kuna mambo mengi siyajui lakini kwa sababu nimo katika dunia hii ambayo wanaishi wanadamu, nasikia kwamba katika dunia hii tuliyoko masuala haya ya ukusanyaji wa kodi katika nchi nyingi duniani hukusanywa na chombo kimoja tu. Nchi hizo hufanya hivyo kwa maana ya kutaka kudhibiti kodi na kutaka kudhibiti hali halisi ya ukusanyaji wa mapato yenyewe katika nchi.

Lakini hapa kwetu Mhe. Spika, kinchi kidogo mno hiki, ni nchi ya visiwa viwili tu, nchi ambayo mpaka leo hii bado hatujafikia milioni mbili pamoja na watoto walioko kwenye matumbo ya wazazi wao. Mhe. Spika, nchi hii inakusanywa kodi na vyombo viwili, *Zanzibar Revenue Board (ZRB)* na *Tanzania Revenue Authority (TRA).*

Mhe. Spika, hapo kabla wakati wa utawala wa Rais aliyemaliza muda wake Dk. Salmin Amour Juma suala hili la *TRA* ndipo lilipozuka. Kwa kweli serikali ya wakati huo haikuwa rahisi kulikubali hili jambo lakini ilifika wakati nguvu ikawa kubwa kutoka huko ambako lilianzia na badala yake likaingia Zanzibar. Lakini Mhe. Spika, suala hili waliokuwepo wakati huo walilikataa kwa maana ya kuona kwamba hili jambo litakuwa ni zito na watawatwisha mzigo mzito Wazanzibari ambao ni wanyonge na ni maskini.

Mhe. Spika, leo tuna *ZRB* lakini kabla ya hapo Zanzibar ilikuwa ina ustawi mzuri mno wa biashara zake, wa shughuli zake kwa sababu chombo ambacho kilikuwa kinasimamia kodi hapa Zanzibar *Incometax* ilikuwa ni chombo kinachosimamia kodi kulingana na hali halisi za watu wenyewe walivyo na walivyo na uwezo navyo.

Lakini Mhe. Spika, mimi sijawahi kuona mke moja kuwa na waume wawili ndani ya nyumba moja. Mfano wa hili ni huu ukusanyaji wa mapato kwa mtu mmoja kukusanya mapato ya ndani pamoja na watu wengine ambao tunasema ni wenzetu.

Mhe. Spika, tuangalie jambo moja katika hili tutapata kigezo kizuri. Kabla ya hali hii kwa sababu mtu anapokuwa na nia yake ambayo wewe huijui atakulazimisha kulifanya jambo ambalo unalihisi litakuwa na uzito lakini akakuzidi nguvu lile jambo ukalifanya, basi litakuwa na athari kubwa baadae kwa sababu yeye ameshaona anafanya vile kwa nini lakini wewe unayefanyiwa hujajua kitatokea nini zaidi ambacho kitakuathiri.

Mhe. Spika, kila mtu ni shahidi hapa. Zanzibar wacha Tanzania Bara, hizi nchi za Afrika Mashariki zote zilikuwa zimekuja Zanzibar hapa kuchukua mizigo na kufunga bidhaa zake na halafu kurudi katika nchi zao na hapo nchi ikaweza

kutangazika vizuri sana kibiashara. Lakini baadae Mhe. Spika, Zanzibar licha ya watu kutoka katika hizo nchi ambazo nimezisema kama vile Kenya, Uganda, Comoro na nchi nyengine za karibu, sisi Wazanzibari wenyewe sasa hivi tunatoka hapa tukenda Bara kufunga mizigo tukirudi hapa na wengine wakenda mpaka Tumbe kule wanachukua mizigo Dar es Salaam. Hii ni kuonesha namna gani azma ya watu hawa ilivyokuwa ndani ya kisiwa chetu hiki. Hilo moja.

Mhe. Spika, kabla ya hapo Zanzibar tulikuwa tunakwenda vizuri, lakini leo hapa Zanzibar tumefika wakati ukiangalia hali halisi ya hapa mjini na pale Dar es Salaam, ukifika Dar es Salaam sasa hivi unafikiri ni Ulaya kwa sababu ya majengo yake na ustawi wa biashara zake.

Leo Mhe. Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo mpaka wale wa kwenda kununua chupi za kutembeza humu barabarani wanakwenda kuchukua Dar es Salaam kwa sababu wao lengo lao ilikuwa ni kuimarisha zaidi nchi yao na sisi kutuweka katika hii hali ambayo tukonayo. Baada ya hali hii kinachofuatia ni ugomvi wa wenyewe kwa wenyewe tu kila siku.

Mhe. Spika, mimi nadhani umefika wakati sasa wa serikali kuuona umuhimu wa hiki chombo *ZRB* ambacho kipo hapa Zanzibar kukusanya mapato yake kwa sababu ya ustawi wa nchi yake pamoja na wananchi wenyewe. Lakini huwezi kusema kwamba *ZRB* eti basi iwe ni wakala. Kwa nini *ZRB* iwe ni wakala wa *TRA*? Sisi watu wa Zanzibar tunahitaji chombo chetu kitusimamie. Sio umchukue mtu mwenye mamlaka yake, mwenye haki yake, halafu ukamwambia rafiki yake basi wewe chukua mamlaka haya kama vile tunakuoza mke. Maana yake kama una mwanao unataka kumuozesha wewe hupo unaweza kumpa mamlaka hata Mhe. Machano Othman Said ukamwambia niozeshee mwanangu.

Sasa Mhe. Spika, sisi wenyewe tupo tuna chombo chetu na hapa ndipo tunapokuja kujidharau hawa watu wa Bara wakatuona hatuna maana hata kuwepo hapa. Ndio maana baadae tunatangaziwa majina mengi, mara ni nchi, si nchi kwa sababu ya utaratibu kama huu.

Mhe. Spika, sisi hatujauza uhuru wetu, sisi tuna mambo yetu katika nchi yetu. Leo tumewafanya Wazanzibari wenyewe wote wakahamie Bara, kwa nini wa Bara hawakuja hapa, ni kwa sababu hili ndio lililokuwa azma yao na ndio lengo lao kutufanya sisi kila kitu iwe tunawategemea wao.

Mhe. Spika, mimi nafikiri kwa sababu Mhe. Waziri ni rafiki yangu na ataliona hili umuhimu wake, afike pahala aone kwamba anachokifanya anakifanya kwa sababu ya Wazanzibari na ustawi wake.

Mhe. Spika, ipo haja ya kukipa nguvu chombo chetu *ZRB*, kukipa mamlaka kamili. Isiwe sasa ni nchi ambayo haijapata uhuru halafu inaambiwa tutakupa uhuru wa ndani kwanza baadae tunakuja kukupa uhuru. Hapana, *ZRB* ni chombo ambacho kipo kisheria kwa hiyo tukipe mamlaka kamili ya ukusanyaji wa kodi za ndani hatutaki *TRA* kutukusanyia hapa wanatunyang'anya. Maana baadae wanasema wakishakuzikusanya wanawapa serikali wenyewe.

Kwani sisi hatuwezi kukusanya mpaka tukusanyiwe na mtu huko halafu aje atwambie chukueni. Kwani tuna kasoro gani. Sasa kama tuna kasoro hatuwezi kukusanya hata hii *ZRB* basi kuwepo kwake isiwepo wakusanye wao halafu watupe. Lakini kama *ZRB* ni chombo ambacho wenyewe tunakiamini kipo kisheria basi watu ni wachache, watu milioni moja na kidogo tu kwa nini wasiweze kuwasimamia. *ZRB* wana uwezo mzuri kusimamia mambo yetu na hayo mapato yakaongezeka hata kama ingelikuwa mapato haya ni taratibu taratibu wanachukua kidogo kidogo, basi pato lake lingelikuwa ni kubwa zaidi kwa sababu haligawiki maeneo mawili.

Unajuaje, una uhakika gani vyombo hivi viwili kwamba hiki kimoja nacho kitakuwa kinasimamia mapato na halafu kinarudisha katika hali ile walivyoyakusanya. Huna uhakika huo kwa sababu hao wanaokusanya nao ni binadamu, kwa nini wasikusanye hawa.

Kwa hiyo, mimi ushauri wangu Mhe. Spika, naomba kwamba kama tunawapenda wananchi wetu ndani ya visiwa hivi tusiwatungie sheria ngumu.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri ataona umuhimu wa chombo hiki kukipa nguvu kamili. Kwa sababu sisi humu ndani ya chombo hiki ndicho chombo tunachokikubali zaidi na ndicho chombo tunachokuwa tukikipangia sheria. Mhe. Spika, kwa kuwa sisi tunawawakilisha Wazanzibari hapa ndani ya chombo hiki hatuwawakilishi Watanzania, sasa basi tupewe hiyo fursa ya kuwa wawakilishi wa Wazanzibari kweli kweli. Kwa hiyo Mhe. Spika, Mhe. Waziri aone umuhimu wa kukifanya chombo hiki ndicho chombo cha kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa Wazanzibari. Kwa sababu hii *TRA* iliyoko hapa, sina hakika Mhe. Spika, labda nimuulize Mhe. Waziri, kule Tanganyika kuna *ZRB*? Sasa kama hakuna kwa nini wao waje kutukusanyia hapa. Maana ingelikuwa na hii *ZRB* iko kule, wao wangesema aah! Lakini na nyinyi mko huku. Wao wako huku kwetu lakini kule kwao sisi hatuko, maana yake sisi vya kwetu tuko shirika, lakini vya kwao ni vyao peke yao.

Mhe. Spika, hakuna jambo kama hili. Kwa hivyo, huku ndio kuoneana kwa dhahiri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, binaadamu hufikiria mambo mbali mbali

kulingana na hali iliyopo. Sasa tubadilikeni, kwa sababu ya ustawi wa watu wetu.

Mhe. Spika, nije katika ujumla huo huo wa uchangiaji. Mhe. Spika, kwanza kuna suala hapa la ukusanyaji wa asilimia hii 50. Kwanza hili ni kubwa. Mhe. Spika, ukusanyaji wa asilimia 50 ni mkubwa mno na huu ndio uliowafanya wafanyabiashara wengi wakimbie hapa. Maana Bara ni nchi kubwa, kwetu hapa ni ndogo. Kwa mfano, ukimchukua yule tajiri wa Bara na uje kumchukua tajiri wa hapa, basi itakuwa ni mara nne au mara tano kwa yule wa Bara.

Mhe. Spika, ikishakuwa ushuru hapa ni asilimia hii, maana yake huyu atatafuta unafuu na ataondoka hapa atakwenda zake huko kwenye unafuu. Ndivyo hivyo hivyo kwa wafanyabiashara wa nchi mbali mbali zamani walivyokuwa wanakuja kutafuta unafuu hapa, zamani unafuu ulikuwa huku Zanzibar na ulikuwa hauko Bara. Ni wafanyabiashara hao hao sasa hivi waliohama Zanzibar na wemekwenda Bara kutafuta unafuu wa biashara zao, kwa sababu kila mtu anayefanya biashara basi anafanyabiashara akitarajia na faida. Sasa hawa wa hapa ndani wote wamekimbia na kwa sheria hizi basi watakimbia zaidi na watamalizika na kubakia wauza vinyago tu hapa, na vinyago haviliwi.

Mhe. Spika, mimi nadhani ni bora kupata kidogo kila siku kuliko kutarajia kikubwa kwa mwezi mzima. Nadhani tukae tufikiri upya namna ya kusubiri kuja kupata kingi ambacho wakati mwengine hutokipata, na kupata kidogo ambacho una uhakika nacho. Hapa sasa ndipo inapokuja ile haja ya kumfanya mfanyabiashara atowe kodi kwa hiyari yake, kwamba tukimpangia unafuu wa mambo basi huyu halazimiki kukimbia na kukwepa kodi, kwa sababu na yeye anajua wajibu wa biashara yake na anajua wajibu wa kulipa kodi na kuifanya nchi iende na ustawi wa mambo mengine. Lakini kodi ikishakuwa kiwango hiki, kwa kweli hiki kiwango ni kikubwa mno.

Mhe. Spika, mimi nafikiri, sikupangii lakini, wala simpangii Mhe. Waziri juu ya jambo hili, ila namshauri tu kwamba aone kuwa anafanya nusu ya hii au kuzidi kidogo tu, ili kumpa unafuu mfanyabiashara na kuistawisha nchi yetu.

Mhe. Spika, tunaweza kulingana na nchi yetu ilivyokuwa na maisha magumu, tunaweza tukayatafuta mambo na tukayafanya kuwa nafuu, ili kuwavutia wafanyabiashara mbali mbali ikiwa ni pamoja na wale wafanyabiashara wetu ambao hapa wameondoka ili warudi nchini kwetu, halafu baadae tunaweza tukenda hatua kwa hatua kupata hichi kiwango tunachokitaka. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia kesho na kesho kutwa tukipata mafuta yetu basi tunaweza tukazidisha baadhi ya mambo, lakini tusubirini ili tupate mambo mengine ambayo yataweza kuziba hapa, halafu ndipo tunaweza kumwangalia mfanyabiashara sasa kwa hali tuliyokuwa nayo, na kumwambia kwa hali

tuliyokuwanayo sasa wewe utalipa kodi ya biashara mpaka kiwango hiki. Lakini kwa sasa hivi kiwango hiki ni kikubwa mno, ndopo hapo wafanyabiashara wanapokimbia na kukwepa kodi na hata akiwa ndani anakwepa na kufanya hadaa na ujanja.

Mhe. Spika, Mhe. dokta Hija Hassan hapa ameniambia kwamba katika nchi alizotembea, au nchi nyingi ukenda na ukitaka kununua chochote kile, basi unapewa risiti kwa maana ya kwamba ule ushuru ndio pale unafungika zaidi, hakuna mtu anayekwepa, kwa sababu hakuna anayeona tabu kuandika kinachonunuliwa.

Lakini Mhe. Spika, kwa hapa ukenda kwenye duka la watu ambao wana risiti na ukinunua kitu cha Shs.200,000/= basi anaweza kukuambia, bwana wee chukua Shs. 5,000/= mimi naandika Shs. 50,000/=, kwa sababu anajua kuna siku atakaguliwa basi akute kwamba ule ulipaji wake wa kodi umekuwa mdogo zaidi kulingana na vile ambavyo alivyouza.

Kwa hivyo, hii ni kwa sababu ya huu ushuru umekuwa ni mkubwa mno. Mimi nadhani Mhe. Spika, tuige utaratibu wa zile nchi ambazo dokta Hija Hassan ameziona na ule utaratibu wa kwenda kununua na halafu mtu akaandika risiti kulingana na kile alichouza, nadhani hii itatusaidia zaidi.

Mwisho Mhe. Spika, mamlaka aliyopewa kamishna pamoja na wajumbe wengi kuchangia, Mhe. Spika, mamlaka haya ni makubwa, kwa nini ni makubwa? ni makubwa kwa sababu huyu ni binadamu na mazingira ya sheria hii yeye hayakumfunga hata pahala pamoja, isipokuwa yamempa uwezo zaidi kuweza kusimamia yale mambo yanayoonekana kwamba hapa yataleta tija serikalini au katika ukusanyaji wa mapato yake.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sheria kama hizi kuwe na sheria ambazo zinambana kidogo kwa sababu na yeye ni binadamu, sio kwa sababu ni kamishna tena iwe ndio hana kosa. Kuna vitu vingi vinaweza vikatokea hapa vikasababisha uharibifu na vikasababisha mazingira mbali mbali ambayo anaweza kuyasababisha yeye kupitia hayo mamlaka aliyopewa. Mimi nafikiri Mhe. Spika, wapo watu wengi katika nchi waliokuwa hawajui kuzifuatilia haki zao baada ya pale wanapopata matatizo.

Mhe. Spika, mfano suala hili kupata *appeal*, kama dokta Hija kukata *appeal* anajua wapi. Huyu ukishamnyang'anya leseni yake, basi atalalamika Mwenyezi Mungu yuko tu basi yamekwisha, mpaka hiyo siku utakayotaka kama utamwachia au hukumwachia basi. Lakini sio kila mtu Mhe. Spika, anauwezo wa kujitetea.

Mhe. Spika, mimi nafikiri kungekuwa na chombo maalum kifanye uchunguzi kwanza na kione kwamba huyu mtu anastahili kulingana na hiki wanacho kilalamikia, ili kusudi kupewa mamlaka na yeye kuonyeshwa njia ya kujitetea.

Mhe. Spika, kwa mswada kama huu ndipo inapoonekana hoja kwanza ya kufanya vitu vile. Kwanza kabla ya kutunga kuwapata wadau na kuwashirikisha juu ya sheria hizi, au si hivyo kupewa semina wananchi mbali mbali hapa ili kuelewa madhumuni ya mswada huu, ili kusikilizwa na wao watasema nini juu ya uzito au wepesi uliomo humu na kuwapa unafuu. Tusitegemee kwamba tunawatungia sheria za kuwakandamiza, tutegemee kwamba tunawatungia sheria ambazo zitawapa unafuu wa shughuli zao na kupata ustawi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, ndio hapa tunapokuja kulaumiwa na kuambiwa, aah! Mnapotunga sheria sisi hamtujali, mnakwenda kuchukua posho tu huko. Tunapondwa, tunatukanwa na tunafanyiwa kila aina ya balaa kwa sababu ya matokeo kama haya. Hii kusema kwamba mimi pamoja na wananchi wangu, kama vile mko pamoja. Utakuta hapa Mhe. Spika, mtu hajenda jimboni kwake mwaka mzima huu, halafu anasema mimi na wananchi wangu tunaunga mkono. Haya mnaunga mkono umewaona wapi? *(Vicheko/Makofi).*

Kwa hivyo Mhe. Spika, tunawafanyia dhulma, tunawafanyia dhambi na halafu tunawasemea. Mimi hili sikubaliani nalo. Mhe. Spika, ipo haja kwa Mhe. waziri kutoa semina kwanza, ili kuona kwamba wafanyabiashara wetu katika hili wanamchango gani, licha ya kwamba sasa hivi limeshachelewa lakini bado halijachelewa, kwa sababu kuna hatua za utekelezaji, ili kuona kwamba wanaweza wakatoa mchango gani juu ya mambo haya. Kwa sababu hizi sheria tunawatungia wao.

Mhe. Spika, baada ya hayo nasema nashukuru ahsante sana.

Mhe. Spika: Majadiliano yanaendelea. Nina jina moja tu la Mhe. Asha Moh'd Hilal lakini hayupo. Naogopa kumwita mjumbe nikaambiwa nimekamatia. *(Kicheko).*

Majadiliano yanaendelea. Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Hija Hassan Hija: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi niliogopa kunyanyuka nisijekuambiwa nimekamatiwa, lakini kwa sababu Mhe. Asha Moh'd hayupo, naomba nimkamatie kidogo.

Mhe. Spika, kabla kwanza ya kuendelea naunga mkono ule mchango wa Mhe. Ali Moh'd Bakar jirani yangu, kwa sababu mwenzangu amefanya utafiti pengine tangu jana, kwa hivyo mimi sina budi niunge mkono.

Baada ya hapo Mhe. Spika, niende kwenye mswada huu na nichangie mambo machache kidogo kulingana na wakati. Kwanza nianzie pale Mhe. Ali Moh'd Bakari alipozungumzia kwamba sasa wakati umefika serikali ione kwamba *ZRB* inapaswa kukusanya kodi zote ndani ya nchi hii. Kwa kweli kauli ya kuwakilishwa na *TRA* nadhani imepitwa na wakati. Sasa mamlaka ambayo inahusika nadhani ilione hili kwamba sasa Zanzibar miaka 40 ya Mapinduzi tumepevuka na tunaweza kufanya kila jambo. Madamu tumewaza kuungana na kutetea mafuta, basi na kodi za ndani zote tunaweza. Mhe. Spika, *ZRB* wana uwezo na wana wataalamu, kwa hivyo hatupaswi kushikiwa na *TRA*.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu mwengine ni kwamba, tumeambiwa humu kuwa sasa walipa kodi wote wanatakiwa watowe risiti ambazo zinatambulikana na serikali. Lakini kumekuwa na risiti ambazo ni za kisasa ambazo wafanyabiashara wengine wanatoa risiti za kisasa lakini ndani yake hamna *tin* namba. Sisi kama wajumbe wa *PAC* tumekuwa tukitizama risiti ambazo ni *electronic* risiti na hizi hazina *tin* namba. Sijui mswada huu umezingatia vipi suala hili ili kuweza kudhibiti mapato ya nchi. Vinginevyo itakuwa wafanyabiashara hasa makampuni wamekuwa wakizitumia risiti hizi za kisasa zaidi na ndani yake hamna *tin* namba na hii ni dalili ya kupotea mapato ya nchi.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. waziri hili alizingatia na pengine angetuambia tofauti ya risiti hizi na risiti za kisasa ambazo baadhi ya makampuni wanazitumia na zinaashiria upotevu wa mapato yetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa nilijuwe, Mhe. waziri anieleze ni kuwa mswada huu umezingatia vipi athari ambazo zinapatikana kutokana na kodi ambazo ni za Muungano? Kwa mfano hivi karibuni tumesikia meli moja kubwa ya uvuvi imekamatwa Tanzania Bara na uvuvi ni eneo la Muungano. Sasa sisi kama *ZRB* na kama Zanzibar je, tumefaidika vipi na mapato yale? Sasa ikiwa *ZRB* haijui pale tumepoteza nini au kuna mapato gani ya Wazanzibari wanaohitaji kuchangia pale, basi itakuwa hatuna maana ya kuweka sheria nyingi, wakati mapato yetu makubwa ya mambo kama yale yanaendelea kupotea siku hadi siku.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. waziri akija hapa anielimishe, athari ile ya ukamataji wa meli ile ya uvuvi je, mapato ya Zanzibar yamepotea vipi na mswada huu unahusianaje na kesi kama zile. Kwa sababu kesi ile ni moja, bila shaka kesi nyengine zitatokezea siku hadi siku.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nizungumzie kidogo suala zima la wafanyabiashara wetu na mlolongo wa kodi ambazo zinawakabili. Ni kweli wazanzibari ni wanyonge sana, ingawa ni watundu kwa biashara ndogo ndogo, lakini lazima serikali izingatie uwezo wa wafanyabiashara wetu, kwa sababu biashara ambazo wazanzibari wanazofanya ni kuuza mafungu ya tungule na mananasi kutoka Muyuni. Lakini mlolongo huu wa kodi ni mwingi. Sasa wazanzibari kuwawekea kodi nyingi na huku wakiandamwa na *TRA*, basi nadhani si kuwafanyia haki. Tathmini ni vyema ingefanywa, ili tuwaangalie uwezo wa wananchi wetu na mlolongo huu wa makodi ambayo sheria zitaendelea kuimarishwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningependa nilizungumze ni mgongano wa sheria kati ya *VAT* ya *TRA* na *VAT* ya *ZRB*. Naomba Mhe. Waziri aje anielimishe, mgongano huu kwa mswada huu utatatuka vipi. Kwa sababu kumekuwa na lalamiko kwamba *VAT* ile ya *TRA* na *VAT* ile ya *ZRB* inakuwa tofauti na kwa kweli wafanyabiashara wetu hawaridhiki nazo. Kwa hivyo, chini ya mswada huu ambao tunataka kuupitisha je, serikali imelizingatia vipi suala hili ili wazanzibari wetu wawe tayari.

Kwa mfano, hatuelewi vyema *VAT* inayolipwa na makampuni ya simu kama vile Zantel, Vodacom, Tigo na nyenginezo. Hapa tupo kwenye usimamizi wa *ZRB*, lakini kule Tanzania Bara kuna usimamizi wa *TRA*. Kwa hivyo, Mhe. Waziri aje atuelimishe mgongano huu wa kisheria chini ya *VAT* ya makampuni haya unakwenda vipi.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka Mhe. Waziri anipe ufafanuzi, toka kwenye kutetea mswada na pengine utapita wakati mfupi ujao. Lakini tumekuwa na kilio kwenye suala la (*JFC*) *Joint Financial Commercial* hili ni tatizo ambalo tumekuwa tukilalamika muda mrefu.

Mhe. Spika, kwa sasa tuna wajumbe kwenye (*JFC*), lakini kabla tulikuwa na wajumbe wengi. Tulikuwa na wajumbe mfano Mhe. Abdulrahman Mwinyi Jumbe na Mhe. Amina Zed Kheir, lakini hadi leo hatujaona mabadiliko yoyote. Sasa hivi tunao wajumbe wapya akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha. Zanzibar wanahitaji mapato na (*JFC*) bila shaka inasimamia fedha nyingi za Muungano. Sasa nadhani Mhe. Waziri atuelimishe mgongano huu na kwa upande wa Zanzibar sisi maslahi yetu ni yepi, chini ya sheria hii ambayo sisi Zanzibar tunakusudia kuipitisha.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu ni kwamba wajumbe wapo, tuna theluthi mbili ya wajumbe pengine, lakini hatuoni mabadiliko ya *JFC* na tunaendelea kuwa na masheria mengi hapa, lakini hatuoni faida yoyote ambayo wazanzibari

wanaipata. Mhe. Spika, namuomba Mhe. waziri kwa uwezo wake anielimishe ili wasi wasi wangu pengine na wananchi wengine wasi wasi uwaondoke.

Jengine Mhe. Spika, ambalo ningechangia kwa ufupi kabisa ni kwamba biashara Zanzibar kwa mtazamo wa kawaida bila shaka hata watafiti wanaunga mkono hilo, kwamba Zanzibar biashara imetoweka. Wazanzibari wengi sasa hivi Zanzibar nzima Unguja na Pemba wanakimbilia Bara hata kwa biashara ndogo ndogo za mitumba na viatu. Sasa wasi wasi wangu ni kwamba *ZRB* itajiimarisha kiutaalamu kwa mitambo na mambo mengine. Lakini bado mapato Zanzibar yatakuwa hayapatikani kama ambavyo tumelenga. Kwa sababu ni dhahiri kwamba *TRA* na Muungano kwa jumla wanadhamiria sisi tuwe watoto chini ya kodi, maana yake kodi zetu zote zimilikiwe na *TRA*.

Mhe. Spika, wazanzibari chini ya *ZRB* wataendelea kubuni njia za mapato, lakini bado mapato Zanzibar yataendelea kuwa hayapo na vinginevyo itakuwa mapato Zanzibar bado tunategemea. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba kwa kweli umefika wakati kwamba kodi zote ambazo ziko ndani ya Zanzibar, basi wazanzibari wenyewe chini ya *ZRB* wakusanye wenyewe na tuache kabisa kukusanyiwa. Mtu mzima jamani hawekewi rahani jambo lake ni aibu.

Mhe. Spika, mimi naishauri serikali kuanzia sasa ikatae kwamba mapato yote ambayo yanaihusu Zanzibar, sasa yakusanywe chini ya vijana wetu wa *ZRB* na mimi naamini kabisa uwezo wa kufanya hivyo wanao, kwa sababu wanaaminika na wataalamu wanao na mitambo wanayo. Kwa hivyo, hakuna haja kukusanyiwa. Mapato yale ambayo yanatokana na wafanyakazi wa Muungano, wafanyakazi wako Tumbe, wako Mwambe, wako Kengeja na wako Makunduchi, kwa hivyo mimi sioni sababu sasa kwa mapato yale kwenda *TRA*. Nadhani mapato yote sasa yaende *ZRB* ili tujuwe hasa kwa mwezi Zanzibar tunaingiza kiasi gani.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba siamini kabisa kwamba fedha ikusanywe na *TRA* baadae ipelekwe *ZRB* halafu uniambie hakuna upotevu, siamini kabisa. Wanaokusanya ni binadamu na kila mwanadamu anamatakwa yake na malengo yake. Kwa hivyo, tungeweza kudhibiti suala zima la upoteaji wa mapato kama mkusanyaji wa mapato ni mtu mmoja tu, lakini hatuwezi kuwa na watu watatu wanakusanya mapato halafu tukasema kwamba mapato yetu hayapotei. Mimi binafsi siamini na siamini kwa sababu tumeona upotevu wa mambo mengi na baadae tutakuja hapa kulaumiana.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningeligusia ni mabenki yetu haya. Mabenki mengine kwa kweli yanafanya kazi Zanzibari lakini nina wasi wasi kwamba taasisi nyengine za fedha hizi kodi zake zinakuwa hazipatikani ipasavyo. Kwa hivyo, serikali wajibu wake ni kufanya utafiti ili kuona kwamba mapato

yanayotokana na kodi za mabenki kwenye taasisi za fedha hizi zinaingia chini ya mapato ya Zanzibar na zitapatikana kwenye mfuko mkuu wa serikali.

Mhe. Spika, kusema kweli maandalizi yangu ni madogo na nilikuwa namshikia Mhe. Asha Moh'd, basi naomba nimalizie hapo na Mhe. Nyonje labda atanisaidia nashukuru sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria kama inavyojieleza kwenye gazeti hili.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea sheria hii yenye uangalifu mzuri na uliopitiwa na wana sheria kwa makini kabisa.

Mhe. Spika, pamoja na wenzangu wengi waliozungumzia kuhusu masuala ya usimamizi wa mapato yetu hapa Zanzibar kupitia *TRA* na *ZRB*. Mhe. Spika, na mimi nitakuwa mmoja ambaye tayari nitaelezea kiasi ambacho kama kile tunachokifahamu sisi wenyewe wazanzibari.

Mhe. Spika, kwa kweli wafanyabiashara hapa Zanzibar wana kilio sana. Wajumbe wengi wametoa mifano mingi, lakini usione ajabu Mhe. Spika, kila mjumbe akisimama akarudia baadhi ya sehemu ile ni moja katika kutaka kuchangia kutokana na ile hali ambayo tunakwenda nayo hapa Zanzibar, hali ya kiuchumi kwa kadri ya siku hadi siku kutuangukia.

Mhe. Spika, kwa kweli usimamizi huu wa kodi hasa tukipitia katika *ZRB*. Mhe. Spika, kuna mjumbe alisema kwamba hakuna haja ya kumpa *ZRB* wakala, kwa sababu bado anastahiki kupewa hizi sehemu za kusimamia kodi, kwa sababu huko nyuma ana historia nzuri, amekusanya vizuri sana kodi na tumeona sote humu wajumbe wako Mhe. Spika, vile viwango ambavyo anawekewa na anapitiliza. Kwa hivyo, tusiwe na mjadala mkubwa sisi tuwape tu *ZRB* kwa sababu wanastahiki kutokana na kazi zao nzuri.

Vile vile Mhe. Spika, kutokana na wasimamizi wetu wa mapato bado wako duni. Mhe. Spika, sasa hivi utawakuta, kwa mfano hawa wawekezaji wetu wa utalii hawa wa mahoteli utawakuta kila siku wanabadilisha majina ndani kwa ndani, wanajua kwamba hoteli ikiuzwa basi pale panatakiwa asilimia fulani iende serikalini. Sasa wao wanatufanyia ujanja, kwa hii namna ya kubadilisha majina ndani kwa ndani, wanakuambia eti *percentage* tuikose, tunapoteza kabisa mheshimiwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. waziri hebu aliangalie hili suala na alione kwa makini kabisa, hawa wanatufanyia ujanja. Kila siku kule Kiwengwa hoteli zinabadilika tu, utasikia leo *Going*, wakati ile *Going* ilikuwa

Bravo na Bravo hiyo unaambiwa imeondoka imekwenda sehemu ya hoteli ya *Sea Club, Sea Club* ile sasa inakuwa *Bravo.*

Mhe. Spika, kwa kweli hawa watu hebu tuwaangalie kwa makini kabisa. Mhe. Spika, wanafanya ujanja huu ili kutupotezea mapato yetu tusiyapate kwa njia ya uhalali kabisa ambayo ni kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, mimi nina mfano mmoja wa mfanyabiashara alikuwa ana kontena lake kule Dar es Salaam, sasa hapa kidogo mimi ilinipa kujiuliza, kuwa hii sheria ya *ZRB* ya Zanzibar na *TRA* ya kule Dar es Salaam, sasa najiuliza inatofauti gani. Kwa sababu yule mfanyabiashara kontena lake lilishuka kule Dar es Salaam, baada ya kushuka kule akalipa ile asilimia ambayo sio kubwa sana ambayo kama angeshukia kwa Zanzibar basi ingemgharibu pesa nyingi sana.

Vile vile alikuja na kontena jengine la mambo ya matairi haya, kwa kweli mfanyabiashara huyu alitaabika sana. Maana yake zile kontena zilikuwa zinapita tu zinakuja zake Zanzibar. Kwa hivyo, akaambiwa sisi hapa sheria zetu hii mipira iliyotumika hapa kwetu ni gharamu kabisa hapa na tunaichoma moto sisi. Yule mfanyabiashara akamuambia hapana hii inakwenda zake Zanzibar. Akasema hataa, hii ndio *TRA* moja. Akamwambia sisi Zanzibar haya mambo ya mipira iliyotumika sisi hatuna sheria hiyo. Kwa hivyo, walimzungusha kwa kiasi kikubwa sana na hili suala niliwahi kulizungumza, hebu tuangalie jinsi mfanyabiashara huyu alivyohangaishwa. Imefika pahala sasa lile kontena limeingia pale na likatozwa pesa chungu nzima. Tunaomba hili suala wale ndugu zetu wa kule bara hebu wakae hasa na waangalie hizi sheria zikoje viwango vyake kati ya Zanzibar na kule Dar es Salaam zikoje.

Mhe. Spika, waheshimiwa wajumbe wengi waliopita wamesema, wafanyabiashara wameshakimbia wengi hawapo. Ni kweli Mhe. Spika, hili tulikubali na tunasisitiza sana. Ndio maana nikasema Mhe. Spika, usione ajabu ukiona mjumbe anaendelea kulizungumzia suala hilo moja ambalo limeshazungumzwa, kwa sababu analisema kwa uchungu.

Mhe. Spika, ukiangalia wenzetu wa nchi nyengine. Kwa mfano nchi kama Comoro na kwengineko basi wanaendelea kwa hizi biashara hawa wadogo wadogo tu na wanainuka vizuri, lakini sisi hata wale wafanyabiashara wadogo wadogo sasa wamekufa kabisa. Hii inakuja baada ya kuwauwa wale sasa tunaleta na wazungu waje kufanya biashara za kuuza tungule hapa. Kwa hivyo, mheshimiwa ndio tunajimaliza kabisa. Wakati biashara zile zimeshamalizwa katika upande mwengine tunaletwa sasa kwa hawa wawekezaji wageni, utawakuta wanafanya biashara za kupaka hina, na wao wanapaka hina mheshimiwa. Hebu tuangalie haya mapato kweli tumekusudia huyu

mfanyabiashara mdogo wa Zanzibar kumuondolea umaskini, ndio tunammaliza kwenye umaskini Mhe. Spika.

Kwa hivyo, hii hali Mhe. Spika, inasikitisha. Ndio maana leo dada yangu pale aliondoka na alieleza kwa ufasaha kabisa na alieleza kutokana na uchungu wa ile hali halisi ilivyo. Miongoni mwa waheshimiwa wajumbe humu watakuwa wanauzoefu ule wa biashara kutokana na hali ilivyo.

Mhe. Spika, kama hili suala la *BoT*. Mhe. Spika, namuomba Mhe. waziri atufahamishe hasa hii haki yetu iko wapi kwenye *BoT* kwa hapa Zanzibar, maana yake naona kila siku kukicha tunakandamizwa tu, hatufahamu zile haki zetu. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja utuambie haki zetu Zanzibar ni zipi kutokana na kutumia benki ya *BoT*, hebu tueleze ili wazanzibari wafahamu kwa kina. Ikiwa tunabana bana basi ndio maana tunafika pahala wananchi wetu wanatuambia kuwa huku tunakuja kupiga kofi, kama ilivyooneshwa mfano pale kuwa tunapiga kofi tu pa pa pa.

Mhe. Spika, nikiendelea kuzungumza tuangalie na hivi viwango vya kodi. Hebu tujaribu kupunguza kidogo ili hawa ndugu zetu wafanyabiashara warudi. Hebu tusimame Mhe. Spika, na tusema sasa njooni na wale waliokuwa wakishusha makontena waweze kurudi hapa kama ilivyokuwa huko nyuma. Mhe. Spika, kwa kweli sitaki nirudie, lakini ilikuwa mpaka yule mfungaji alikuwa anapata riziki yake, mbeba rikwama alikuwa akipata riziki yake, wenye mahoteli na wao walikuwa wakipata riziki zao. Baada ya kuifanya hii minimum na maximum sasa ndio imetuharibia sana hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. waziri hebu tuiangalie hii hali halisi ilivyo, hebu tupunguzeni, tuwapunguzie kidogo ushuru mheshimiwa na tujiamini. Hali inabadilika. Tukisema leo mafuta tuyasubiri ni ya leo hayo, si ya leo hayo wala sio kitu cha mchezo, tunayataka sasa hivi yaje mafuta ili tuondoshe huu umaskini, lakini mheshimiwa si ya leo haya yanataka maandalizi.

Mhe. Waziri juzi hapa katuambia ndio kwanza anataka kutupa semina, hajaandaa wataalamu kupeleka nje. Mhe. Spika, hii hali ya kusema kuwa mafuta tunayo, mafuta tunayo kweli. Lakini sasa bado hali Mhe. Spika, haijafikia ya kusema kuwa tayari sasa hivi tunachimba, isipokuwa mambo yanaandaliwa yako chunguni na tutachimba mafuta na Zanzibar tutaondoka umaskini.

Mhe. Spika, kwa kuwa tunasubiri mafuta, tuko katika mpango wa mafuta tunasubiri basi na hili suala Mhe. waziri ulione ili ushuru upunguke na wafanyabiashara wetu wapate kurudi Zanzibar na waweze kufanya biashara na tuendelee na shughuli zetu na umaskini uondoke.

Mhe. Spika, nimejitahidi kiasi cha kujitahidi. Mhe. Spika, kusema unawashirikisha wananchi, yaani kusema na wananchi wangu na wao, basi ni lazima kwa sababu ni kiongozi wao nimesimama nimesema na wao ndio walionileta hapa. Kwa hivyo, nasema naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope, kwa kuwa wamejua kiongozi wao na yeye kasimama, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nawashukuru waheshimiwa wajumbe nyote, nafikiri jioni tufanye majumuisho kwenye mswada huu. Maana wachangiaji wote ambao wameomba wamemalizika. Kwa maana hiyo basi naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 za mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kufanya majumuisho ya Mswada wetu wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na Mambo Yanayohusiana nayo.

Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuendeleza mjadala ambao niseme kwa kweli ulikuwa mzuri na wenye manufaa kwetu sote. Kwa sababu mbali ya kama sisi Wizara, lakini kinchi kama Waheshimiwa Wajumbe wengi walivyozungumza masuala ya kodi ndio mambo ya msingi ambao mtazamo wetu sasa, kama mapato au kitu kinachochangia mapato makubwa katika uendeshaji wa Serikali yetu.

Lazima nikiri kwamba ni kweli kwa bahati mbaya Miswada ya mara hii imechelewa kuwafika Waheshimiwa Wajumbe. Kwa sababu kwenye *Cabinet* tulimaliza kwa wakati isipokuwa yalitokezea matatizo katika *drafting* ya Miswada ile kwenye Afisi ya Mwanasheria Mkuu mpaka Afisi ya Uchapaji, yaani ule mtiririko uliofuata baadaye ndio ulichelewa kidogo.

Mhe. Spika, hili kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza tunaomba radhi sana na tutajitahidi siku za usoni hili lisitokee. Lakini zaidi Mhe. Spika, kwamba Miswada yenyewe ya safari hii nadhani mtaiona ni Miswada mikubwa ambayo ni migumu na lazima tukiri. Kwa sababu baadae atakuja mwenzangu Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Mswada wake wa Madawa ya Kulevya nafikiri walikaa siku tatu. Sisi unakuja Mswada mwengine wa fedha

chafu nao tulikataa siku tatu. Sasa mbali ya ukubwa lakini na ugumu wenyewe wa ule Mswada.

Lakini Mhe. Spika, lazima nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Kamati ya Fedha ya Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin na wajumbe wake wote wa kamati. Kwa kweli kwa upande wetu wamefanya kazi nzuri sana kuupitia Mswada ule na kusahihisha makosa yote. Hata utaona katika karatasi alizosambaza Mhe. Salmin za marekebisho utakuta mengi ni madogo madogo. Hii inaonesha wazi kwamba haikuripuliwa, imefanyiwa kazi watu wamekaa wakaona aaa! Haidhuru umechelewa lakini tuifanyie kazi inayopaswa ili tutoe kitu kinachofaa.

Kwa hiyo kama nilivyosema Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali hili tunaomba radhi lakini pia tunatoa pongezi za dhati kabisa kwa Wajumbe wa Kamati lakini hata kwa Wajumbe wako Mhe. Spika. Mhe. Zahra Ali Hamad alisema kwamba umekuja siku tatu tu, mimi namsifu sana siku tatu lakini kauchambua utafikiri labda kapata siku 33. Si yeye tu, hata Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Mwenyekiti mwenyewe.

Kwa kweli wote wamepata wasaa wameuchambua na hili ndio ninalotaka kwamba tupate *constructive criticism*, mtukosoe, mtuelekeze, halafu yale ya maana yote na ninaamini mengi ni ya maana yatatusaidia kuufanya Mswada wetu uwe bora zaidi na hatimaye kuweza kupitisha sheria hii.

Mhe. Spika, kwa jumla Waheshimiwa 15 walipata wasaa wa kuchangia mswada huu ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi

2. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Kny: Mhe. Said Ali Mbarouk, Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi
3. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
4. Mhe. Rashid Seif Suleiman
5. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
6. Mhe. Ali Denge Makame
7. Mhe. Ali Abdalla Ali
8. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
9. Mhe. Haji Mkema Haji
10. Mhe. Ali Suleiman Ali
11. Mhe. Assaa Othman Hamad
12 Mhe. Zahra Ali Hamad

13. Mhe. Ali Moh'd Bakari
14 .Mhe. Hija Hassan Hija
15 .Mhe. Makame Mshimba Mbarouk *(Makofi)*.

Kwa kweli wote tunawashukuru sana kwa michango yao, naamini Mhe. Spika kwamba wengine baada ya *Weekend* hii kuupata Mswada huu na kuukalia vizuri, basi wangependa kuitumia fursa ya kuchangia, lakini muda haukuwa kwenye upande wao.

Mhe. Spika, hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu zimegawika katika maeneo 17 kama ifuatavyo:-

1. Suala zima la ushirikishwaji wa wadau katika maandalizi ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

2. Suala la elimu kwa walipakodi na utoaji wa risiti.

3. Uwezo wa Kamishna katika sheria hii, yaani Waheshimiwa wengi wameonesha wasi wasi kwamba Kamishna amepewa madaraka makubwa, hata wengine wamesema kuwa yeye atakapokosea ataadhibiwa vipi ?

4. Kuhusu suala zima la usajili, vigezo vyake pamoja na kufuta usajili.

5. Makosa na adhabu zake.

6. Haki za mlipakodi.
7. Kuna suala hili mara nyingi huwa linajirudia kuhusu kuwepo mamlaka mbili za kodi.
8. Kutozwa kwa *VAT* kwa biashara ya mkopo.

9. Marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*).

10. Waheshimiwa walizungumzia mapitio ya mara kwa mara ya sheria za kodi, yaani kuwepo na haja hiyo.

11. Kuthaminiwa kwa walipakodi wanaolipa kodi kwa wakati.

12. Maana ya baadhi ya maneno yaliyotumika.

13. Kugongana kwa Sheri ya Usimamizi wa Kodi na sheria Nyengine.

14. Mawasiliano kati ya *ZRB* na taasisi nyengine.

15. Kodi ya *Income Tax* kwa wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar.

16. Ukaguzi wa mara kwa mara kwa wafanyabiashara, na

17. Kufidiwa kwa wafanyabiashara, yaani walipakodi wazuri waliofilisika.

Mhe. Spika, huu ni mtiririko mkubwa na kama nilivyosema nikianza kutafakari kila moja point hizi 17 basi pengine jioni nzima hii nitaichukua. Lakini nifanye kama *shopping list* ya mambo yote.

Kwa kweli tukiangalia Waheshimiwa wengi walichangia suala zima la biashara, yaani kutaka kujua hii biashra iliyozungumzwa hapa mbona kidogo *definition* yake tofauti.

Pili suala kubwa Waheshimiwa wengi walizungumzia kuhusu Kamishna, yeye kama nilivyosema madaraka mengi tena makubwa.

Tatu ni kuhusu suala la usajili kwenye kifungu 5 pamoja na kusajiliwa kifungu cha 11. Mhe. Spika, haya mambo yamekwenda na yakijirudia sana kwa Waheshimiwa wengi ambao wamepata fursa ya kuchangia.

Vile vile suala jengine ambalo limejitokeza kwa Waheshimiwa wengi ni kuhusu adhabu kuonekana ni nyingi tena ni kali. kwa hivyo, walitushauri kwamba tuchukue hadhari kidogo hapa kwetu hatujafikia huko.
Mhe. Spika, ninachotaka kusisitiza ni kwamba nilieleza wakati nilipokuwa nikiwasilisha Mswada huu, naomba nisisitize tena kuwa Mswada huu wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Kodi haukusudii kuanzisha vifungu vipya kabisa vya sheria. Kwa sababu vifungu vilivyomo kwenye Mswada huu tayari vipo, isipokuwa vimetawanyika kwenye sheria mbali mbali zilizopo za kodi na wakati mwengine vinatafautiana.

Lengo la Mswada huu ni kuviweka pamoja vifungu vyote vya sheria zilizopo na kuweka utaratibu mmoja tu kwa mambo yanayofanana katika usimamizi wa Sheria zote za Kodi zinazosimamiwa na *ZRB*.

Aidha Mhe. Spika, Mswada huu madhumuni yake ni kuwapunguzia usumbufu walipakodi, kuimarisha usimamizi bora wa sheria za kodi, kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa watendaji pamoja na kuimarisha mapato ya Serikali.

Kwa hivyo, tunapozungumza kwamba kuna kodi au adhabu kali, kwa kweli hapa hakuna kipya, isipokuwa sisi tumeziweka na tukaziainisha, yaani tumeziweka kwa mtiririko tu, hizi zote zimo kwenye sheri zile tulizozitaja. Mhe. Spika, naomba nizikariri tena kwa mara nyengine nadhani tulizitaja wakati ule kama hivi ifuatavyo:-

1. Sheria ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998.
2. Sheria ya Kodi ya Ushuru wa Stamp Nam. 6 ya mwaka 1996.
3. Sheria ya Kodi za Hoteli Nam. 1 ya mwaka 1995.
4. Sheria ya Kodi za Huduma za Bandari Nam. 2 ya mwaka 1999.
5. Sheria ya Kodi za Mafuta Nam. 5 ya mwaka 2001.

Mhe. Spika, msingi wote ni sheria hizi na tungependa tuzitoe *photocopies* sheria zote zile kwa ajili ya kuwagawia Waheshimiwa, lakini nayo tukaangalia masuala ya bajeti. Lakini tulijitahidi kwenye semina nadhani kwenye mkopa ule kila mmoja wetu walipata uchambuzi mzuri kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza kwa sheria zile, nini kipo na kipi kinachorekebishwa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe ningewaombeni sana kwenye makabrasha yetu yale turejee tena na tupitie na tutaona hasa ule mtiririko wenyewe na nini kilichokusudiwa. Kwa kweli sio mambo magumu kama yanavyoonekana, isipokuwa ni suala la mtiririko tu.

Mhe. Spika, kwenye maelezo yangu nitajitahidi kuzipitia hoja zote za Waheshimiwa Wajumbe kwa kuzingatia maeneo hayo niliyoyataja. Kwa hivyo, pale ambapo itajitokeza hoja ya Mhe. Mjumbe haikujitokeza wazi wazi, basi isichukuliwe kama nimeliwacha au nimelidharau labda itakuwa ni suala la muda tu. Lakini nitajitahidi kuyazungumza kadri ya muda nilionao.

Kuna hoja ya wadau mbali mbali hawakushirikishwa katika hatua za awali za matayarisho ya Mswada huu. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Rashid Seif Suleiman pamoja na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba Mswada huu wa sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Kodi kama nilivyosema haukusudii kuanzisha vifungu vipya vya sheria, bali ni kuweka utaratibu wa aina moja katika usimamizi wa sheria zote za kodi zinazosimamiwa na *ZRB*. Vifungu hivi vya sheria tayari vimeshapitishwa na Baraza lako tukufu katika vikao vilivyopita chini ya sheria tofauti.

Serikali imechukua hatua maalum za kushirikiana na Sekta Binafsi katika maendeleo ya nchi yetu. Mfano mzuri ni kuanzishwa na kuanza kufanyakazi kwa Baraza la Biashara la Taifa, linaloshirikisha wadau kutoka Serikalini

pamoja na sekta binafsi chini ya Uwenyekiti wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduuzi, yaani *Zanzibar Business Council*.

Mhe. Spika, kwanza tulikaa Nungwi kule Lagema, tulifanya mkutano mzuri tu na baadaye tulifanya mwengine baada ya mwezi mmoja tu katika hoteli ya Bwawani. Kwa kweli wafanyabiashara walipata kubadilishana mawazo na Serikali . Kwa upande wetu Mhe. Rais wa Zanzibar ndiye aliyeongoza, yaani walikuwa wakihoja kila swali walilokuwa nalo, mpaka tulifika pahala kama kuna mabishano kati ya Serikali na wafanyabiashara.

Lakini kwa lengo la kutafuta ufanisi kwa yale mambo ambayo walihitaji ufafanuzi wayapate. Kwa hivyo, mikutano ile miwili ilifanikiwa sana Mhe. Spika. Nadhani huo ndio naweza kusema ushirikishwaji mkubwa na vikao vile vitakuwa vikiendelea na wala sio mwisho *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara ya Fedha na Uchumi inao utaratibu wa kuwashirikisha wadau kwenye mambo mbali mbali. Kwa mfano, kuwepo wajumbe wa Sekta Binafsi kama vile *ZAT* na *Zanzibar Chamber of Commerce, Industry and Agriculture* pamoja na taasisi nyengine kutoka Sekta Binafsi katika Kamati Maalum ya Kuzingatia Mageuzi katika Mfumo wa Kodi, yaani *Tax Reform Taskforce*.

Kwa maana hiyo, hawa wajumbe tunawaalika na tunakuwa nao kwa ajili ya kuzungumza nao pamoja na kubadilishana mawazo mpaka tunafikia pahala tunapopataka.

Mhe. Spika, kamati hii imetoa mapendekezo kadhaa ya kuimarisha mfumo wa kodi moja wapo likiwa ni haja ya kurahisisha usimamizi wa kodi. Mswada huu ni hatua muhimu ya utekelezaji wa mapendekezo hayo *(Makofi)*.

Vile vile kuna hoja nyengine ambayo imetolewa na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, kwamba mfumo uliotumika katika uandishi wa sheria na kuweka adhabu kwenye kila kifungu unaifanya sheria iwe ngumu kufahamika.

Mhe. Spika, lengo la sheria hii ni kuondosha usumbufu uliopo kwenye sheria mbali mbali za awali. Usumbufu uliokuwepo hapo awali ni kuweka adhabu mbali na kifungu husika jambo ambalo hupelekea kusahauliwa kwa baadhi ya makosa.

Sheria hii ya Usimamizi wa Kodi imeweka adhabu katika kila kifungu kwa lengo la kurahisisha mapitio kwa walipakodi pamoja na watendaji wa *ZRB*. Kwa kuzingatia kuwa adhabu zinatafautiana kutegemea na uzito wa kosa

lenyewe. Aidha katika utungaji wa sheria hakuna athari yoyote kwa kuweka sehemu maalum ya adhabu au kuweka adhabu kwenye kila kifungu husika.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na suala ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi walilichangia kuhusu kupewa kwa madaraka makubwa kwa Kamishna wa Bodi ya Mapato ya Zanzibar chini ya Kifungu cha 11 katika usajili, kufuta usajili pamoja na kuamua kumsajili.

Kwa hivyo, kwanza hicho kifungu cha madaraka makubwa vile vile kwenye kifungu cha 11 katika usajili, kufuta usajili pamoja na kuamua kumsajili kwa aina gani ya kodi. Kwa kweli hapa Waheshimiwa wengi walidhani kwamba huyu Kamishna amepewa madaraka makubwa kwenye kazi hizi.

Mhe. Spika, hoja hii imezungumzwa na Mhe. Zahra Ali Hamad, Mhe. Assaa Othman Hamad, Mhe. Ali Moh'd Bakari, Mhe. Ali Suleiman Ali pamoja na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji.

Ukweli ni kwamba lengo la kifungu cha 11 (1) na (2) ni kuweka taratibu na kumuwezesha Kamishna kuigomboa kodi ambayo haikulipwa kutokana na sababu ya kutokujisajili kwa mfanyabiashara kwa njia moja au nyengine, ambapo mfanyabiashara huyo alifanyabiashara na kukusanya kodi na kushindwa kuiwasilisha Serikalini.

Kwa hivyo, hatuzungumzii Moh'd Hashim au Ali Bakari, Seif wala Mwinyihaji. Aaa! Hii ni taasisi na wala hatokwenda Kamishna kwa ajili ya kumpekuwa mtu na hilo silo lengo lake. Isipokuwa lengo ni kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali hayaathiriwi na udanganyifu wa wafanyabiashara ikiwemo kutojisajili kwa wakati. Mhe. Spika, hayo yaliyozungumzwa baada ya yule mfanyabiashara mwenyewe kwenda kinyume na yale maagizo ya ulipaji wa kodi.

Kwa maana hiyo, ili kupata mantiki ya kifungu husika, Mhe. Spika nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wavisome vifungu hivyo nilivyovitaja vya 11 (1) na (2) kwa pamoja, yaani kifungu chote ukisome ndio utaupata ule mtiririko wenyewe, badala ya kuchukua senteni moja moja.

Aidha Mhe. Spika, vigezo vyote vya usajili vimetajwa kwenye kanuni za sheria husika ambavyo Kamishna wa *ZRB* anavitumia kusajili mfanyabiashara kwa ajili ya kulipa kodi. Kwa mfano, Kanuni iliyotungwa chini ya Sheria ya *VAT* inaelezea kiwango cha mauzo ya shilingi 15,000,000/- kwa mwaka kuwa ni miongoni mwa vigezo vya mfanyabiashara kusajiliwa *VAT*.

Kwa hivyo, indhari ya Waheshimiwa Wawakilishi itaendelea kuzingatiwa katika uandaajiwa kanuni chini ya sheria hii. Hivyo, maoni yenu tumeyasikia na wakati tutakapoandaa kanuni tutayazingatia maoni yenu.

Mhe. Spika, kwa ujumla madaraka yaliyotolewa kwa Kamishna ni ya afisi kama nilivyosema na wala sio ya mtu binafsi na yanahusisha pia maafisa wa *ZRB* waliokasimiwa madaraka. Kwa kweli madaraka haya ni muhimu kwa kuepusha ukwepaji pamoja na uepukaji wa kodi, haya ndiyo yanayotusumbua sana.

Kwa sababu kwenye kodi wenyewe wanazo *terminology* mbili hizo za *avoidance* na *invasion*. *Avoidance* mtu anakwepa kodi ule ujanja wa kukwepa kodi na *invasion* anavunja sheria hasa, yaani yeye anajua sheria hii lakini halipi tu. Lengo hasa za kuweka taratibu au adhabu hizi kwa huyo atakayekwenda kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, walipakodi hawathamini suala hili nalo limejitokeza na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Mhe. Rashid Seif Suleiman pamoja na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja walizungumzia suala hili.

Ukweli ni kwamba Serikali inatambua umuhimu wa sekta binafsi katika ukuwaji pamoja na uzalishaji kwa uchumi wa nchi kama nilivyosema hapo awali. Vile vile Serikali inafahamu umuhimu wa walipakodi katika kufanikisha utekelezaji wa mipango mbali mbali hususan ya kuimarisha huduma kwa jamii na miundombinu.

Umuhimu huu umeelezwa bayana katika mipango ya nchi ukiwemo MKUZA. Kutokana na kutambua huko umuhimu wa walipakodi ndio maana Serikali inawashirikisha kwenye michakato tofauti ya maendeleo pamoja na mustakbali wa nchi ikiwemo utayarishaji wa mapitio ya mipango ya maendeleo. Bajeti ya Serikali, Miswada mbali mbali ya mabadiliko ya sheria za kodi pamoja na zile zinazohusiana na biashara.

Aidha Serikali pia imetoa vyeti kwa walipakodi bora wanaofuata sheria na taratibu kwa kutambua mchango wao. Kwa kweli kila mwaka *TRA* Zanzibar na *ZRB* wanafanya tafrija ndogo ya kuwazawadia wale walipakodi wakubwa na hata wadogo, lakini wale wanaofuata taratibu tena wanaolipa kwa wakati. Mhe. Spika, nakumbuka mimi mwenyewe nimeshaalikwa mara mbili mpaka tatu kwenye sherehe kama hizo.

Kwa hivyo, hali hii inaonesha wazi kwamba kweli tunawathamini, tuko pamoja nao pia tunawashukuru sana wao kwa kutambua mchango wao katika maendeleo ya taifa hili.

Mhe. Spika, mfanyabiashara kutakiwa kusajiliwa kwa kila biashara ni tatizo kwa kuzingatia hali ya wafanyabiashara wa Zanzibar. Nadhani hoja hii Waheshimiwa wengi sana wameizungumzia hasa kwenye sehemu ya pili ya kusajili na kufuta usajili kifungu cha 5 (1), (2) na (3). Lakini hasa cha kifungu cha 5 (1) au (2) kwamba mtu anakusudia kufanyabiashara zaidi ya moja, basi atalazimika kusajiliwa kwa kila biashara.

Mhe. Spika, hoja hii imezungumzwa na Waheshimiwa wengi kama nilivyosema Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Haji Mkema Haji, Mhe. Ali Suleiman Ali pamoja na Mhe. Zahra Ali Hamad.

Ukweli ni kwamba wanaomba Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kuwa watafautishe baina ya biashara na bidhaa. Sheria inataka mfanyabiashara ajisajili kwa kila biashara na sio kila bidhaa anayouza na wala hatukusudii kama alivyosema Mhe. Zahra Ali Hamad kwamba vipodozi, lakini biashara anayoifanya ile ndio akate leseni kwa ajili ya kusajiliwa na hiyo mantiki tunayoikusudia.

Mswada huu umefafanua maana ya biashara chini ya kifungu cha pili. Kweli nakumbuka Waheshimiwa wengi waliuliza, napande kuisoma kwa Lugha ya Kiswahili maana ya biashara, maana yake ni aina yoyote ya biashara au shughuli ya kibiashara. Mhe. Spika, nadhani kidogo haileti mtiririko mzuri.

Vile vile nakumbuka kwamba tunayo *definition* kwa Lugha ya Kiingereza, nadhani ile imeweka wazi kabisa, baadaye tutakaa pamoja na wataalam wa Lugha ya Kiswahili, kwa ajili ya kupata ile maana hasa ya kiswahili. Lakini kwa Lugha ya Kiingereza inasema *business includes any form or trade or commercial activity*, sasa hii inaweka kwa ufasaha kabisa na wala hakuna sehemu iliyorudiwa biashara. Kwa hivyo, kama nilivyosema kwamba baadaye tutakaa pamoja, ili tuone vipi tunaweza kuipata tafsiri nzuri.

Mhe. Spika, kwa mfano mfanyabiashara wa hoteli na wakati huo huo anafanya biashara ya reja reja ya bidhaa nyengine kama vile nguo, basi mfanyabiashara huyo huwajibika kusajiliwa tofauti kwa kuwa biashara zake ni tofauti. Mfanyabiashara hahitaji kujisajili tofauti ikiwa biashara yake inahusisha bidhaa tofauti kama vile mabegi, nguo nakadhalika kama nilivyosema pamoja na mifano iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Aidha ili kurahisisha kuwa Serikali inazo taarifa zote za wafanyabiashara husika, sheria inamtaka ajisajili kwa kila eneo iwapo anafanyabiashara kwenye maeneo tofauti hata kama ni ya aina ile ile. Kwa mfano biashara ya ujenzi,

usajili huu ni mara moja tu na wala hautarajiwi kuleta usumbufu kwa wafanyabiashara waaminifu.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza lengo ni kuzuia udanganyifu wowote unaoweza kujitokeza kwa wafanyabiashara wasio waaminifu, ambao pia wanataka kukwepa kodi kwa upande wa leseni za biashara.

Kuwepo kwa mamlaka mbili za kodi ni usumbufu kwa walipakodi nalo pia lilizungumzwa na Waheshimiwa wengi wakiwemo Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji. Mhe. Spika, ukweli ni kwamba suala hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara kwenye vikao vyetu, ingawa kodi hizi ni tofauti na muda na utaratibu wake wa malipo hauhusiani.

Serikali tayari imelichukua suala hili na inalifanyiakazi kwa kuangalia uwezekano wa kuziweka chini ya taasisi moja. Taarifa rasmi itawasilishwa Serikalini mara baada ya kukamilika kwa kazi hiyo. Mhe. Spika, nakumbuka kwenye kikao chetu cha bajeti suala hili Waheshimiwa Wajumbe walitushauri pamoja na kutuagiza Wizara ya Fedha na Uchumi tukalifanyie kazi na tunalifanyia kazi.

Kwa maana hiyo, wakati huu *TRA* na *ZRB* zinafanyakazi kwa mashirikiano katika maeneo mbali mbali yakiwemo ya ukaguzi wa walipakodi, utafiti, mafunzo, elimu kwa walipakodi pamoja na kubadilishana taarifa zinazosaidia ukusanyaji wa mapato. Mashirikiano haya yanatokana na makubaliano yaliyofikiwa baina yao. Mhe. Spika, hoja hii pia ilichangiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Ali Moh'd Bakari.

Mhe. Spika, kuna hoja nyengine nyengine kwamba sheria za kodi ziwe zinafanyiwa mapitio mara kwa mara wakiangaliwa viwango vya kodi ikiwemo suala la kutozwa kwa *VAT* kwa biashara ya mkopo. Hili lilichangiwa na Mhe. Zahra Ali Hamad, Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba serikali imekuwa ikifanya marekebisho ya sheria mara kwa mara pale inapokuwa kuna haja ya kufanya hivyo. Itakumbukwa kwamba miswada ya marekebisho ya sheria imekuwa ikiwasilishwa mara kwa mara katika Baraza lako tukufu kwa lengo kwenda sambamba na hali ya uchumi, kuongeza ufanisi kwa usimamizi wa kodi na kuziba mianya ya upotevu wa kodi. Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la thamani Nam. 4 ya mwaka 1998 kodi huwajibika kulipwa inapotokea mambo yafuatayo.

a) Mzigo unapotolewa na kukabidhiwa mwenye mali.
b) Huduma inapotolewa
c) Malipo yanapopokelewa.

Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha kwamba mapato ya serikali yanapatikana kwa wakati. Wakati wafanyabiashara wana uhuru wa kukopeshana, mapato ya serikali hayakopeshwi chini ya utaratibu huo. Utaratibu huu unahakikisha kutimizwa kwa vigezo vyengine muhimu vya utozaji kodi kama vile *fairness*.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala zima liliulizwa kwamba serikali haifanyi marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kama inavyotakiwa na sheria. Hili Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji alizungumza suala hili. Mhe. Spika, ni kwamba kuna njia tofauti za kushughulikia madai ya kodi inayolipwa na muhusika. Utaratibu unaotumika Zanzibar ni kumruhusu mlipaji kujipunguzia kodi hiyo, kinachotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998 ni mfanyabiashara husika kukaguliwa ili kuthibitisha uhalali wa madai yake. *ZRB* imekuwa ikiruhusu wafanyabiashara wanaothibitisha uhalali wa madai yao kujipunguzia kodi wanaolipa kwa utaratibu maalum utakaowekwa.

Mhe. Spika, suala jengine muhimu ambalo waheshimiwa wengi wamelizungumza akiwemo Mhe. Khamis Jabir Makame, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Mzee Ali Ussi, Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Haji Mkema Haji, Mhe. Ali Suleiman Ali ni kuhusu suala la elimu kwa walipa kodi na utoaji wa risiti uimarishwe.

Mhe. Spika, sisi upande wa wizara tunakubaliana na *observation* za Waheshimiwa Wajumbe kuwa elimu kwa walipa kodi lazima itolewe na ni muhimu sana katika kuimarisha uajibikaji wa hiari. Pia kupunguza urasimu na kukusanya mapato ya serikali kwa wakati, nakubaliana nalo hilo na tutajitahidi kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuona kwamba hili tunalifanikisha kupitia vyombo vyetu vya habari. Kutokana na utambuzi huo ambapo elimu hiyo imekuwa ikitolewa kila mara kupitia vyombo vya habari kama nilivyosema na tutazidi kuimarisha. Pia semina na warsha juu ya masuala mbali mbali yanayohusiana na kodi ikiwemo sheria inavyofanyiwa marekebisho. Mhe. Spika, hata hivyo maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu juu ya kuongeza utoaji wa elimu zaidi kwa jamii juu ya umuhimu wa kodi yatazingatiwa na kutekelezwa.

Mhe. Spika, kuhusu adhabu ikiwemo riba ni kubwa na makosa yaliyoanishwa. Hili Mhe. Ali Abdalla Ali alizungumza, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Mzee Ali Ussi na Mhe. Zahra Ali Hamad wote walizungumza jambo hili.

Ukweli ni kwamba mfanyabiashara ni wakala wa serikali katika kukusanya mapato kutoka kwa wananchi, hivyo huajibika kuwasilisha kodi hiyo aliyoikusanya sehemu husika kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizokuwepo. Mhe. Spika, kuwepo kwa adhabu hizo huondoa kivutio kwa wafanyabiashara kuitumia kodi waliyoikusanya kutoka kwa wananchi badala ya kuiwasilisha serikalini kunakohusika tena kwa wakati.

Mhe. Spika, juu ya riba kuwa itozwe kwa kiwango cha Benki Kuu baada ya kufuata viwango vya benki za biashara. Mhe. Spika, lengo la riba hii ni kuondoa kivutio kwa mfanyabiashara kutumia fedha za kodi, iwapo kiwango cha adhabu ni chini na faida anayoweza kuipata akiwekeza fedha hizo benki, kuna kivutio kwake kuzitumia badala ya kuziwasilisha serikalini. Kwa hivyo, kiwango cha riba kinapofuata kiwango kilichopo kwenye Benki za Biashara kunaondoa fursa hiyo.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine adhabu iliyoainisha katika kifungu cha 27 cha sheria hii inamuhusu mtu anayejifanya kuwa Afisa wa *ZRB* wakati si muajiriwa wa *ZRB*. Lengo la adhabu hiyo ni kuzuia utapeli unaoweza kufanywa na watu kujitambulisha kama wafanyakazi wa *ZRB* kwa nia ya kuwaibia wafanyabiashara.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala jengine la haki za mlipa kodi hazikuanishwa katika sheria ya usimamizi wa kodi. Hili Mhe. Salmin Awadh Salmin aliliulizia, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Ninachotaka kusema kwamba sheria hii imejikita katika masuala ya usimamizi na utaratibu wa ulipaji kodi.

Mhe. Spika, suala la haki za walipa kodi ni muhimu, lakini linashughulikiwa na sheria nyengine ya rufaa za kodi Nam. 1 ya mwaka 2006 iliyopitishwa na Baraza lako tukufu imebainisha haki zote mlipa kodi ikiwemo kupinga maamuzi yaliyofanywa na kamishna juu ya sheria zote zinazosimamiwa na *ZRB*.

Mhe. Spika, wajumbe wengi walionesha wasi wasi wao juu ya uwezekano wa kugongana kwa sheria ya usimamizi wa kodi na sheria nyengine. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja alizungumzia, Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Ali Abdalla Ali. Ninachotaka kusema ni kwamba wakati wa maandalizi wa sheria hii suala la kugongana kati ya sheria hii na sheria nyengine lilizingatiwa na kwamba hakuna mgongano wowote uliopo kati ya sheria zinazosimamiwa na taasisi nyengine.

Hilo tumelizingatia na tumejaribu kwa uwezo wetu kuondosha hiyo migongano inayoweza kutokea. Lakini labda watu hawafahamu kwamba kodi hii inapaswa

ilipwe wapi kwa hizi tafsiri zetu mbili. Mhe. Spika, hilo kama nilivyosema tutajitahidi kuhakikisha kwamba haya tunatoa taaluma kwa walipa kodi wetu. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba walipa kodi wetu wengi sasa wameshafahamu na wanatekeleza ipasavyo, ndio maana utaona zile asilimia zetu za utekelezaji kwa kweli ni nzuri tu.

Mhe. Spika, mawasiliano kati ya *ZRB* na taasisi nyengine ziimarishwe. Ushauri huo umetolewa na tumeupokea na tunaona ni muhimu kwani lazima inafaa tuimarishe mawasiliano kati ya *ZRB* na taasisi nyengine. Ushauri huu ulitolewa na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wote walizungumzia suala hili.

Mhe. Spika, kwa kiasi kikubwa *ZRB* imepiga hatua kwa kuimarisha mawasiliano na taasisi nyengine hususan taasisi zinazohusiana na biashara, utalii, uwekezaji na vyombo vya ulinzi na usalama. Hata hivyo, maoni ya wajumbe yatazingatiwa katika kuimarisha mawasiliano kwa lengo la kuongeza ukusanyaji.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la kodi ya *income tax* kwa wafanyakazi wa muungano waliopo Zanzibar kulipwa Zanzibar. Hili nakumbuka tokea wakati wa bajeti tuliwahi kupewa fikra hii na katika mswada huu Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi walizungumzia suala hili. Mhe. Spika, ni kwamba tunakubali na nathubutu kusema kwamba kwa kiasi kikubwa *ZRB* imepiga hatua kwa kuimarisha mawasiliano na taasisi nyengine. Hata hivyo, nataka kusema kwamba suala hili linafanyiwa kazi na serikali. Aidha, eneo hili ni moja kati ya mambo yaliyotolewa mapendekezo na tume ya pamoja ya fedha.

Kwa hivyo, haidhuru kwamba tunachelewa lakini bora kwani haya masuala ni mazito na ni nyeti pia haya yanaendana na katiba kwani ukifungua Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesema kodi hizi zinapaswa zilipwe wapi. Mhe. Spika, kama nilivyosema haya tunayashughulikia na Mhe. Hija Hassan Hija aliuliza suala la *GFC* basi tumo tunakwenda nalo na hatma yake tutaliwasilisha kwa Waheshimiwa Wajumbe hapa ili tupate michango yao.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala zima la *tin* tuliulizwa hapa nakumbuka sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja yeye aliuliza kwamba ni nani anayestahiki kuwa na *tin*?

Mhe. Spika, suala la *tin* tunasema kwamba kila mfanyabiashara, mlipa kodi na yeyote atakayekuwa anaingiza chombo cha moto nchini anatakiwa kuwa na *tin*. Huo ndio utaratibu wake. Kuwepo kwa kumbukumbu za walipa kodi katika mtandao wa kompyuta hili Mhe. Haji Mkema Haji alisisitiza sana suala hili.

Mhe. Spika, tunamshukuru na anasema kwamba kwa upande wa *ZRB* katika kuweka kumbukumbu za walipa kodi inatumia mitandao mbali mbali yaani *computer software's* ikiwemo *VIMS* kwa walipa kodi *VAT*, *PIMS* kwa walipa kodi wa mafuta na *CMVRS* kwa ada za usajili wa vyombo vya moto, leseni za njia na leseni za udereva. Aidha, *ZRB* ipo njiani kukamilisha mtandao wa walipa kodi wadogo wadogo wanaolipa ushuru wa *stamp* na hoteli.

Vile vile Mhe. Haji Mkema Haji alizungumzia suala zima la usajili kwamba ni muda mfupi na mpito. Nataka kusema kwamba lengo kuu la usajili wa muda ni udhibiti wa walipa kodi wakubwa ambao mara nyingi huwa wameshinda *tender* au zabuni zenye thamani kubwa kwa ajili ya kuja kutoa huduma au kuuza bidhaa nchini kwa kipindi maalum, na makaazi yao ya kudumu sio Zanzibar. Hivyo, kwa kipengele hiki kinawafanya walipe kodi kutokana na biashara au huduma wanayoitoa nchini hata kama kwa muda mfupi, kipengele hiki huwa kinatumika kwa wakandarasi na washauri elekezi.

Mhe. Spika, pia Mhe. Haji Mkema Haji alizungumzia lile suala mara linaulizwa kuhusu utitiri wa walipa kodi uliopo Zanzibar kwa wafanyabiashara. Mhe. Spika, ukweli ni kwamba serikali imekuwa ikipata mapato yake kupitia vianzio mbali mbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake za kila siku. Kodi na ada hukusanywa nchini kupitia serikali kuu na taasisi zake kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi. Hivyo, ada hutozwa kutokana na huduma zinazotolewa na taasisi husika. Pia Mhe. Haji Mkema Haji aliulizia je, taasisi zote zinatumia sheria hii kwa upande wa utoaji wa leseni za biashara kwa Kamishna ndiye atakayekuwa akitoa maamuzi ya mwisho.

Mhe. Spika, naomba kusema kwamba kila mfanyabiashara atakuwa analipa kodi kwa mujibu wa biashara anayofanya. Hivyo leseni zitatolewa kwa mujibu wa biashara itakayokuwa inafanywa. Kwa mfano, Kamisheni ya utalii itatoa leseni inayohusiana na biashara yake ya utalii na vile vile atawajibika kusajiliwa na *ZRB* kwa ajili ya kulipa kodi za serikali. Kwa sababu hatutaki yale mapato yatapakae ni lengo letu kwamba mapato yote yalipwe pahali pamoja, lakini *authority* ya kutoa leseni tunawaachia wenyewe taasisi husika na tutakaa pamoja na wao watakuwa na *authority* kamili kwa yule anayepewa. Si kweli kama ikisemwa kwamba labda pesa zinalipwa kwengine wao watakuwa hawana meno, ni kwamba hatuna mtizamo huo. Mimi nafikiri tutashirikiana kwa pamoja kufanikisha lengo kwamba kodi ipatikane na kazi au huduma zao ziende kama zinavyopaswa.

Mhe. Asaa Othman Hamad na Mhe. Ali Suleiman Ali waliuliza kwamba kwa nini bidhaa zinazotoka Zanzibar zinatozwa kodi tena Tanzania Bara. Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba hili tatizo ni sugu na serikali kupitia Kamati yetu ya Pamoja ya Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Waziri Mkuu imekuwa ikilifanyia kazi kwa muda mrefu na tayari tumefika hata kuunda kamati na watendaji wetu wakakaa wakatafakari na wakatembelea Bara na nafikiri bado kuna mambo wanayazingatia kabla ya kuwasilishwa kwenye kikao kijacho cha viongozi wetu. Kama ninavyosema kimsingi pale tunapozungumza watakubali wenzetu siku mbili tatu litatekelezwa baada ya muda mfupi wanarudi kibao kile kile. Nafikiri tunazungumza na baada ya kufanya utafiti kuweza kupata *solution* juu ya suala hili.

Mhe. Spika, Mhe. Asaa Othman Hamad pia aliuliza mapato yanayokusanywa na taasisi za muungano mfano, *TCRA* hayanufaishi Zanzibar. Nataka kusema hapo nyuma ni kweli tulikuwa na tatizo hilo lakini sasa mapato haya tayari tunayakusanya na tunayatumia hapa Zanzibar. Tulikuwa na tatizo hilo huko nyuma lakini sasa hivi tumeanza kuzungumza na wenzetu na wametufahamu kwa mantiki ile ile kama tunavyokusanya kodi zile za *TRA* za hapa Zanzibar basi kodi hizi nazo tunataka tuzikusanye hapa hapa.

Vile vile Mhe. Asaa Othman Hamad pia aliuliza kwamba kusiwe na matumizi mabaya ya misamaha ya kodi. Hilo tunakubaliana nae kwa kweli wizara na serikali imekuwa ikijitahidi kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha ya kodi kwa lengo la kuhakikisha ukusanyaji mzuri wa mapato.

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba ni kweli tumegundua kama kuna wenye mahoteli wanauza wanafanya kama biashara, mwaka huu wanauza baada ya miezi sita anakuja mwengine anauza, anakaa miaka miwili akishakupata faida anauza anakuja mwengine huwa hawarudi tena serikalini hasa kwenye taasisi yetu ya *ZIPA* kujiandikisha au kufuata utaratibu. Hilo tumeliona na tunalifuatilia na nafikiri tutajitahidi kuona wapi tunaweza tukafikia katika kulipatia ufanisi. Nawaomba sana waheshimiwa tusaidiane kwa sababu wengi hasa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na wengine walioko katika mitaa ile ya utalii, unajua hawa wanafanya mambo haya kisirisiri hata unakuja kutahamaki basi muda umeshapita. Lakini kama ninavyosema na vyombo vyetu vinajitahidi kufuatilia kuona kwamba kila penye mwanya wa kodi kutokulipwa ipasavyo basi tunaziba.

Mhe. Spika, tulizungumza mapema hili suala la kuchelewa kuwasilishwa kwa mswada hapa Barazani. Nafikiri sina haja ya kulirejea tena kama nilivyosema naomba radhi tu kwamba kwa bahati mbaya mwaka huu kutokana na hasa na

ugumu na mtiririko wenyewe ndio umesababisha tuchelewe, hilo tutajipanga vizuri serikalini tuone kwamba halitotokea tena na tunalifanikisha.

Mhe. Ame Mati Wadi yeye alitaka kujua marekebisho ya sheria hii inamlenga na kumnufaisha nani? Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba mswada huu hautomuongezea mzigo yeyote kati ya mfanyabiashara au mlaji, isipokuwa lengo ni kumrahisishia mlipa kodi utaratibu wa uwajibikaji pamoja na mkusanyaji. Sisi tumerekebisha ule mtiririko tu basi ili kuweza kurahisisha yale mambo yaende kwa upesi na kwa ufasaha, hatukubadilisha kitu sheria ndio zile zile. Mabadiliko haya hajaongeza kiwango cha kodi yoyote kwa hivyo mheshimiwa usiwe na wasi wasi wowote. Pia tunakuomba sana utusaidie kwani wewe uko kwenye mahoteli uwaelimishe jamaa wasije wakashtuka kusikia kama tumebadilisha kitu, sio hivyo ila sisi tumejaribu kuweka mambo yaende vizuri tu.

Mhe. Spika, pia Mhe. Ame Mati Wadi ametaka kujua kutoa ufafanuzi kuhusu masharti ya ridhaa ya kulipa kodi. Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba kumejitokeza makosa katika kutafsiri kutoka mswada wa Kiengereza na ile ya Kiswahili. Mhe. Spika, ibara hii ilipaswa isomeke masharti ya uthibitisho wa kulipa kodi, sio kama ilivyosemeka na kila inaposomeka ridhaa ya kulipa kodi ilipaswa isomeke uthibitisho wa kulipa kodi. Kwa hivyo, tunaomba radhi na ndio hayo makosa tuliyoyapata wakati wa *drafting* ya huu mswada, unajua kutafsiri kutoka Kiengereza kuja Kiswahili ina kazi kidogo na inataka utulivu na umakini mkubwa kabisa. Mhe. Spika, nashukuru kwamba tumeifanikisha hiyo kazi kwa hivyo hasa kilichokusudia Mhe. Mwakilishi ni hilo.

Vile vile Mhe. Ame Mati Wadi alitaka kuuliza kuhusu uteuzi wa mawakala wa kukusanya kodi utegemee uwezo na sifa na sio kujuana. Mhe. Spika, ni kweli mawakala waliotajwa ni kwa ajili ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). Mawakala hawa ni wafanyabiashara wenye manunuzi makubwa pamoja na taasisi za serikali sio wengineo.

Mhe. Zahra Ali Hamad tunakushukuru sana kwa michango yako naamini mwisho wa wiki ulijipinda kweli kweli kuupitia huu. Kama ulivyosema mwenyewe kama muda mfupi lakini naona sio mfupi kwako, ulifanya kazi nzuri sana ya kuupitia na michango yako tumeipokea na kwa kweli tumeifanyia kazi vizuri.

Kuhusu ufafanuzi wa vifaa vya kuhifadhia bidhaa zitakazopaswa kusajiliwa. Mhe. Spika, kama ilivyo ndani ya sheria hii vifaa ambavyo vitahitajika kusajiliwa vitaanishwa katika kanuni chini ya sheria hii. Hata hivyo vifaa hivyo havitahusisha bidhaa kama vile freezer, friji, kontena na kadhalika aa, hizo zitatoka kwenye kanuni zitawekwa vizuri kabisa.

Mhe. Spika, Mhe. Zahra pia kwenye kifungu cha 15(1) alisema hakitekelezeki kwa mazingira ya biashara ya ya Zanzibar. Nataka kusema kwamba, kifungu hiki kinahitaji mtu anapobadilisha biashara au eneo la biashara, atapaswa kumtaarifu Kamishna. Utaratibu huu hauhusu mabadiliko ya aina ya bidhaa anazouza, wewe ukiondoka kutoka steshini moja kwenda nyengine ndio unatujuilisha pako hivi, basi, hauhusu mabadiliko yako ya bidhaa. Ndio ninaposema tutofautishe biashara sio bidhaa, hapa ndicho tunachokikusudia hasa.

Pia alisema kwamba serikali haiangalii sababu za kushindwa mlipa kodi kulipa kodi kwa wakati. Ninachotaka kusema ni kwamba serikali lengo lake ni kujaribu kuziba mianya ya ukwepaji na uepukaji wa kodi, hilo ndio suala la msingi kabisa. Najua utamaduni wa kulipa kodi kwetu umekuja hivi karibuni na tunashukuru wafanyabiashara wetu wameupokea vizuri sana na leo *Alhamdulillah* nathubutu kusema kwamba tunajiendesha kwa kiasi kikubwa sana kwa mapato yetu haya ya kodi. Lakini bado kuna wafanyabiashara wengine wajanja, na tukiregea basi tena wanachukua pakubwa. Kwa hivyo, tukiregea au tukiruhusu kila mtu alipe kwa tarehe anayotaka kodi haitakusanyika, mishahara hatutaweza kulipa, serikali haitokwenda, lazima serikali isimame kama serikali bwana, tarehe imewekwa na bodi yetu hii kwa hivyo makusanyo yote yafike wakati ule na yafanywe hivyo. Mtu akichelewa tena hapo ndio zile *penalty* zinafanya kazi.

Sasa hii ningekuombeni sana Waheshimiwa tusaidiane tuwaelimishe wenzetu, kama si hivyo hii kodi haitopatikana kila mmoja atakaa nazo mfukoni mpaka anapoona sasa hivi nimeshapungukiwa na matumizi ndio akalipe kodi, hivyo hatutokwenda.

Mhe. Spika, nisema kwamba hoja nyingi alizozisema Mhe. Zahra nimezigusa, neyngine nafikiri ulikuwa ushauri na tumeuchukua na kuufanyia kazi.

Mhe. Hija Hassan Hija alisema kwamba mswada umezingatia vipi hivi kodi zinazokusanywa na Serikali ya Muungano wa Tanzania kama vile meli ya uvuvi iliyokamatwa karibuni wakati wa uvuvi. Uvuvi ni jambo la Muungano? Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali mswada huu umelenga kurahisisha usimamizi wa sheria zinazosimamiwa na *ZRB* tu. Mswada huu hauhusishi sheria za Muungano.

Kuhusu mfano alioutoa Mhe. Hija angefaa kurejea jadweli ya kwanza na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoorodhesha mambo ya Muungano. Uvuvi si miongoni mwa mambo yaliyoorodheshwa na hivyo sio suala la Muungano. Hata hivyo, kwa kutambua haja ya kuratibu kwa pamoja

uvuvi katika Bahari Kuu hususan katika eneo la Tengefu la kiuchumi yaani hii *ZEC* Serikali zetu mbili zilikubaliana kusimamia kwa pamoja suala la uvuvi wa bahari kuu. Kwa upande mwengine suala alilozungumza Mhe. Hija ni shauri linaloendelea kusikilizwa mahakamani ambapo hukumu bado haijatolewa.

Mhe. Hija pia aliulizia mswada umezingatia vipi migongano ya sheria za *VAT* na SMT na hususan kwa kampuni za simu. Mhe. Spika, hakuna mgongano wowote wa sheria za *VAT*. Suala la utozaji kodi wa kampuni za simu ni la utendaji zaidi na tayari kwa kiasi kikubwa limeshazungumzwa na kutatuliwa kwa pamoja kati ya *ZRB* na *TRA*.

Pia Mheshimiwa alitaka kujua mafanikio yoyote yaliyoonekana kutokana na kuanzishwa kwa tume ya pamoja ya fedha. Yapo Mhe. Hija, ingawa suala hili halihusiani na mswada huu uliowasilishwa, hili ni suala jengine ambalo limekuwa likijitokeza sana katika siku za karibuni. Ni kweli kwamba bado haijaonekana athari ya kuanzishwa kwa tume hiyo, hata hivyo kutoonekana huko si kwa sababu ya kutokufanya kazi kwa tume, bali kumetokana na sababu nyengine kadhaa ikiwemo upya wa tume ambako hakukuwa na utaratibu bayana ndani ya serikali wakishughulikia mapendekezo ya tume pale yanapotolewa.

Kwa sasa serikali zetu mbili zinakubaliana kuwa kila upande hupitia mapendekezo haya na hatimae ijadiliwe kwenye kikao cha Mhe. Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu chini ya Uenyekiti wa Mhe. Makao wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mapendekezo hayo yameshafanyiwa kazi na tuko tayari kwa majadiliano na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, nafikiri itafikia kikomo kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa masuala yao na hoja zao pamoja na fikra zao walizochangia kufanikisha mswada huu. Kama walivyosema mswada ni wa marekebisho na yale yote yaliyotuelekeza tutayafanyia kazi na hatimae kupata ufanisi tuliotaka katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya kama nimesahau hoja ya mtu naomba tuje tubadilishane mawazo zaidi na wizara tuko tayari kufanikisha hayo kwa manufaa ya nchi yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, 2009

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Kutumika
Kifungu 3 Ufafanuzi
Kifungu 4 Tathmini ya Kodi na Marekebisho yake

Sehemu ya Pili
Usajili na Kufuta Usajili

Kifungu 5 Usajili
Kifungu 6 Maombi ya usajili.
Kifungu 7 Usajili kukataliwa, kuzuiliwa na kufutwa usajili na marekebisho yake.
Kifungu 8 Usajili wa muda.
Kifungu 9 Cheti cha Usajili.
Kifungu 10 Kuweka jina la biashara.
Kifungu 11 Kusajiliwa.
Kifungu 12 Maombi ya kufutwa usajili.
Kifungu 13 Usajili wa mpito na marekebisho yake.
Kifungu 14 Usajili wa vifaa vya kuhifadhia biashara.
Kifungu 15 Taarifa ya mabadiliko na marekebisho yake.

Sehemu ya Tatu
Masharti ya Uthibitisho wa Kulipa Kodi

Kifungu 16 Masharti ya uthibitisho wa kulipa kodi na marekebisho yake.
Kifungu 17 Wajibu wa mamlaka ya leseni.

Sehemu ya Nne
Makisio na Marekebisho ya Kodi

Kifungu 18 Marekebisho ya kodi
Kifungu 19 Uwezo wa kufanya tathmini
Kifungu 20 Yaliyomo katika tathmini
Kifungu 21 Taarifa ya tathmini na marekebisho yake.

Sehemu ya Tano
Kumbukumbu, Nyaraka na Ukaguzi

Kifungu 22 Kumbukumbu za hesabu na marekebisho yake.
Kifungu 23 Ankara ya kodi na risiti.
Kifungu 24 Kodi kuonesha katika Ankara ya kodi au risiti.
Kifungu 25 Bei iliyotangazwa kujumuisha kodi.
Kifungu 26 Ukaguzi na uchunguzi na marekebisho yake.
Kifungu 27 Kujifanya kuwa afisa.
Kifungu 28 Taarifa ya kupata nyaraka na maelezo.
Kifungu 29 Uwezo wa kuchukua na kutoa nyaraka
na marekebisho yake.
Kifungu 30 Kutoa taarifa.

Sehemu ya Sita
Malipo ya Kodi

Kifungu 31 Tarehe ya malipo ya kodi na marekebisho yake.
Kifungu 32 Malipo ya mapema.
Kifungu 33 Riba na marekebisho yake.
Kifungu 34 Aina ya fedha kwa malipo na marekebisho yake.
Kifungu 35 Mfumo maalum wa hesabu na marekebisho yake.
Kifungu 36 Kurejesha na kufuta malipo.
Kifungu 37 Kutozwa kodi ya ziada.

Sehemu ya Saba
Kurejesha Kodi

Kifungu 38 Kodi kuwa ni deni la serikali.
Kifungu 39 Taarifa ya ukumbusho.
Kifungu 40 Malipo kwa awamu.
Kifungu 41 Malipo yanayofanywa na mtu wa tatu.
Kifungu 42 Taarifa ya malipo kwa mtu wa tatu.
Kifungu 43 Kufunga biashara na marekebisho yake.

Kifungu 44 Kujilipa.
Kifungu 45 Bakaa ya deni la kodi
Kifungu 46 Kuzuia bidhaa.

Sehemu ya Nane
Uongozi

Kifungu 47 Kuchukuliwa sampuli.
Kifungu 48 Tathmini kwa taarifa ya kikazi.
Kifungu 49 Wajibu wa kutunza siri na marekebisho yake.
Kifungu 50 Uteuzi wa wakala wa kuzuia kodi.
Kifungu 51 Kutia alama kwa bidhaa inayosafirishwa.
Kifungu 52 Msaada wa polisi.

Sehemu ya Tisa
Masharti Mengineyo

Kifungu 53 Kukwepa kulipa kodi.
Kifungu 54 Kosa la kampuni.
Kifungu 55 Adhabu ya jumla.
Kifungu 56 Kumaliza kosa na marekebisho yake.
Kifungu 57 Kuacha kulipa adhabu au riba.
Kifungu 58 Kutangaza majina.
Kifungu 59 Kukasimu madaraka.
Kifungu 60 Ukomo wa kuwajibika.
Kifungu 61 Rufaa.
Kifungu 62 Mtu kufanya kazi kama mwakilishi.
Kifungu 63 Wakala na marekebisho yake.
Kifungu 64 Biashara baada ya kufilisika au kufariki na marekebisho yake.
Kifungu 65 Kipaumbele kwa deni la kodi kwa mtu aliyefilisika.
Kifungu 66 Kupeleka taarifa na marekebisho yake.
Kifungu 67 Uwezo kuhusiana na bidhaa iliyoingizwa na kusafirishwa na marekebisho yake.
Kifungu 68 Uwezo katika kukusanya mapato ya serikali.
Kifungu 69 Kanuni.

Sehemu ya Kumi
Marekebisho Yatokanayo

Kifungu 70 Marekebisho ya sheria ya ongezeko la thamani.
Kifungu 71 Marekebisho ya sheria ya kodi ya ushuru wa stempu.
Kifungu 72 Marekebisho ya sheria ya kodi ya hoteli.

Kifungu 73 Marekebisho ya sheria ya kodi za huduma za bandari.
Kifungu 74 Marekebisho ya sheria ya kodi za mafuta.
Kifungu 75 Kubakiza na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeupitia Mswada huu wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na mambo yanayohusiana nayo pamoja na marekebisho yake kifungu kwa kifungu na kuukubali, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi ya 2009

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa kuendesha shughuli zetu za Baraza na vikao vyetu mbali mbali. Waheshimiwa Wajumbe wiki iliyopita tulipokuwa tunakutana katika *briefing* tulimuomba Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naye afanye utaratibu wa kufanya semina na alisema kwamba atalifanyia kazi. Semina kwa pale iliombwa haraka haraka ilikuwa kuhusu masuala ya Benki ya Damu.

Lakini pia kwa sababu ya mswada ambao utawasilishwa mbele yetu wiki hii wa madawa ya kulevya, nao wamezingatia kwa uzito na urefu wake basi ungefaa kufanyiwa semina. Amekwenda mbia za ajabu sana ili kutafuta utaratibu wa uwezekano wa kufanya semina hiyo. Hivyo, naomba nitoe taarifa kwamba Mhe. Waziri wa Afya sasa yuko tayari kuweza kufanya semina kwa ajili ya mswada huo wa madawa ya kulevya kabla ya kuwasilishwa. Lakini pia katika semina hiyo hiyo atoe ajenda inayohusiana na masuala ya Benki ya Damu ambayo tuliomba wiki iliyopita.

Kwa hivyo, naomba niwape taarifa kwamba semina kuhusu mswada huo pamoja na masuala ya Benki ya Damu itafanyika hapa katika Baraza la Wawakilishi siku ya Jumatano tarehe 21/10/2009 mara baada ya kipindi cha mswali asubuhi. Siku hiyo ataeleza kwa mapana kabisa juu ya masuala ya mswada ule ambao ni mgumu kidogo, pia kuhusu masuala ya Benki ya Damu ambayo wiki iliyopita tulimuomba sana Mhe. Waziri.

Sasa ameniomba nitoe taarifa hii na itoshe kwamba taarifa hii ndio mwaliko wenyewe kwa sababu muda wenyewe ni mfupi. Anahangaika kutayarisha makabrasha na kila kitu siku ya Jumatano mara baada ya kipindi cha maswali tutafanya semina hiyo *Inshaallah.* Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya kwa kuwa msikivu na kuchukua hatua pale anapoombwa na Waheshimiwa Wajumbe.

KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa leo tumemaliza shughuli zetu mapema kabla ya wakati naomba uliahirishe Baraza lako tukufu hadi kesho Jumanne ya tarehe 20 Oktoba, 2009 saa tatu asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wangu wa upande wa mkono wangu wa kushoto wao wako tayari tuendelee na kazi. *(Kicheko)*

(Saa 12:15 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 20/10/2009 saa 3:00 asubuhi)